ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kwanza – Tarehe 23 Machi, 2011

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kukutana hapa, katika shughuli zetu hizi za Baraza Mkutano wa tatu Kikao cha kwanza, Tarehe 23 Machi, 2011.

Pili niwashukuru wajumbe wote kwa niaba ya wenzangu wenyeviti Mhe. Mahamoud na Mhe. Mgeni kwamba baada ya kuchagua hatukupata muda wa kutoa shukurani, leo kwa niaba ya wenzangu na mimi mwenyewe binafsi, tunashukuru kwa imani mliyotuonyesha na sisi tunaahidi kwenu kwamba kazi hii tutaifanya na Mwenyezi Mungu atatusaidia kwa kufuata kanuni, sheria na katiba ya nchi yetu.

Baada ya kusema hayo mafupi nawashukuru ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mizani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 29 Januari, 2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Kipindi cha mwaka 2008/2009. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na
Mashirika (PAC) (Mhe. Omar Ali Shehe): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Kipindi cha Mwaka 2008/2009. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6 ya 2001 na Kuweka Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. (Mhe. Amina Iddi Maboruok): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6 ya 2001 na kuweka Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu ya Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 21

Matumizi ya Fedha za Mauzo ya Viza

Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Aliuliza:-

Kwa kuwa fedha za mauzo ya Visa kwa wageni wanaokuja Zanzibar zinatakiwa zitumike hapa hapa Zanzibar kwa maslahi ya Wazanzibari. Na kwa kuwa katika siku za hivi karibuni kumekuwa na mtindo wa baadhi ya Balozi zetu zilizoko nchi za nje kuuza Visa huko waliko. Na kwa kuwa fedha za mauzo hayo kwa wageni wanaokuja Zanzibar huwa haziletwi hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali haioni kwamba mapato hayo yanapotea.

(b) Kwa kuzingatia upotevu wa mapato ya Wazanzibari na huku wakiitegemea Serikali yao kuwatetea katika maslahi yao. Je, Serikali haioni kwamba, kulinyamazia kimya jambo hilo ni kutowajibika ipasavyo.

(c) Je, Serikali itachukuwa hatua zipi ili kuhakikisha pesa za walipa kodi wetu hazipotei kiholela.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 21 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, mapato ya maduhuli yanayotokana na *VISA* kwa wageni wanaoingia nchini yanasimamiwa na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kupitia Balozi zetu ina jukumu la kukusanya mapato hayo kwa wageni wanaoomba *VISA* ya kuingia nchini. Maamuzi ya kwamba malipo ya maduhuli kwa ajili ya *VISA* yafanyike katika Balozi zetu au kulipwa na wageni wanapoingia nchini yanatokana na makubaliano kati ya nchi na nchi. Kwa mnasaba huo, mgeni anapotaka kuja nchini ama huchukua *VISA* katika Ofisi zetu za Ubalozi zilizoko nje ya nchi au kuchukua *VISA* anapowasili nchini *(VISA on arrival).* *VISA* anayopatiwa mgeni inamruhusu kuingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla wake. Kwa hivyo, mgeni anaweza kuingia nchini kwa kupitia Zanzibar na baadaye akaelekea Tanzania Bara kwa kutumia *VISA* hiyo hiyo na kinyume chake.

Aidha, kutokana na makubaliano yaliyopo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mapato yote yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar yanayotokana na mauzo ya *VISA*, vibali vya ukaazi au kufanya kazi nchini, na mapato mengineyo yanabakia Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Mapinduzi. Ni vyema ikaeleweka kuwa mbali na mapato ya *VISA* yanayotokana na mgeni kuingia nchini, Serikali pia hukusanya mapato mengine yanayotokana na kodi mbali mbali na matumizi mengine atakayoyafanya mgeni.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli lipo tatizo la kupata taarifa kamili juu ya ulipaji wa maduhuli ya fedha kutoka Ofisi zetu za Ubalozi zilizo nje. Hata hivyo, Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inawasiliana na Uhamiaji ili kupatikana taarifa juu ya wageni wanaoingia Zanzibar na kujua ni wangapi wanaolipia fedha za *VISA* katika Ofisi za Ubalozi zetu zilizo nje. Usahihi wa taarifa hii utapelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuatilia fedha zinazostahiki kulipwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kuchukua hatua ipasavyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali haiwezi kukaa kimya na itaendelea kuhakikisha kuwa mapato ya Serikali ya Mapinduzi yanapatikana kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kushirikiana na taaisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia kwa ukamilifu ugawaji wa mapato baina ya Serikali mbili kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kila upande unapata haki kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Waziri, kakiri kwamba kuna kasoro ya upatikanaji wa mapato kwa walii wanaokuja Zanzibar ambao wanachukulia visa katika balozi zetu za nchi za nje, pamoja na maelezo yake mazuri kwamba Wizara ya fedha inafanya juhudi za kuwasiliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulirekebisha hili, lakini haoni kuna sababu ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya juhudi ikahakikisha kwamba wale watalii wanaokuja hapa Zanzibar wasiuziwe viza kule na badala yake waji wachukulie hapa ili tuhakikishe kwamba hakuna kinachovuja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Kama nilivyosema awali kupatikana kwa visa inategemea pia makubaliano kati ya nchi na nchi, zipo nchi ambazo tumekubaliana nazo na wananchi wake wanapotaka kuja Zanzibar wanaweza kupata visa katika balozi zetu zilizopo katika nchi zao, kwa hivyo ikiwa nafasi hiyo ipo itakuwa ni vigumu kumlazimisha mgeni ambae anayo nafasi ya kuomba visa kupitia ubalozini kwetu katika nchi hizo kuwa lazima aje apate visa hapa Zanzibar.

Tunafurahi sana wale ambao watachukua visa zao watakapowasili hapa Zanzibar, lakini kwa wale ambao wataomba visa zao katika nchi zao vile vile hatuna budi tukubaliane nao kwa sababu ni utaratibu ambao tumekubaliana kati ya nchi na nchi, cha msingi hapa ni kuhakikisha kwamba mapato yanayostahiki Zanzibar kupata kwa kuchukuliwa hatua zinazofaa ili Zanzibar ipate mapato yake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa sauala hili kama alivyojibu katika suala mama kwamba hatua zinazofaa zitachukuliwa kushughulikia pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa suala hili la ugawanaji wa mapato ya aina hii ni kongwe sana, mwaka 2003

ilipitishwa sheria ya kuanzisha *Jounce finance Committee* na kwa kuwa 2006 ilianza kazi, yeye Mhe. Waziri atatueleza ni lini tutegemee matunda ya *Committee* hii ili ugawanaji wa mapato uweze kuwa ni suala la kawaida, na sio la kufuatiliwa tena.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Nataka kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba kamati ya pamoja ya mambo ya fedha imemaliza kutayarisha tipoti yake na hivi sasa iko katika serikali zetu mbili, mara baada ya kupitiwa na serikali zetu mbili, miongozo itatolewa ili utekelezaji uanze na mapato yagawanywe vizuri kila upande upate haki yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye vifungu a na b. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba mapato yanayotokana na visa yako chini ya balozi zetu ambayo yanaratibiwa na waasisi wa uhamiaji, lakini katika viwanja vya ndege na bandari Zanzibar wapo uhamiaji ambao kila mgeni anapoingia huchaji dola 38 na anapoondoka dola 53 na mapato haya huwa chini ya Uhamiaji fedha ambazo bado hupelekwa kwenye Serikali ya Muungano wa Tanzania. Naomba kuelezwa pia haya yako chini ya ubalozi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Katika suala langu la msingi nilieleza kwamba mapato yote yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar yanakwenda katika mfuko wa Hazina wa Zanzibar, kama kuna mapato yoyote yanakusanywa hapa Zanzibar na Idara ya Uhamiaji au TRA yanakwenda katika mfuko wa Hazina wa Serikali ya Mapindui ya Zanzibar.

Nam. 95

Watendaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Kupatiwa Mafunzo

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni kikosi muhimu sana. Kwa umuhimu wake watendaji wa kikosi hiki wanahitaji kupatiwa mafunzo mbali mbali.

(a) Ili kuinua uwezo wa watendaji hao, Je,Wizara huwa inawapeleka kujifunza katika vyuo gani vyenye sifa na kutambulika Kitaifa na Kimataifa.

(b) Je, Wizara imeshawapatia mafunzo watendaji wangapi na kwa asilimia ngapi ya walioko Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuhusu umuhimu wa Idara Maalum ya Zimamoto na Uokozi katika kutoa mafunzo kwa maafisa na wapiganaji wake. Mafunzo haya yanalenga katika malengo mawili, kwanza tunatoa mafunzo junsi ya kuukinga moto usitokee, pili mafunzo haya yanalenga kudhibiti au kuuzima moto hapo utakapotokea pamoja na shughuli za uokozi. Katika kutekeleza hili Idara Maalum ya Zimamoto na Uokozi imeanzisha Chuo chake cha Mafunzo hapo Kitogani kwa ajili ya kutoa mafunzo ya awali na Uongozi mdogo. Vile vile katika mipango yake ya baadae kuna nia ya kukikuza chuo hicho na kufikia hadhi ya kitaifa. Pia kwa nyakati tofauti Idara Maalum ya zimamoto na Uokozi hupeleka Maafisa wake kupata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi.

(b) Mhe. Naibu Spika, Idara Maalum ya Zimamoto na Uokozi imewapatia mafunzo wapiganaji 595 kuanzia mwaka 2001 hadi Machi, 2011 katika chuo chake cha Kitogani. Kati ya hao 400 walikuwa wakifanyakazi Unguja na 195 walikuwa wakifanyakazi Pemba. Aidha, Maafisa 8 wamepatiwa mafunzo nje ya nchi za China, Singapore, Uingereza, Japan na Sweden.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Idara ya Zimamoto pamoja na uokozi tunazifanya ndani ya visiwa na visiwa vyetu ni vidogo na vimezungurukwa na bahari.

a) Katika mafunzo haya yaliyotolewa tuna wazamiaji wangapi ambao wanaweza kufanya kazi ya uokozi baharini wakati hatari zinapotokea.

b) Je, waokozi hawa wamepewa zana ngapi na zipi za kufanyia kazi zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kwa bahati nzuri hii sekta ya uzamiaji iko katika kikosi chetu cha KMKM wao ndio wenye wataalam na wako makini kweli kweli, nikithibitisha hayo hata ilipozama meli yetu ya MV Fatihi walijitahidi kuzamia pale, lakini kutokana na mzigo uliokuwemo ndani ya meli walishindwa kuinyanyua. Juzi

pamoja na Mhe. Rais tulitembelea katika vikosi na tukaona zana walizokuwa nazo KMKM na tumesema ipo haja ya kuziendeleza zana zao.

Lakini pia wazo lako sio baya kwamba hata hawa vijana wetu wa Zimamoto basi mafunzo haya wangeyapata, kwa hivyo hilo tunalichukua na tutalifanyia kazi na mara nyingi yanapotokea mambo kama haya wanafanya *joint operation* kwa vikosi vyote vya KMKM na Zimamoto, lakini kama nilivyosema kwa shughuli za uzamiaji tuna *dives* wazuri sana na inashughulikiwa na kikosi cha KMKM.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa kazi ya kuzimamoto na kuokoa ni kazi ngumu inayohitaji ujasiri na kujitolea muhanga, hivi askari wetu wa Zimamoto kuna posho maalum wanayopata wakati wanapofanya kazi zile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nakubaliana nae kwamba kweli kazi wanayoifanya ni nzito na inataka ujasiri na ndio maana mafunzo ya awali hawa wapiganaji wa Ziamamoto wanatakiwa wafunzwe kijeshi ili wakomae na kuwa askari kamili. Suala la nyongeza au tunzo lipo na mara nyingi wanazawadiwa hata vyeo wale wanaofana vizri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu suala kama vikosi vyetu vya Zimamoto vimepata mafunzo ya kutosha na wamehitimu na sasa wako tayari kufanya kazi kama inavyotakiwa.

Je, tuna magari mengapi ya Zimamoto Unguja na Pemba, na Je, baada ya hayo magari ya kuzimia moto kwa sababu kuna maeneo mengine magari hayawezi kufika. Je, tuna zana gani nyengine za kuweza kufika zie sehemu ambazo magari hayafiki na kusima huo moto.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kikosi cha Zimamoto hivi sasa kina magari 18 kwa kazi za Zimamoto na uokozi, magari hayo yana vifaa aina tofauti naomba nikujulishe tu kwamba kuna vifaa vinaitwa *Air creftender* ziko tatu katika Uwanja wa Ndege wa Unguja, kuna *Air creftender* moja kwenye kiwanja cha ndege cha Pemba, kuna *Ambulance* mbili Uwanja wa Ndege Unguja, kuna *Ambulance* moja kiwanja cha Karume Pemba. Kuna gari la ngazi moja Mjini Unguja linaweza kwenda hata mita miambili juu kabisa, pia kuna gari la *creen* moja Unguja, kuna gari la kubebea maji moja Unguja. Kuna *pumper* moja Unguja, kuna *worterfom tender* moja Unguja, kuna *worterform tender* moja Chake Chake Pemba, kuna *worte tender* moja Kigunda Unguja. Kuna *pump* moja

Mahonda Unguja, kuna gari la maji Mahonda moja Unguja, kuna *woter tender* moja Kitogani Mkoa wa Kusingi Unguja na *pump* moja Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja. Kwa hivyo magari haya jumla yapo kumi na nane.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba sera moja kubwa ya kikosi chetu ni kwenda kisasa, kwa hivyo tuna magari ya kisasa kabisa kushughulikia masuala haya.

Nam. 1

Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Zanzibar:

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Wakati wa Uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi tarehe 11/11/2010 Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Moh'd Shein aliahidi kuimarisha maisha ya Wanawake kwa kuanzisha Benki ya Wanawake kama ilivyo kwa Tanzania Bara.

(a) Hadi hivi sasa ni hatua zipi ambazo Serikali imeanza kuchukua katika kutekeleza suala hili.

(b) Kwa kuwa jambo hilo lina manufaa makubwa kwa maendeleo ya wanawake wa Zanzibar, Serikali imekusudia kulitekeleza kwa muda gani.

(c) Ni wajasiriamali wangapi wa kike ambao wameweza kupata mikopo katika Benki zetu mfano *PBZ.*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Ali Mohamed Shein, alitamka katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 11/11/2010 wakati wa uzinduzi wa Baraza lako tukufu kuwa jitihada zitafanywa katika kuanzisha Benki ya Wanawake Zanzibar .

Mhe. Naibu Spika, msingi mkuu wa kuanzisha Benki ya Wanawake Zanzibar ni kuwawezesha wanawake ili waweze kushiriki kikamilifu katika uzalishaji na hatimae kuwapunguzia umasikini wa kipato.

Katika kulifanikisha suala hili, serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Kuzungumza na uongozi wa Benki ya Wanawake Tanzania juu ya utekelezaji wa suala hili kwa kutilia maanani kuwa wao tayari wana uzoefu.

- Kutafuta jengo ambalo litatumika kwa ajili ya shughuli za Benki hiyo juhudi hizi bado zinaendelea.

- Kufanya tathmini juu ya idadi na sifa za watumishi watakaoajiriwa katika kufanyakazi ndani ya Benki hiyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, uanzishwaji wa Benki kamili ya Wanawake unaweza ikachukua muda mrefu na unahitaji mtaji mkubwa. Kutokana na hali hiyo, serikali imeona ni busara kuanzisha Tawi la Benki ya Wanawake Tanzania hapa Zanzibar. Kama shughuli zote zitakwenda zilivyopangwa, tawi hilo litafunguliwa kabla ya mwisho wa mwezi wa Juni, 2011.

(c) Mhe. Naibu Spika, wajasiriamali wa kike waliopata mikopo kutoka PBZ hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2011 walikuwa ni 267, hii ni sawa na asilimia 40 ya watu binafsi waliokopa PBZ. Idadi hii haijumuishi wajasiriamali wa kike waliomo katika vikundi vya *SACCOS* ambao wamekopa kupitia vikundi hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri kwamba mtaji wa kufungua Benki ya Wanawake ni mkubwa. Taarifa ambazo tunazo ni zaidi ya shilingi bilioni 12 kwa kuanzia kufungua benki hiyo. Na kwa kuwa serikali imesema inazungumza na Benki ya Wanawake Tanzania kuja kufungua tawi hapa Zanzibar.

Je, faida itakayopatikana ni kwa ajili ya wanawake wa Zanzibar au wa Tanzania Bara.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, uwanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania umeanzishwa kwa misingi miwili.

Kwanza Benki ile kuna wananchi wa Tanzania wana-*share* katika Benki ile. Nathubutu kusema hata mimi Mhe. Naibu Spika, nina hisa kidogo katika benki ile.

Pili Serikali yetu ya Muungano nayo ina hisa katika benki ile. Kwa maana hiyo faida itakayopatikana katika kufanya biashara za kibenki kupitia Benki ya Wanawake wa Tanzania itagawiwa kwa wana hisa kulingana na hisa zao. Na mimi naiombea dua Benki hii ifanye vizuri, hizo hisa kidogo nilizonazo na mimi nipate gawio.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri amejibu kwamba kuna mpango wa kuanzishwa Benki haraka haraka kwa ajili ya kuwaondolea matatizo wanawake. Amesema kwamba Mwenyezi Mungu akipenda itaanzishwa tawi lake hapa Zanzibar.

Je, kwa sababu ya kuwaondolea usumbufu wanawake, sisi Zanzibar ni visiwa viwili yaani Unguja na Pemba katika taratibu hizo ili kuwaondolea usumbufu wanawake waliokuwepo Pemba na kule Pemba litaanzishwa tawi kama hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Zanzibar ni visiwa viwili Unguja na Pemba lakini uanzishwaji wa Benki yoyote ile kwanza unaanzishwa katika sehemu moja, ili benki ile iweze kukua na baadaye inatambaa katika maeneo mengine. Nataka nimwambie Mhe. Subeit kwamba hata Tanzania Bara Benki ya Wanawake kwa sababu ndio kwanza imeanzishwa ina umri wa miaka miwili na kidogo matawi yake yapo Dar-es-Salaam kwanza na Zanzibar linakuja. Tuombe Mungu, sote tujiunge na benki hii tununue hisa ndani ya benki hii ili iweze kukua. Matumaini yetu siku za baadaye na Pemba tutawaomba wenzetu wapeleke tawi la Benki hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri aliyotoa Mhe. Waziri, napenda nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa sera ya Benki Kuu ni kuanzishwa kwa Benki za kijamii, haoni kwamba kuwa ukombozi wa Zanzibar kwa wanawake ni serikali kuchukua juhudi ya kuwafanya wakaanzishwa hizi Benki za Kijumuia, kuliko kuanza tena kujiingiza katika mabenki makubwa kama hayo ambayo yana malengo makubwa na riba ni lazima itakuwa kubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, serikali inatilia mkazo sana uwazishwaji wa benki za jamii *(Community Development Bank)* na haikatazi. Jamii yoyote ile inaweza ikajikusanya na kuanzisha Benki yao ilimradi inazingatia misingi ya uwazishwaji wa Benki hiyo. Mtu mmoja katika uwazishwaji wa Benki hiyo hawezi akamiliki zaidi ya hisa asilimia 20.

Kwa maana hiyo benki ya jamii inaweza ikaanzishwa na watu 5 kila mmoja akamiliki hisa asilimia 20 sio zaidi, lakini unatakiwa uwe na mtaji wa shilingi milioni 500. Lakini katika uwazishwaji wa benki za jamii serikali haitakiwi itie pesa yake. Kwa misingi hii serikali haiwezi ikaanzisha benki za jamii lakini wananchi wanaweza kuanzisha benki za jamii. Nitawaomba sana wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba kuanza kuanzisha benki za jamii ili iwe ni faida kwao, kwa sababu hata viwango vya riba wataviweka kwa kuzingatia benki za kijamii badala ya hizi *Commercial Bank.*

Nam. 14

Usajili wa Kazi za Sanaa

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza**:-**

Baraza la Wawakilishi lilipitisha Sheria ya Hakimiliki na tayari hivi sasa Afisi imeshaanza kusajili kazi hizo na kufikia 1,389 kwa Unguja na Pemba kwa kuanzia mwezi Januari 2010 hadi mwezi Novemba 2010.

(a) Je, Mhe. Waziri taaluma gani imetolewa kwa jamii ili waweze kuitumia Afisi hiyo na kupelekea kutimiza malengo ya uanzishwaji wake.

(b) Kwa kuwa suala hili ni jipya Je, katika zoezi la usajili kazi hizo kuna ada yoyote anayolipa mwenye kazi au zoezi hilo hufanywa bure.

Mhe. Mwanasheria Mkuu – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Baraza la Wawakilishi limepitisha Sheria ya Hakimiliki Nam. 14 ya 2003 na imeshaanza kusajili kazi hizo Unguja na Pemba. Hata hivyo idadi sahihi ya kazi zilizosajiliwa kuanzia Januari hadi Novemba 2010 ni 596 tu na sio 1389 kama ilivyofikiriwa na Mhe. Mjumbe.

Mchanganuo wa kazi hizo ni kama ifuatavyo. Aina ya kazi ya idadi ya kazi.

AINA YA KAZI:	**IDADI YA KAZI:**
Miziki mbali mbali	45
Bongo Flavour	8
Gospel	2
Jazz	8
Qasida	13
Taarab	353
Zenj Flavour	48
Drama	17
Film	16
Documentary	2
Novel	4
Play	6
Poetry	17
Mawaidha	25
Maombi ya miradi *(projects write up)*	2
Michoro	30
JUMLA KUU	**596**

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kupitia Idara yake ya Hakimiliki imekuwa ikitoa taaluma hiyo kwa njia nyingi. Kwanza ni kwa kutumia TVZ kwa kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 3.45 usiku hadi saa 4.15 na kurejewa tena siku ya Alkhamis saa 12.00 jioni. Taalum hii kwa kupitia TVZ haikufanikisha sana hasa kwa Pemba kutokana na kukosekana kwa TVZ na pia umeme kwa wakati huo. Kwa upande wa mashamba hapa Unguja vile vile hatukufanikiwa sana kutokana na jamii kubwa kutokuwa na TV zao wenyewe au na jamii kutokuangalia vipindi vya aina hii.

Hata hivyo, Idara ya Hakimiliki imejitahidi kuendesha warsha kwa makundi mbali mbali kama vile maafisa wa serikali, wamiliki wa Hakimiliki na watumiaji wa kazi hizo nchini kote, Unguja na Pemba. Warsha hizi zilifanywa kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu *(WIPO – World Intellectual Property Organisation*), mfuko wa Utamaduni Tanzania Wizara ya Habari nakadhalika.

Taaluma nyengine ilitolewa ni kwa kutumia vipeperushi mbali mbali vikijumuisha elimu ya dhana ya hakimiliki, usajili wa hakimiliki, leseni za hakimiliki na umuhimu wake pamoja na kuwaelimisha wahusika wenyewe wa hakimiliki pale wanapofika afisini kwa kujisajili.

(b) Mhe. Naibu Spika, suala hili bado lingali jipya sana na wizara yangu inafanya kazi ya ziada ili jamii ielewe vyema umuhimu wa Hakimiliki na umuhimu wa kuzisajili. Kwa maana hiyo, hivi sasa hatutozi ada yoyote pale mwananchi anapokuja kwa kujisajili na kuisajili kazi yake. Idara yetu baada kuridhika kwa uhalali wa kazi ya mtu, na baada ya muombaji kutimiza taratibu zote zinazohusika basi muombaji huyo husajiliwa bure.

Nam. 3

Kampuni ya *Indigo Aviation* Kusita Kufanya Kazi Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:**

Miezi michache iliyopita, wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla walifurahia safari zao kupitia ndege za Kampuni ya *Indigo Aviation*, ndege ambazo zimeleta matumaini makubwa kwa wananchi wanyonge kwa unafuu wa bei zake. Hata hivyo, kwa sasa usafiri wa ndege za kampuni hii umesita.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea ndege hizi kusitisha safari zake hapa Zanzibar.

(b) Je, Wizara inaweza kutufahamisha mmiliki halali wa kampuni hiyo.

(c) Hivi sasa ndege za kampuni hii zipo pembeni mwa kiwanja cha ndege cha Zanzibar kwa muda mrefu, Je, zipo kwa ajili gani na zinatoa malipo yoyote kwa kuwepo kwake kiwanjani hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatavyo:

Mhe. Naibu Spika ni kweli kampuni ya Ndege ya *Indigo Aviation* ilianzisha safari zake hapa Zanzibar mnamo tarehe 26 Juni 2009 kwa kuanzia Dar es Salaam kupitia Zanzibar na Pemba na kutoa unafuu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar hasa wale wa kipato cha chini.

Aina ya ndege iliyokuwa ikitumia kampuni hii ni *DC3* ambazo kwa kiasi kikubwa zimeanza kuondoka katika soko la usafiri wa anga duniani. Ndege hizo bado zinaruhusiwa kuendelea kutumika ikiwa zitakuwa na hali nzuri na kufanyiwa matengenezo kila baada ya muda kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania na taratibu iliyowekwa na watengenezaji wa ndege husika.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya kutokana na kampuni hiyo kushindwa kuzihuisha vyeti vya ukaguzi vya ndege hizo *(renewal of certificate of Air worthiness)* na kukosekana kwa mkataba wa marubani wa ndege pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga kama ambavyo taratibu za Mamlaka zinavyoelekeza. Pamoja na hali hiyo ndege hizo zimekabiliwa na tatizo la kuharibika mara kwa mara. Mamlaka ya usafiri wa Anga Tanzania baada ya kuzifanyia ukaguzi ndege hizo iliagiza kusitisha safari zake na kutakiwa kuhuisha *Certificate of Air Worthiness* ndege hizo pamoja na kukamilisha taratibu nyengine za kuzifanyia matengenezo kabla ya kuruhusiwa kuruka. Kampuni hiyo hadi sasa haijaweza kukamilisha mahitaji hayo na bado ndege zake hizo zipo katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kueleza katika maelezo yangu yaliotangulia kampuni ya ndege ya *INDIGO* imesitisha safari zake hapa Zanzibar mnamo tarehe 15 Februari 2010 kutokana na sababu za kiufundi ikiwemo kukosekana kwa *Certificate of Air Worthiness* na mkataba baina ya marubani wa ndege za kampuni hiyo na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania na kushindwa kwa kampuni hiyo kuzifanyia matengenezo ya uhakika kama yalivyoagizwa.

(b) Mhe. Naibu Spika, kampuni hiyo ya *Indigo Aviation* yenye makao makuu yake mjini Dar es Salaam inamilikiwa kwa pamoja na Bw. John Martin Venter, Managing Director raia wa Afrika ya Kusini, Bwa. James Peter Sekei, ambaye ni Mtanzania na Bw. Robert Bruce Kellet ambye ni raia wa Afrika ya Kusini.

Anuani ya kampuni hiyo ni:

INDIGO AVIATION
P.O.BOX 23124
Dar es Salaam

(c) Mhe. Spika, ndege hizo zipo pembezoni mwa kiwanja karibu na karakana ya matengenezo ya ndege ya kampuni ya *Tropical Air* zikisubiri kufanyiwa matengenezo. Kwa kuwa ndege hizo zipo ndani ya eneo la kiwanja cha ndege, zinalazimika kufanyiwa malipo ya uegeshaji kama taratibu za uendeshaji kiwanja cha ndege zinavyoelekeza ambapo kila mwezi kama ilivyo kwa ndege nyengine yoyote ile kampuni hiyo hupatiwa *bill* za malipo ya uegeshaji ndege kiwanjani kwa ajili ya kufanya malipo husika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba ndege hizo ni mbovu na ni za aina ya *DC3* ambazo ulimwenguni hazipo tena. Je, sasa anawambia Wazanzibari hata zikitengenea ndege hizo Wazanzibari wasizipande.

(b) Ndege hizo zipo pembezoni mwa kiwanja cha ndege cha Zanzibar na kinatakiwa kilipe mafao. Je, wanalipa.

(c) Taarifa nilizonazo ni kwamba wamiliki wa kampuni hiyo wanadaiwa zaidi ya shilingi milioni 8 hadi sasa. Lini fedha hizo watazilipa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika,

(a) Tumeeleza katika majibu mama kwamba ndege hizi ni aina ya *DC3* ambazo kwa kiasi kikubwa zinaondoka katika soko la biashara ya anga. Ndege hizi zimesajiliwa na *TCIA* na kuratibiwa pamoja na kukaguliwa baada ya mamlaka husika kuridhika na umadhubuti na uwezo wa ndege hizi kutoa huduma zimeruhusiwa. Hivyo basi ni imani yangu baada ya kufanyiwa matengenezo hayo na kukamilisha taratibu hizo zilizoelekezwa na mamlaka husika hakuna kikwazo kwa wananchi wetu wa Zanzibar kuweza kutumia kwa ajili ya usafiri.

(b) Mhe. Naibu Spika, ndege hizi wamiliki wao kama tulivyoeleza kwamba wapo Dar-es-salaam na wanatakiwa kulipa kwa mujibu wa taratibu za kuegesha ndege katika kiwanja cha ndege. Mamlaka ya Uwanja wa Ndege tunafanya mawasiliano nao kwa kuwafikishia *bill*

zao kila mwezi na kuwataka kulipa. Ingawa mpaka hivi sasa hawajaweza kulipa *bill* hizo.

(c) Ni kweli kwamba tunawadai kiasi hicho cha shilingi milioni 8 ikiwa ni ada ya maegesho kwa mujibu wa taratibu na sheria na ni imani yetu tuwasiliane na wamiliki wenyewe. Ikiwezekana mashirikia yanayosajili, mashirika hayo kwa maana ya Brela na Idara ya Mrajis kuweza kuwapata wahusika wenyewe ili waweze kutulipa fedha zetu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi hii.

Kwa kuwa maelezo mengi yameelezwa na Mhe. Naibu Waziri. Je, haoni kwamba tokea ndege zile ziharibike umeshatimia mwaka.

Je, ni kweli hivyo ndege zile zitaweza kuondoshwa hayatobakia yakawa ni maozaoza pale uwanja wa ndege. Naomba nijibiwe swali langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli ndege hizo zimesitisha safari zake tokea mwezi wa pili mwaka wa 2010. Na ni kweli hivi sasa ni kipindi cha mwaka mmoja.

Sababu zilizopelekea kusitisha ndege hizo safari zake kama tulivyoeleza, na tunafanya mawasiliano na wenyewe wahusika ili waweze kuziondosha ili kuweza kutoa fursa na nafasi ya uwanja wa ndege kuweza kutumika kwa mambo mengine.

Kipindi hiki chote ambacho ndege hizi zitakuwa zipo katika maeneo ya uwanja tutahakikisha kwamba malipo husika yanafanyika ili kufidia nafasi hiyo inayochukuliwa na ndege hizo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika majibu yake mama Mhe. Naibu Waziri alikiri kwamba ndege hizi zilikaguliwa na vyombo husika na kwa sababu zilichukua muda mdogo sana kufanya kazi kabla hazijawekwa kuegeshwa katika uwanja wa ndege.

Je, ni funzo gani walilolipata Wizara yake kwamba ukaguzi ule ulikuwa umekamilika au kuna wasi wasi wa ukaguzi kama vile wanavyofanya wasi wasi watu wengi kwamba ndege zinazokuja Zanzibar huwa zinakuja kutupwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Mamlaka ya *TCIA* ni chombo chenye mamlaka husika na ni chombo ambacho kipo makini. Sitegemei kwamba ukaguzi huo wa ndege

uliofanywa ulifanywa kwa maana ya kwamba kuja Zanzibar kwa ajili ya ndege hizo kuja kutupwa.

Imani yangu kwamba ndege ni kama vyombo vyengine inawezekana leo kikakaguliwa kikawa kizima na kesho kikapata hitilafu. Ninachoweza kukipongeza chombo cha *TCIA* baada ya kuona mapungufu na hitilafu kuzizuia ndege hizi zisifanye safari ili kuwakinga wananchi wetu na majanga ambayo yangeweza kutokea.

Nam. 30

Kukosekana kwa Madaktari wa Kichina, Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Abdalla Moh'd Ali – Aliuliza**:-**

Kwa muda mrefu sasa, Hospitali ya Abdalla Mzee, Mkoani inapata msaada wa madaktari na madawa kutoka Serikali ya China. Hata hivyo, hivi sasa imejitokeza kuondoka kwa madaktari hao mara kwa mara na kusababisha kukosekana kwa huduma ya operesheni jambo ambalo linawasumbua na kuhatarisha maisha ya wananchi.

(a) Je, sababu zipi zinazopelekea kuondoka na hatimae kukosekana kwa madaktari hao.

(b) Je, ni lini Serikali itaondokana na utegemezi wa madaktari wa Kichina.

(c) Je, kuna muongozo gani wa Sheria ama Kanuni inayotumika katika kutekeleza uhusiano huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.30 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, madaktari wa Kichina wameanza kutoa huduma katika Hospitali ya Abdulla Mzee Mkoani baada tu ya kufunguliwa hospitali hiyo mwaka 1969. Hospitali hiyo ilijengwa kwa msaada Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China mara tu baada ya mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964. Kwa makubaliano baina ya Serikali mbili hizo; makubaliana ambayo yalitiwa saini na Rais wa Kwanza wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Hayati Abeid Amani Karume.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo madaktari wa Kichina walikuwa wakifanya kazi kwa muda wa miaka miwili mfululizo bila ya mapumziko ya aina yoyote, isipokuwa mapumziko ya siku Uhuru wa China ambayo yalikuwa ni ya wiki moja tu katika mwaka.

Kutokana na mabadiliko ya Utawala ya Serikali ya China na makubaliano maalum, madaktari hao sasa inawabidi kupata likizo kila mwaka, likizo ambalo inawabidi kuondoka kutembelea sehemu mbali mbali nchini na wakati mwengine hulazimika kwenda kwao China, gharama ambazo hutolewa na serikali yetu au wanaweza familia yao ikaja wakati wa likizo kuja kuwaona watu wao waliokuwepo hapa kuja kutufanyia kazi.

Kwa mantiki hiyo madaktari kuondoka kwenda likizo hiyo nafikiri ni haki yao ya msingi kama mfanyakazi mwengine yeyote. Na kama wakati huo walipoanza kuja utawala ulikuwa mwengine sasa kwenye mabadiliko ya demokrasia mfanyakazi lazima aende likizo. Kwa hiyo wanaondoka wanakwenda likizo. Kutokwenda likizo kwao kwa miaka hiyo sio kwamba ilikuwa ni jambo ambalo lilikuwa likiwapa faraja isipokuwa ilikuwa ndio utaratibu uliopo.

Miaka miwili binadamu asiende likizo akae nje ya nchi na nyumba yake kwa kweli nafikiri ni mtihani. Si kwa waliokuwa wanaume wala wanawake, wengi wao walikuwa wakirudi majumbani kwao hali haikuwa shwari.

Hata hivyo kwa muda ambao baadhi yao watakuwa hawapo hapa nchini, huduma huwa zinaendelea kutolewa na madaktari wetu wazalendo na pale linapotokezea kubwa wanaloliweza wagonjwa huwa wanapelekwa jirani ya Chake-Chake.

(d) Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kila juhudi ya kupeleka vijana wake sehemu mbali mbali ulimwenguni kuchukua mafunzo ya udaktari kwa lengo la kujitosheleza. Hata hivyo kuwepo kwa madaktari wa Kichina katika

hospitali zetu za Abdulla Mzee na hata katika Hospitali ya Mnazi mmoja.

Mnazi Mmoja sasa hivi ni magurupu ya 23 kwa sababu wanakaa miaka miwili miwili. Na kwa Pemba pia miaka miwili miwili na hili lililokuwepo ni gurupu la 21. Wanakuja kila baada ya miaka miwili bila ya kusita. Haimaanishi kwamba kuja huku ina maana kwamba Zanzibar tunaweza kusema kwamba tuko wategemezi kwa hao madaktari wanaokuja. Hayo ni makubaliano ambayo tumekubaliana kila mwaka wanapokuja madaktari tunakuwa tunaulizwa mnauwataka madaktari wa fani zipi, fani tunayoitaka ni ile ambayo sisi hapa hatuna. Kwa hivyo, tukianza kuchagua huyu kaolewa au hajaolewa ina maana ili daktari aweze kuwa tunayemtaka basi anachukua miaka mingi hatusubiri miaka yote asome tu asiowe.

Mhe. Spika, miaka yake daktari anasoma ina maana kwamba asiowe au asiolewe? Kwa hivyo, sisi tunataka daktari anayehusiana na mafigo, tunataka daktari anayehusiana na moyo na ukiwatizama hao miaka yao iko kwenye arubaini na tano mpaka hamsini, hivyo kweli atakaa asiowe. Mhe. Spika, au sisi tutampata daktari gani ambaye ana miaka 18 mpaka 20 atakayekuwa na utaalamu huo, hilo sharti kwa kweli ni gumu tunachotaka ni utaalamu na miaka miwili ndio makubaliano na ndivyo itakavyokuwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali lake la msingi alisema kwamba kuwepo kwa madaktari wa kigeni si kwamba Zanzibar ni wategemezi. Lakini kwa kuwa daktari mzalendo aliyeko pale ni mmoja na ana kiwango cha *AMO* (*Assistance Medical Officer*) na kwa kuwa tunapeleka madaktari wengi kusoma katika vyuo kadhaa vya ndani na nje ya nchi hii na wanaporudi madaktari wale mara nyingi baada ya kupangiwa hospitali zetu za Zanzibar huwa wanaondoka kwenda kufanya kazi nje au katika hospitali za private zilizoko Bara. Mhe. Naibu Spika, hii ni kutokana na kiwango duni cha malipo.

Je, Mhe. Naibu Waziri serikali itatumia mbinu gani ili kuwadhibiti madaktari wetu wanaorudi kusoma nje na ndani ya nchi ili waweze kutoa huduma hapa badala ya kwenda nje kutokana na maslahi mabovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar nafikiri mishahara yetu yote tunaifahamu kwa madktari, kwa walimu kwa kazi yoyote ile, nafikiri serikali huwa inalipa wafanyakazi wake kwa mujibu wa inachokipata. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uchumi wake tunaujua na sisi wawakilishi ndio tulioko hapa na sisi ndio siku zote tunachangia na tunaielewa hali halisi. Kwa hivyo, Serikali ya

Zanzibar itamlipa daktari kwa mujibu wa uwezo ulionao, wanafunzi wa Zanzibar wengi wetu tunasomeshwa na serikali. Mhe. Naibu Spika, mimi nimesoma vyote hivyo nilivyovisoma sikuwahi kulipa pesa yangu mfukoni, hivyo nitailipa nini mimi serikali ni mamilioni ya pesa yaliyotoka kwenye serikali hii.

Kwa hivyo, kinachotakiwa ni kwamba tuwe na uzalendo wa kulipa angalau zile fadhila serikali iliyotupa, maana hakuna *AMO* wala daktari aliyekwenda kusoma nje kwa mapesa yake kwa nchi yetu hii ya Zanzibar kwa vyovyote vile mkono wa serikali utaingia, lakini mia kwa mia ni wachache sana, na wanaosoma hivyo basi sio mara nyingi kurudi hapa kwa sababu wana uhuru wa kwenda wanakotaka kwa sababu wamejilipia wao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, suala la madaktari wetu kutokana hapa wakenda wakasoma *AMO* Tanzania Bara halafu wakawa hawarudi maana hawawezi kwenda nje ya Tanzania Bara, *AMO* hajawa daktari wakutoka kwenda Boswana wala Afrika ya Kusini, mwisho wake ni Tanzania Bara kwa sababu hiyo kada inatambulikana hapa kwetu tu. Nchi nyengine wanatambua daktari ni yule aliyesoma miaka mitano, Tanzania Bara sasa hivi ina mpango wa kupeleka huduma mpaka vijijini. Mhe. Naibu Spika, na hao madaktari wanaokimbia hapa hawakai Dar es Salaam wanakwenda vichochoroni hata gari hazifiki bora hata hapa kwetu.

Kwa hivyo, mimi nasema ni imani ya mtu sisi hatuwezi tukaenda nayo kwa sababu hiyo ni *attitude* yake binafsi. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wanachotakiwa waende wakasome hiyo miaka miwili wanayosoma elimu wanayoipata serikali inaigharamia vikubwa hawaendi kwa pesa zao na wala hawasomi bure. Kwa hivyo, kama wanataka basi angalau warudi watulipe hiyo miaka yetu miwili halafu waende wakatafute huo mshahara mkubwa vyenginevyo tukitaka kujilinganisha sisi na hapo Tanzania Bara tutashindwa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba serikali inajitahidi na tutajitahidi juu chini kuomba angalau yale maslahi ya msingi serikali itupe na hayo tunayafanyia kazi na nina imani kwamba serikali itasikia kilio chetu na tutalipwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Pemba upo upungufu wa madaktari Mheshimiwa ni kwamba huoni kuna umuhimu wa kuanzishwa Chuo cha Afya Pemba ili wanafunzi wanapomaliza kusoma waanze kufanya kazi zao huko Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi mia kwa mia kwamba Pemba kuna tatizo la madaktari na Unguja

kuna tatizo la madaktari lakini Pemba imezidi. Nimekaa Pemba wiki tatu mfululizo kupita kuingalia na kuitathmini hali ya Pemba, si madaktari tu kada zote na Unguja pia lakini Pemba imezidi. Kwa hivyo, suala la kufungua chuo Pemba kwa madaktari tayari wako pale 12, Unguja wanasoma na Pemba wanasoma, isipokuwa tu mazingira hayakuniridhisha kwa madaktari wanaosoma.

Kwa hivyo, suala la kusomesha tunaweza tukasomesha Unguja tukapeleka Pemba kwani hii yote ni nchi moja, utaratibu mzuri unatakiwa upangwe kwamba hawa wakae Unguja na hawa waende Pemba, na ikiwezekana tuwe na mikakati maalum ambayo tunataka tuitekeleze ili tuweze kupata watoto kila sehemu angalu kila mmoja akirudi kwao akifanya kazi kwao atakuwa na moyo wa kufanya kazi kwao.

Kwa hivyo, suala la Pemba wanafunzi wanasomeshwa wako pale Chake Chake na Unguja pia wapo, lakini mazingira kidogo ni magumu hivyo tunatafuta utaratibu ili tuweze kuwarudisha hapa ili wasome kwa amani, maana daktari unayemsomesha kwa dhiki usifikiri atakapomaliza atakuwa na raha ya kukutibu, atakuwa na chuki ndani ya nafsi yake atasema kwamba sasa hivi na mimi nimeshapata cheti watanikoma. Kwa hivyo, tumeona bora tuwarudishe ili waje wapate nafuu lakini watakapomaliza tutagawanya Unguja na Pemba kwa sababu utaratibu utakuwepo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya ningependa kutoa maelezo kidogo kwenye mambo mawili.

Kwanza lile linaloambiwa kwamba madaktari huwa wanakimbilia Tanzania Bara. Jana mlimsikia Mhe. Waziri wa Fedha akizungumza juu ya hali yetu ya uchumi, lakini nadhani tumeshalieleza kama mara moja au mbili hapa kwamba serikali inazingatia kurekebisha mambo hasa sekta ya afya. Lakini naomba ifahamike na bahati nzuri leo wananchi wananisikita, nataka ifahamike kwamba kukimbilia Tanzania Bara si suala la kukimbilia mshahara, mwenzangu amesema ni uzalendo.

Mhe. Naibu Spika, kiasi mwaka mmoja na nusu au miwili tumewapeleka vijana wanne Moshi kusoma mambo ya nusu kaputi, tumewapeleka kwa kujua kwamba tunashida na wizara ikauchukua umuhimu mkubwa wa hilo, hivyo wameshamaliza na wamerudi wawili. Lakini wazee wao walitia saini hapa na kwamba watahakikisha kwamba vijana wale wakishasoma watarudi, hivyo hawajarudi wako hapo Muhimbili. Hivyo, je tuwachukulie hatua wazee wao ni kwamba haielekei na wote wamelipwa kila kitu na serikali na mikataba wazee

wao wametia. Kwa hivyo, angalau basi wangekuja mwaka mmoja au miwili halafu wakaondoka.

Mhe. Naibu Spika, wengine wakumbuke kwamba sisi tulipomaliza Chuo Kikuu tulikuwa tukilipwa shilingi mia moja na arubaini na nne, tukiita *growth* tulikuwa tunakwenda zetu nyumbani na shilingi mia na thalathini na nane. Tumefanya kazi mwaka ukamalizika tukaaza kulipwa shilingi elfu moja kwa wakati ule kwa sasa ni shilingi laki tatu, lakini ukweli ni kwamba kama hakuna moyo wa uzalendo kapu la Bara halijai na mshahara wa Bara hauwezi kulinganishwa na mshahara wa Unguja.

Mimi ukinipa milioni moja nikakae Bara na laki tano za hapa basi nitakubali za hapa. Maana nina hakika kwamba huo mshahara nikitoka nao kwenye afisi ya Bara nitafika ninakokaa sijapigwa kabari. Kwa hivyo, suala la msingi ni uzalendo na wazee wetu tunaomba kuwaambiwa kwamba tunachofanya ni kusaidia kujenga nchi yetu kutokana na hali yetu. Mhe. Naibu Spika, mishahara inazingatiwa na serikali, maslahi ya wafanyakazi yanazingatiwa na serikali na tunayajua kwamba mengine yanastahiki wapewe hivyo tunarekebisha. Lakini suala la kumaliza masomo kwa watu waliosomeshwa na serikali wakakimbia nalo vile vile halitoi moyo kwa wale wazee ambao wanawaachia watoto wao. Hivyo, tunajitahidi tutarekebisha sheria ili wazee wawajibike, nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 11

Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi kwa Majengo ya Serikali

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak – Aliuliza**:-**

Itakumbukwa kwamba Serikali ilianzisha Tume ya Ujenzi kwa ajili ya kusimamia masuala ya ujenzi pamoja na kununua vifaa vya ujenzi kwa majengo yake.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizopelekea Tume hiyo muhimu kufa.

(b) Kwa kuwa kila taasisi ya Serikali inaagiza vifaa vya ujenzi kwa kutumia njia inayoona inafaa, hamuoni kuwa kitendo hicho kinatoa mwanya wa ubadhirifu wa fedha za umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hivi sasa wizara yangu haina Tume ya Ujenzi Kitaifa, lakini kuna chombo kinachofanana na hicho ndani ya wizara yangu nacho ni Bodi ya Wasanifu, Wahandishi na Wakadiriaji wa Majengo ambayo kimeundwa kwa mujibu wa sheria Nam. 6 ya mwaka 2008 ambayo inaendelea na kazi zake.

(b) Taasisi zote zinalazimika kutumia taratibu moja ya manunuzi kulingana na Kanuni ya Mwaka 2006 iliyopo katika Toleo la Serikali Nam. 62 zilizo chini ya Sheria iliyotajwa hapo juu ambamo mwanya wa ubadhirifu wa fedha za umma umedhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Nam. 22

Wananchi wa Pemba Kunufaika na Huduma za TVZ

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza**:-**

Kama inavyofahamika kwamba kwa kupitia vyombo vya habari, wananchi wetu walio wengi wanapenda sana kujuwa taarifa za nchi yao na taarifa mbali mbali za matokeo mbali mbali ya dunia na suala hili limekuwa zaidi baada ya kuongezeka kwa vyombo vya habari nchini.

(a) Kwa kuwa wananchi wa Pemba hawapati fursa hii ipasavyo. Je, kuna sababu zipi zinazokwamisha juhudi za kuwawezesha kuona Televisheni yao ya Zanzibar *(TVZ).*

(b) Kwa kuwa tatizo hili lipo muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi, Je, Wizara itachukua hatua zipi kulimaliza mara moja.

(c) Je, Wizara inatarajia kuchukua muda gani kuliondosha tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama inavyofahamika kwamba kwa kupitia vyombo vya habari, wananchi wetu walio wengi wanapenda sana kujua taarifa za nchi yao na matokeo mbali mbali ya dunia. Suala hili limekuwa zaidi baada ya kuongezeka kwa vyombo vya habari nchini.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba wananchi wa Pemba kwa kipindi kirefu wamekuwa wakikosa fursa ya kupata taarifa za nchi na matokeo ya dunia kupitia chombo chao cha Televisheni Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, si madhumuni wala si malengo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwanyima wananchi wake haki hiyo ya msingi ya kupata habari na taarifa za matokeo duniani. Katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata habari na taarifa ipasavyo, Serikali huwa inatumia fedha kadri hali inavyoruhusu. Baada ya kutoa utangulizi huo sasa naomba nijibu swali Nam. 22 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sababu hasa zinazopelekea wananchi wa Pemba kukosa matangazo ya TVZ ni mtambo wa kurushia matangazo uliopo Pemba ulifungwa mnamo mwaka 2005. Kwa bahati mbaya mtambo huo wa masafa ya *VHF* katika kipindi kifupi tokea kufungwa uliathirika na tatizo sugu lililokuwepo Pemba wakati huo la kuzimwa, kuwasha, kupanda na kushuka umeme kusikokuwa na mpangilio. Hali hiyo mbaya ya umeme imepelekea kutofanya kazi mtambo huo kikawaida.

Sambamba na tatizo hilo pia lilikuwepo tatizo la *antenna* ya kurushia matangazo ambayo ilihitaji kubadilishwa. Bahati nzuri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoa fedha za kununua *antenna* mpya kwa ajili ya mtambo huo wa Pemba. Lakini katika kulitekeleza hilo, lilitokea tatizo jengine la teknolojia, ambalo ni la mfumo wa kurushia matangazo kutoka *Analog* na kwenda *Digital*. Naomba ifahamike hivi; Katika kuhamia urushaji wa matangazo kwa njia ya *Digital*, ukanda wa Afrika Mashariki umeamuliwa na Taasisi ya Kimataifa ya Mawasiliano (*IT.U*) kutumia masafa ya *UHF*. Kwa hivyo, katika kulitatua tatizo la TV kwa Pemba haitokuwa busara kutumia fedha nyingi kununua vitu ambavyo vitatumika kwa muda mfupi.

(b) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshachukua hatua za kulitatua tatizo la TV Pemba. Hatua hizo ni pamoja na juhudi za hivi sasa za kuingia katika mfumo mpya wa urushaji wa matangazo kwa njia ya *Digital* ambapo hatua za kununua mitambo miwili ya *digital*, *antenna* 2 pamoja na vidhibiti umeme zinaendelea. Mtambo mmoja kati ya hiyo utafungwa Unguja na mwengine Pemba.

(c) Tatizo hilo linatarajiwa kupatiwa ufumbuzi kati ya mwezi wa Mei na Juni mwaka huu wakati mitambo hiyo iliyonunuliwa itakapokuwa imeshafungwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alikiri kwamba hii haki ya habari ni miongoni mwa haki za msingi za mwanadamu na kwa kuwa wananchi wa Pemba muda mrefu hawapati huduma ya televisheni yao. Je, serikali itakubaliana na mimi kwamba kwa hapa serikali iliwaonea wananchi na ilivunja haki zao.

b) Kwa kuwa uamuzi wa dunia kuachana na *system* ya analog haukuja leo, kwa nini serikali ikaamua kununua mtambo wa analog wakati maamuzi ya dunia hayakuanza leo yameanza zamani kwamba system analog tuiache na tuingie katika digital. Kwa nini serikali ikaamua kununua mtambo huo wakati wanajua kwamba mtambo huo haufai tena katika matumizi ya dunia ya sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwenye swali mama nimeeleza mambo muhimu ya televisheni ya Pemba kuingia kwenye mfumo wa digital kwa sababu serikali na umoja wa kitaifa ndio tunaotakiwa tuufuate sasa hivi kwa kuingia kwenye mfumo huu ambao utatuletea maendeleo ya uhakika nchini petu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa ufafanuzi zaidi kutokana na suala la Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba ilikuwa si haki kukosa haki hii ya msingi ya kupata habari tu, lakini lilikuwa ni suala ambalo kwa kweli lilikuwa ni nje ya uwezo wetu kwa sababu ni suala ambalo limekuja baada tu ya mtiririko mbaya wa umeme sote tunajua kwamba Pemba kulikuwa na matatizo ya umeme kwa muda mrefu, lakini kwa muda wote huo kwa kweli matangazo yamekwenda kama kawaida.

Lakini baada ya mtiririko ule baadae tukapata matatizo ya vyombo vyetu kuharibika na baada ya kuona hilo ndipo tukagundua mimi mwenyewe binafsi nimekwenda na nikaona hiyo hali ni kwamba matangazo yanakwenda mpaka station isipokuwa sasa ile kuyarusha wananchi ndio wahawapati. Hata hivyo, kwa bahati tukalipeleka hili suala serikalini na serikali wamelichukulia umuhimu mkubwa sana na wameshatoa fedha hizo tukanunue hicho kifaa

ambacho kilikuwa kimeharibika na kwa wakati ule ilikuwa bado suala digital, hivyo hatuwezi tukafanya kitu kama hicho wakati tunajua kwamba kuna mfumo mwengine halafu tukafanye kosa kama hilo ilikuwa ni bado kabisa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kufunga kile chombo matokeo yake ikawa kumbe nacho kimeathirika kile cha antenna cha kurushia. Kwa hivyo, tukaona hatuwezi kununua mtambo wakati tayari wazo la kwamba tuingia kwenye mfumo wa digital umeshaingizwa nchini, hivyo tukasema tusinunue kwanza wacha tusubiri ili tuje tununue kwa ujumla yaani chombo hicho pamoja na antenna ya kurushia. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunashukuru kwamba serikali imetoa fedha na tayari hivyo vitu viko njiani na kama walivyoeleza Mhe. Naibu Waziri kwamba mwezi wa Mei vitafungwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa tujenge subra kidogo hilo suala tutalikamilisha, ahsanteni sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba muda wa maswali unakaribia kumalizika na tumebaki na suala moja kwa hivyo naomba ridhaa ya wajumbe tuongeze muda ili tumalize hili suala moja. Je, Waheshimiwa Wajumbe mmeafiki juu ya suala hili la kuongeza muda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nam. 16

Udhalilishaji wa Kijinsia

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza**:-**

Ripoti ya udhalilishaji wa kijinsia kwa mwaka 2010 imeeleza kuwa asilimia 50 ya kesi 389 zinawahusu watoto chini ya miaka 18.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inaitambua ripoti hiyo.

(b) Kwakuwa asilimia 50 ya kesi hizo zinawahusu watoto wadogo, Je, wizara yako ina mikakati gani katika kupunguza tatizo hilo.

(c) Je, unatoa wito gani kwa jamii.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara inapenda kujua taarifa hiyo imetoka wapi na imetolewa na nani, hata hivyo, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi juu ya kuwepo kwa ongezeko la vitendo vya udhalilishaji wa Watoto Nchini hali hii imedhihirika kufuatia tafiti kadhaa zilizofanywa na wizara na wadau wengine. Kwa kipindi cha Mwaka 2010 taarifa kutoka Hospitali ya Mnazimmoja imeonyesha kuwa jumla ya kesi 870 ziliripotiwa.

Kesi hizo zilihusisha udhalilishaji wa kingono. Aidha, wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la kuwahudumua watoto *UNICEF* imetoa ripoti ya udhalilishaji ambapo takwimu zimeonyesha kuwa silimia 9 ya watoto wa kike na asilimia ya Watoto wa Kiume waliohojiwa katika utafiti huo wamekiri kufanyiwa udhalilishaji wa kingono. Kwa upande wa wizara tulipokea malalamiko ya Watoto waliodhalilishwa 362 Unguja na Pemba kwa mwaka 2009/2010.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara katika kukabiliana na vitendo vya udhalilisha wa watoto, imeunda kitengo maalum cha hifadhi ya watoto ambacho kinaunganisha juhudi za wadau wote pamoja katika kushughulikia masuala ya watoto. Pamoja na mambo mengine kitengo hicho kinapokea malalamiko ya udhalilishaji wa watoto, kuyafuatilia na kuyapatia ufumbuzi.

Pia wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia Watoto Duniani *UNICEF* imefanya utafiti juu ya ukatili dhidi ya Watoto *(Violence Against Children – VAC)*, matokeo ya utafiti huu yameshakamilika na hatua iliobakia ni uzinduzi rasmi wa matokeo ya utafiti huo na kuandaa mpango wa utekelezaji.

Mhe. Naibu Sppika, vile vile, wizara yangu iko katika hatua za mwisho za kupitisha sheria ya mtoto, sheria ambayo pamoja na mambo mengine imetilia mkazo kukomesha masuala ya udhalilishaji na ukatili dhini ya watoto ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kali kwa watendaji wa vitendo hivyo. Vile vile wizara imekamilisha mpango wa kisekta

dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia mpango ambao unashirikisha sekta zote katika kukabiliana na tatizo hilo.

(c) Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa jamii kwanza wasisite kutoa taarifa za udhalilishaji wa watoto kwenye taasisi zinazohusika na kushirikiana kikamilifu na vyombo vya sheria katika kushughulikia masuala haya. Aidha, napenda kuiomba jamii kuhakikisha kuwa hawapotezi ushahidi wa kesi za udhalilishaji kwa kuwakosha watoto wanaobakwa au kuchoma nguo zao moto kabla ya kuwafikisha katika vyombo vinavyohusika ikiwa ni pamoja na hospitali ambapo pamoja na mambo mengine waathirika hupatiwa dawa ya kuzuia maambukizi ya virusi vya ukimwi kabla ya masaa 72.

Vile vile naisisitiza jamii kuacha tabia ya kumaliza kesi za udhalilishaji kienyeji kwa kutaka suluhu baina ya mtendwa na mtendewa. Jambo hili huchangia kasi ya ongezeko la vitendo hivi na kuviviza vyombo vya kisheria kuchukua mkondo wake.

Mbali na hayo, naiomba jamii kushirikiana katika malezi na kuimarisha udhibiti wa watoto, ikiwa ni pamoja na kuwafuatilia nyendo zao mchana na usiku.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Skipa, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kisiwani Unguja amesema kesi 362 na Pemba kesi 162. Je, Mhe. Waziri kuna hatua gani za kisheria ambazo zimechukuliwa kwa wadhalilishaji hawa wa kijinsia Pemba na Unguja.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama ameyasikiliza vizuri majibu yangu ya kifungu (a) basi atahakikisha kwamba hatua mbali mbali zimechukuliwa dhidi ya hao watu wanaodhalilisha watoto na kuwabaka.

KAULI ZA MAWAZIRI

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Kipindi cha mwaka 2008/2009

Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka

katika hali ya uzima na afya njema na kuweza kuwasilisha ripoti hii muhimu katika Baraza lako tukufu. Shukurani zangu za dhati nazitoa pia kwako wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kuipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo sasa napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2008/2009. ni matumaini yangu kwamba, wajumbe wataipitia na kuifanyia kazi kwa lengo la kuimarisha misingi ya utawala bora na nidhamu katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii inawasilishwa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 84 Kifungu 112(5), hali inayoashiria kukomaa kwa demokrasia na utawala bora katika nchi yetu. Aidha, ripoti hii baadaye itafanyiwa kazi na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*) na kuliarifu Baraza lako tukufu kama zinavyoelekeza kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Ripoti hii imeelezea mambo yote yaliyogunduliwa wakati wa ukaguzi ambapo dosari na kasoro zozote katika uwekaji wa mahesabu pamoja na kasoro katika udhibiti wa matumizi ya fedha na mali za serikali zimeainishwa. Lengo kuu la zoezi hili ni kupata ufanisi katika matumizi, utunzaji na uendeshaji wa fedha za serikali na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu zote za matumizi na udhibiti wa fedha na mali za serikali zinafuatwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, mkaguzi mkuu wa hesabu ana majukumu yafuatayo:

1. Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria.
2. Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi ya serikali yameidhinishwa na Baraza la Wawakilishi na zimetumika kwa ajili ya shughuli husika.
3. Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya hesabu na utendaji wa shughuli za serikali na kuripoti Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, uimarishaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaendelea kuimarisha huduma za ukaguzi nchini na kutoa mafunzo kwa watendaji wake hali iliyopelekea kuwa na wafanyakazi wenye taaluma na kuimarisha utoaji wa huduma.

Muongozo wa ukaguzi umeshatayarishwa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi duniani. Napenda vile vile kutoa taarifa kwamba, kwa upande wa mahesabu ya mwaka 2009/2010 ukaguzi wake umeshakamilika kwa taasisi zote za serikali, mashirika, miradi ya maendeleo na halmashauri za wilaya Unguja na Pemba.

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kutoa taarifa ya ripoti hiyo kwa mujibu wa sheria ziliopo baada ya kukamilisha taratibu za mwisho za uchapishaji wa kitabu hicho.

Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka 2008/2009

Mhe. Naibu Spika, aidha ripoti hii imejumuisha taarifa za matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo pamoja na mapato yaliyokusanywa kutoka vianzio mbali mbali vya mapato ya kawaida na ya maendeleo.

Kiwango cha Uwekaji na Utunzaji wa Hesabu za Serikali

Mhe. Naibu Spika, uwekaji wa hesabu katika taasisi za serikali yakiwemo mashirika ya serikali, unadhihirisha kwa kiasi kikubwa kwa ujumla kumekuwa na mabadiliko makubwa kuhusu uwekaji na utunzaji wa vitabu vya mahesabu pamoja na kumbukumbu zake.

Kuanzishwa kwa utaratibu wa malipo kupitia mfumo wa mtandao, kumepelekea kuimarika kwa utunzaji wa hesabu katika taasisi za serikali.. hata hivyo, ufungaji wa mahesabu kwa baadhi ya taasisi haufikii kiwango kinachohitajika kwa mujibu wa sheria pamoja na kutowasilishwa kwa wakati unapelekea utoaji wa ripoti za ukaguzi kuchelewa. Juhudi za kuwaelimisha na kupata watendaji wenye ujuzi katika fani za uhasibu zinaendelea na zinapaswa kuchukuliwa kuwa ni endelevu.

Mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka 2008/2009

Mhe. Naibu Spika, katika ukaguzi wa mahesabu kwa kipindi cha ukaguzi cha mwaka 2008/2009, dosari za kiutendaji ziliweza kubainika katika taasisi mbali mbali, baadhi ya dosari na kasoro ziliweza kurekebishwa. Ufungaji wa hesabu unaotumiwa na serikali hivi sasa hauendani na taratibu za viwango vya kimataifa. Afisi inashauri mabadiliko ya ufungaji wa hesabu za mwaka ufuanyike kwa kufuata mfumo wa matumizi unaotumika hivi sasa na kufuata utaratibu unaotumika kimataifa kwa serikali na taasisi za umma bila ya kuathiri sheria zilozopo.

Aidha, dosari nyengine zilizogunduliwa wakati wa ukaguzi hazikujibika kutokana na kukosekana kwa maelezo pamoja na vielezo vinavyohusiana na hoja hizo. Hoja hizo zilihusu matumizi ya masurufu na matumizi ya kuendesha kazi. Vile vile baadhi ya hati za malipo hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi kwa baadhi ya taasisi za serikali.

Matumizi ya masurufu

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 5,170,000/- zimetumika kwa njia ya masurufu kwa shughuli mbali mbali za taasisi zikiwemo safari za kikazi, matumizi hayo hayakuweza kuthibitishwa kutokana na ukosefu wa vielelezo zikiwemo stakabadhi za matumizi pamoja na marejesho ya fedha hizo.

Matumizi yasiokuwa na vielezo vya uthibitisho

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 138,053,207 na US$ 94,209 zilitumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kuendeshea kazi kwa taasisi mbali mbali. Matumizi hayo hayakuweza kuthibitishwa uhalali wake kutokana na kukosekana vielelezo husika.

Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la vifaa

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 29,251,380 zilitumika kwa ajili ya kununulia vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya afisi kwa baadhi ya taasisi za serikali, lakini vifaa hivyo havikuingizwa katika daftari la vifaa ili kuonesha mapokezi ya vifaa hivyo pamoja na matumizi yake.

Malipo yasiyo na Stakabadhi *(RISITI)*

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 103,294,571 zilitumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kuendesha kazi kwa taasisi mbali mbali. Matumizi hayo hayakuweza kuthibitishwa uhalali wake kwa kukosekana stakabadhi husika.

Malipo yasiyo na Mikataba

Jumla ya shilingi 413,648,097 zimetumika kwa kazi tafauti za ujenzi, lakini mikataba ya kuhalalisha malipo hayo haikupatikana kwa ukaguzi.

Changamoto zinazoikabili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imekabiliwa na changamoto mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Mabadiliko ya teknolojia katika mfumo wa fedha.
- Upungufu wa vitendea kazi vya kisasa.
- Upungufu wa wa wataalamu katika fani nyenginezo zitakazosaidia kufanyika ukaguzi yakinifu na ukaguzi wa mazingira.
- Ufinyu wa bajeti kutokana na hali ya uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hali hii imetokana na hali mbaya ya uchumi inayoikabili serikali. Hata hivyo, ni mategemeo yetu kwamba hali ya uchumi itakapokuwa nzuri changamoto hizo zitapungua kwa kiasi kikubwa au kumalizika kabisa.

Malengo ya Baadaye

Afisi tayari imeandaa mpango mkakati wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2011 – 2014. mpango huo wa miaka mitatu umeandaliwa wakati mpango ulioanza kutumika mwaka 2008 unategemea kumalizika Juni 11, katika mpango huo afisi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuongeza ufanisi kwa kuimarisha shughuli za ukaguzi na kutoa taarifa za ukaguzi kila mwaka kwa wakati na kwa mujibu wa sheria zilizopo.
- Kuendeleza viwango na ubora wa ripoti za ukaguzi kulingana na viwango vilivyowekwa vya kitaifa na kimataifa kwa kufufata kanuni na taratibu za kimataifa.
- Kufanya ukaguzi yakinifu utakaozingatia thamani, ubora na ufanisi.
- Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi..
- Kutoa huduma bora za ukaguzi kwa taasisi za serikali pamoja na miradi ya maendeleo.
- Kukuza mashirikiano kati ya afisi ya taasisi kama hizi katika kanda ya Afrika na ulimwengu kwa ujumla.
- Kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye taaluma za uhasibu na ukaguzi na taaluma nyenginezo zitakazosaidia kufanyika kwa ukaguzi yakinifu.
- Kuwapatia vitendea kazi vya kisasa wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

HITIMISHO:

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inaendelea na kutekeleza majukumu yake yatakayolenga kuunga mkono juhudi za serikali za kusimamia na kuimarisha huduma za jamii na maendeleo kwa nia ya kujenga maisha bora kwa wananchi wa Zanzibar. Ili kufikia malengo ya kupunguza umasikini na kupambana na rushwa, hatua zitachukuliwa kutekeleza majukumu yetu katika kupambana na vitendo vyote vya rushwa na ubadhirifu wa mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa muhtasari sasa naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe maelezo kidogo ya kanuni juu ya suala hili tunaloendelea nalo hivi sasa. Kanuni ya 43 Kauli ya Mawaziri, naomba ninukuu.

> *"Waziri anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika na baada ya hapo mwenyekiti wa kamati inayohusika anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya kamati juu ya kauli hiyo".*

Kifungu cha 3 kinasema kwamba:

> *"Hakutokuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, lakini wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika, kumuuliza maswali waziri juu ya kauli aliyoitoa kwa madhumuni ya kueleweshwa zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo".*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kanuni zetu hakutokuwa na majadiliano, isipokuwa kwanza tutampa nafasi mwenyekiti wa kamati inayohusika aje kutoa maelezo baadaye wajumbe tutawapa nafasi ya kuuliza maswali kwa wale waliokuwanayo. Kwa hivyo, baada ya maelezo haya namuomba Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) aje kutoa maoni kwa niaba ya kamati yake.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu na mafanikio yake ni kuijenga nchi yetu ya Zanzibar itakayowanufaisha wananchi wetu wa sasa na vizazi vijavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niziwasilishe shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuzungumza machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishaji wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Napenda pia kabla ya kuanza kuzungumzia lolote kuhusu ripoti hii, kuipongeza kwa dhati Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwasilisha ripoti hii ambayo kwa mnasaba wa kamati yetu kufuatia kuundwa tena kwa mwaka 2011 na kwa kuwa wajumbe wengi ni wapya na baada ya kupatiwa mafunzo ya awali na afisi hii na hatimaye kuanza kazi kwa wiki mbili zilizopita, kama tutakavyokuja kutoa ripoti yetu wiki ijayo ripoti hii imekuja kwa wakati muwafaka.

Mhe. Naibu Spika, sasa napenda kuanza na kamati yetu ya *PAC*. Kamati yetu imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 115 cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2011 lenye majukumu yafuatayo:-

1. Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za serikali na mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
2. Kuchambua na kutafakari ripoti yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.
3. Kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa, mambo yote yanayohusu hesabu za serikali na asasi zake.
4. Kutoa ripoti yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.
5. Katika kufanya kazi zake Kamati ya *PAC* itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama fedha zilizooneshwa katika makadirio ya matumizi ya serikali na mashirika yake zimetumika kama ilivyokubaliwa na matumizi yaliyokuwa chini ya mamlaka iliyohusika, na matumizi yalizingatia thamani halisi ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa miaka miwili na nusu tuliyonayo, kamati yetu imeundwa na wajumbe wanane na makatibu wawili kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Ali Shehe	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Fatma Mbarouk Said-		Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Mjumbe
4.	Mhe. Farida Amour Moh'd	-	Mjumbe

5.	Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	-	Mjumbe
6.	Mhe. Moh'd Mbwana Hamad	-	Mjumbe
7.	Mhe. Shadya Moh'd Suleiman	-	Mjumbe
8.	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	Mjumbe
	Ndugu Abdalla Ali Shauri		Katibu
	Ndugu Othman Ali Haji	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu yake yameelezwa katika kifungu cha 3 cha kifungu hicho kama yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zilizokusudiwa kutolewa katika Mfumo Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti haya yatatekelezwa ipasavyo, basi yataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo.

Matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo na angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za tume au vyombo vyengine vilivyoidhinishwa na katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 ambayo hivi sasa iko mbele yetu, haina tofauti na ripoti zilizopita. Takriban imeonesha udhaifu ule ule wa taasisi za serikali na ukiangalia kwa makini utakuta kuna hoja nyingi sana zimejirejea kwa taasisi hizo.

Kwa mfano, hoja nambari 24(1)(1) ya Hoteli ya Bwawani ya udhaifu katika udhibiti wa ndani ni ile ile iliyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2007/2008. Aidha, madeni ya ada za

utuaji wa ndege inayohusiana na Idara ya Anga yameendelea kuripotiwa kama vile yalivyoripotiwa mwaka 2007/2008 na miaka iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, hoja za kukosekana stakabadhi zimeshazoeleka wakati udhati wake ni kuipaka matope serikali. Kinachoshangaza ni kwamba, stakabadhi hizo zilizokosekana wakati wa ukaguzi ambao hufanywa kwa takriban mwaka mzima na Afisi ya Mdhibiti, hupatikana kwa siku moja tu ama masaa matatu yanayofanyiwa kazi na kamati yetu.

Hili linashangaza na linaonesha dhahiri kwamba, taasisi hizi haziwajibiki ipasavyo katika matumizi ya fedha za umma. Kwa ufupi tuseme stakabadhi hizi zinazowasilishwa mbele ya kamati mara nyingi huwa za udanganyifu. Tunaitaka serikali ikae na watendaji wake wa fedha na kuondosha kabisa kasoro hizi.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti hii tatizo hili la kukosekana kwa vielelezo ikiwa ni pamoja na stakabadhi linaonekana kwa taasisi zifuatazo:-

- Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais
- Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
- Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
- Wizara ya Kilimo na Maliasili
- Wizara ya Fedha
- Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Pemba
- Kikosi ya Kuzuia Magendo (KMKM)
- Baraza la Manispaa
- Tume ya UKIMWI
- Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale
- Chuo cha Taifa (*SUZA*)
- Hoteli ya Bwawani
- Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi (*ZIPA*)
- Shirika la Utalii
- Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*)

Mhe. Naibu Spika, tatizo linaloendelea kujirejea katika ripoti nyingi za mdhibiti ni kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali za kudumu, ambalo hili pia linaihusu afisi yako ya Baraza la Wawakilishi. Kama ilivyoripotiwa na ripoti hii, tatizo hili takriban linaendelea kuzikabili taasisi zote za serikali. Tunachotaka kusema ni kwamba, baada ya kamati kukaa na Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kamati imefahamishwa sasa lile daftari la pamoja, fomu za muongozo za kuhifadhia mali hizo yaani lenye kutoa muongozo mmoja wa kuhifadhia mali za serikali limeshatayarishwa na

kutolewa kwa wahasibu na watendaji wote wa fedha pamoja na mafunzo ya namna ya kuzitumia.

Aidha, kamati inapenda kuchukua fursa hii kuzitaka taasisi au serikali zirekebishe kasoro hii ili kamati ikiifanyia kazi ripoti hii kusiwe tena na majibu tuliyoyazowea kukosa muongozo kutoka Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imo katika mageuzi ya kiutendaji. Mageuzi haya yanahusiana na ukaguzi wa thamani halisi ya matumizi *(value for money)*, ukaguzi wa mahesabu kupitia kompyuta *(computerize auditing)* na ukaguzi wa kimazingira *(environmental auditing).*

Mageuzi haya pia yanahusika na ripoti hii tunayowasilisha leo. Umefika wakati sasa twende huko na sio kubakia katika kupekua marisiti ambayo mara nyingi hupikwa na watendaji. Kamati ya *PAC* hugeuka wakaguzi kwa kupekua risiti zilizokosekana wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ulimwengu sasa uko katika mageuzi ya kiukaguzi. Ukaguzi wa kuangalia thamani halisi ya fedha na kaguzi nyengine kama nilivyoeleza hapo awali hutoa sura halisi ya matumizi ya fedha za umma. Tunashauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanza ukaguzi huo ama ndani ya mwaka huu kwa ukaguzi wa dharura ama kwa ukaguzi wa mwaka unaofuata.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za kufanya ukaguzi na hatimaye kuwasilisha ripoti hizo Barazani na kutekeleza majukumu mengine ya kiutendaji, afisi hii inakabiliwa na changamoto mbali mbali. Kamati itaendelea kuzizungumzia changamoto hizo kupitia ripoti ya kamati na kila tutakapopata nafasi hadi hapo serikali itakaporekebisha changamoto hizo.

Mhe. Naibu Spika, changamoto kubwa inayokabili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kuwepo kwa maslahi madogo ya watendaji wake. Inasikitisha sana unapoikuta afisi hii yenye kazi ngumu ya kuzichunguza namna gani fedha za umma zinavyotumika, uhalali wa matumizi yake kama ilivyoidhinishwa na kwa kuzingatia thamani halisi ya matumizi ya fedha hizo katika ujenzi wa taifa letu. Wakati huo huo, maslahi ya watendaji wa kazi hizi za uchunguzi na udhibiti wa fedha za umma ni madogo mno ukilinganisha na baadhi ya taasisi wanazozikagua.

Mhe. Naibu Spika, hebu na kwa haraka tu tuipitie ripoti hii iliyowasilishwa hapa bila shaka tutafahamu kuwa kasoro zilizooneshwa katika ripoti hii ni nzito na mara nyingi wakaguzi wetu hupata kebehi, dharau ama kuonekana maadui kwa taasisi wanazozikagua. Kamati ya *PAC* imeshuhudia mara kadhaa watendaji wa taasisi zinazokaguliwa kuwatupia lawama wakaguzi. Ili kupunguza hali hiyo, jambo la busara ni kuongezwa kwa maslahi ya wafanyakazi wa afisi hii kutakakowafanya wajisikie huru na kuwajengea msimamo imara wa kuifanya kazi yao.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine ni uhuru wa watendajikazi. Ifahamike tu kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa uhuru wa kufanya kazi zake na Katiba ya Zanzibar kifungu cha 112 (7) kinakataza kabisa kuingiliwa katika kazi zake. Tunapenda kuzifahamisha taasisi za serikali ziheshimu maelekezo haya ya katiba ili kuiwezesha afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa maana iwapo afisi itatekeleza majukumu yake vizuri na kamati nayo itaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo, hatimaye na Baraza la Wawakilishi litajenga heshima mbele ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* nayo inakabiliwa na changamoto kadhaa. Wajumbe wa kamati ni wanasiasa ambao wametoka katika historia tofauti za kiutendaji. Masuala ya fedha yanahitaji ufundi mkubwa na baadhi ya watendaji wa serikali ni wajanja mno. Jambo la msingi la kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake ni kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara juu ya utekelezaji wa kazi zake. Tunaishauri serikali iliangalie hili.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Afisi ya Baraza la Wawakilishi ni wadau wakubwa wa kamati hii kimafunzo. Tunaiomba serikali iziwezeshe taasisi hizi kwa namna yoyote inayofaa ziweze kuandaa mafunzo mbali mbali kwa kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine inayokabili kamati ni muda mdogo wa kufanya kazi za kamati. Kamati inayozifanyia kazi wizara zote za serikali kupangiwa wiki nane tu hazitoshi. Kwa mfano, tukiipitia ripoti hii tunagundua kuwa wizara zote 16, mashirika yote na baadhi ya serikali za mitaa zimehusika ndani ya hoja ya mdhibiti. Hivyo, Kamati ya *PAC* inapopangiwa muda sawa na kamati nyengine zenye wizara mbili ama tatu huinyima kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kamati imekuwa ikipigia kelele suala hili muda mrefu na hata kumuandikia Mhe. Spika barua yenye kumbukumbu namba BLW/K10/25 ya tarehe 27/02/2011 kumuomba kuiongezea muda kamati. Aidha, tunaiomba serikali iliwezeshe Baraza kifedha ili liweze kutuongezea muda wa kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, sheria zetu za fedha zimeonesha adhabu, ila adhabu hiyo haiendani na wakati husika ama ni ndogo kulinganisha na makosa yanayofanyika. Kwa mfano, ukifanya rejea kifungu cha 38 cha Sheria ya Fedha za Umma *Act No. 12* ya mwaka 2005 adhabu inayotolewa kwa anayekiuka sheria hiyo ni kupigwa faini kwa kutozwa fedha zisizozidi shilingi laki tano baada ya kutiwa hatiani. Hii ni adhabu ndogo sana kwa mtendaji ama mtu aliyejikusanyia mabilioni ya fedha za umma kwa manufaa binafsi. *(Makofi)*

Aidha, kifungu hicho kinaendelea kutaja adhabu ya kifungo kwa mkiukaji wa sheria hiyo kwa anayeshtakiwa na kutiwa hatiani ni kutumikia kifungo kisichozidi miaka miwili. Adhabu hii kwa kweli ni kichekesho kabisa. Tunaomba sheria za fedha zipitiwe tena na ikiwezekana zitoe adhabu ya kila kifungu kinachohusika na isiwe tu kwa jumla kama ilivyo sasa. Adhabu hiyo ilingane na wakati na uhalisia wa kosa lenyewe.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kwa kuishauri serikali isifumbie macho kuwachukulia hatua watendaji wanaokiuka sheria na kanuni za fedha. Tunasisitiza serikali kuifanyia kazi ripoti ya kamati hii ili ifahamu nafasi yake ya uwajibikaji kwa upande wa matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, napenda nimalizie kusema kwa vile makosa mengi ya kiutendaji katika ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 ni yale yale yaliyopigiwa kelele na kukemewa na Kamati ya *PAC* kwa ripoti zake zote zilizotangulia. Makosa ambayo hutendeka wakati wa ukaguzi na kuthibitishwa na kamati. Kwa kuwa kufanya makosa hayo ni kwenda kinyume na sheria na kanuni za fedha na sheria za manunuzi ya mali ya umma. Kwa kuwa serikali haioneshi dalili ya kuwachukulia hatua watendaji wanaokiuka sheria hizo. Mhe. Naibu Naibu Spika, naomba muongozo wako juu ya kamati yetu nini kitaendelea baada ya hapo. Nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali naomba nitoe pongezi za dhati kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri sana walizozifanya. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 inaonesha bado kuna mambo yanayokwenda kinyume na kanuni za fedha ambayo yamekuwa yakijirudia rudia katika kila ripoti ya ukaguzi inapowasilishwa hapa Barazani.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuendelea na kazi hizi za ukaguzi zisizokuwa na hata mabadiliko yoyote ya kiutendaji zinakwenda kinyume na kanuni zetu na kupoteza fedha za walipa kodi bure.

(b) Je, serikali inaahidi nini juu ya kurejea makosa kama haya katika ripoti za kila mwaka hasa zinapowasilishwa hapa Barazani. Au Mhe. Waziri, ripoti hizi huwa zinawasilishwa hapa tuone tu jinsi ya uwajibikaji katika taasisi na mawizara ya serikali yasivyokuwa makini na kuona namna gani viashiria vinavyoonesha ubadhirifu katika ripoti hizi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali matatu kwa Mhe. Waziri kutokana na ripoti yake ya Kamati ya *PAC*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akieleza ripoti yake ameonesha kwamba fedha nyingi kwenye ripoti ya *CAG* zimepotea katika malipo yasiyo na mikataba. Kwa mujibu wa sheria za fedha malipo ambayo yanatolewa pasipo na taratibu za kifedha ni kosa kwa mujibu wa sheria.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa sababu ripoti imeonesha wazi wazi kwamba watendaji wa serikali wamelipa fedha bila ya kuzingatia mikataba na hii ni dhahiri kwamba kunakuwa na mwanya wa wizi. Sasa nini itakuwa hatua ya serikali kwa watendaji wote ambao wamehusika na matumizi haya.

(b) Miaka miwili nyuma Wizara ya Fedha kupitia kitengo chake cha Mitaji ya Umma kiliandaa mfumo mzuri wa daftari la kuwekea mali za serikali *(asset register)* na kusambaza katika wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hapa Zanzibar. Ni kwa nini hadi leo idara na wizara za serikali hazijatumia mfumo ule wa kuhifadhi mali za serikali.

(c) Kwa kuwa ripoti za *PAC* zinaonesha kwamba kila mara hutolewa mapendekezo juu ya ubadhirifu wa mali za umma. Kwa kuwa watendaji wa serikali yenyewe haioneshi mabadiliko yoyote katika ripoti ya *PAC*. Sasa Mhe. Waziri unashauri nini kwa Baraza hili juu ya uamuzi wa kuchukuliwa kwa sababu ripoti zake zinadharauliwa hakuna hatua inayochukuliwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri ni hatua gani zinazochukuliwa na serikali kwa watendaji wanaokiuka sheria na kuiba ama kupoteza fedha za umma.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yangu kwa kukalia kiti cha Naibu Spika hapo ukiwa umependeza kabisa. Nikutakie kila la kheri *inshaallah* katika kazi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nimuulize swali Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, kutokana na masuala ambayo yameulizwa hapa na wajumbe wenzangu na kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya ripoti kama hizi kutokuchukuliwa hatua na kwa hivyo mambo yake kuendelea kujirejea.

Je, Mhe. Waziri haoni kama kuna haja ya kumshauri Mhe. Rais kuanzisha utaratibu ambao ulianzishwa na upande wa pili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ingawa nao haukuendelezwa. Lakini ulikuwa utaratibu mzuri wa kuwa na mkutano kila baada ya kutolewa ripoti hii ambayo inahusisha Viongozi Wakuu wa Serikali na Wajumbe wa Baraza kujadili ripoti hii kwa pamoja na kudai maelezo kuhusiana na yale mambo ambayo yamehojiwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Haoni kwamba kuna haja ya kuiga mfano huu mzuri hapa Zanzibar kuhusiana na ripoti hizi ziweze kufanyiwa kazi na zilete ile tija ambayo imekusudiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nirejee tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha tena kusimama hapa na kuja kutekeleza wajibu wangu. Lakini pili nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, Mhe. Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chake Chake ndugu yangu Omar Ali Shehe pamoja na wajumbe wake wa kamati kwa maelekezo yao ambayo wameyatoa juu ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Ni imani yangu kwamba baada ya mimi kuwasilisha muhtasari wa taarifa hii na wajumbe kuchukua vitabu hivi kama nilivyosema kwenye muhtasari wangu kwamba wajumbe watakwenda kuufanyia kazi na wadau wakubwa kwa niaba ya Baraza ni kamati hii ya *PAC*. Ni imani yangu kwamba kamati hii ina uwezo wa kutosha kuweza kuja na taarifa ya kulisaidia Baraza juu ya ripoti hii. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana wewe pamoja na wajumbe wako wa Kamati ya *PAC* hasa tukizingatia kwamba kamati hii na wizara yangu kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanazungumza lugha moja kuichunguza serikali.

Baada ya shukurani hizo Mhe. Naibu Spika, mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine karibu wote waliosimama kwanza wameshangazwa na suala zima la kukerwa na kurejewa rejewa kwa makosa ambayo yameainishwa kwenye ripoti

hii na pengine kutakiwa kujulikana serikali inachukua hatua gani katika jambo hili. Sasa badala ya kumjibu mtu mmoja mmoja naomba niwajibu kwa jumla.

Ripoti hii kama mnavyojua kwamba inaandaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hatimaye huwasilishwa kwa Mhe. Rais ambaye huniagiza mimi kuileta Barazani. Sasa kwa sababu serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu wa saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa imelipa umuhimu suala la utawala bora *(good governance).*

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mara tu baada ya mimi kuagizwa na kuiwasilisha na kitabu hichi kukabidhiwa Kamati ya *PAC* serikali itakaa. Nikizungumza serikali maana yake mnaelewa. Kila waziri atabebeshwa jukumu kwa mujibu wa ripoti inavyoeleza na hatimaye atakwenda kukaa na watendaji wake na kuyafanyia kazi yale yote ambayo yameonekana katika ripoti hii. Naomba niwaahidi kwamba kwa mfumo huo na utaratibu huo sasa nadhani kipindi kijacho hatutopata ripoti ambayo inajirejea rejea.

Mhe. Naibu Spika, la pili ambalo limeulizwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Je, haioni serikali kwamba ripoti hii kujirejea rejea na kutokufanyiwa kazi tutakuwa tunapoteza fedha za umma bure. Mimi nasema kwamba serikali haipotezi fedha za umma bure na ndio maana kuna mgawanyo huu wa madaraka kati ya mihimili hii mitatu. Serikali hii ni sikivu, maoni ya Mhe. Salmin tumeyasikia. Ninachotaka kuwaahidi kama nilivyosema mwanzo kwamba tutahakikisha sasa serikali yale mambo yanayoripotiwa hayajirejei na yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Suala jengine ambalo limezungumzwa ni juu ya ukiukwaji wa sheria ya fedha. Serikali tumesikia kwamba tutaiangalia Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ili kuhakikisha kama kuna mapungufu tuweze kuyafanyia kazi, kama kuna mwanya unaowafanya baadhi ya watendaji wa serikali (watumishi wa umma) juu ya ubadhirifu, basi tutaviondosha vipengele hivyo au tutavirekebisha ili kuona kwamba sheria hiyo haitoi mwanya wa kuweza pengine kutoa adhabu ndogo na kufanya mambo mengine.

Lakini jengine ambalo serikali inaendelea nalo na italitekeleza kwa umakini sana ni juu ya suala la kuwa na chombo cha rushwa. Hivi sasa nchi yetu ya Zanzibar hatuna taasisi hii. Wizara yangu katika kutekeleza suala zima la utawala bora tayari imeandaa Sera ya Utawala Bora na hivi karibuni tunatarajia kuipeleka serikalini ambayo hiyo yenyewe inatupa njia za kuweza kukamilisha sheria ya kuzuia rushwa na maadili ya viongozi.

Sasa tutakapofikia huko hii mianya mingine itakuwa haipo. Lakini je, hivi sasa watendaji ambao watabainika kufanya makosa bila shaka sheria ziliopo zitachukua mkondo wake na kuweza kuwachukulia hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, limeulizwa swali lakini zaidi umeulizwa wewe kwamba muongozo wako ni nini juu ya hili. Sasa hilo naomba nikuachie mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jengine lililoulizwa naomba radhi nimeyajibu kwa jumla kwa sababu maswali yote yalikuwa yanalingana. Naomba nijibu swali la mwisho kabla ya mwisho kabisa. Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kulihakikishia Baraza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haingiliwi anapofanya kazi zake. Ushahidi wa hilo ni hiyo ripoti ambayo mnaiona. Ripoti hii amepelekewa Mhe. Rais na baada ya kuipitia ameona mdhibiti ametekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, hakuna pahala serikali ilipomwambia kwamba kwenye ukurasa fulani kwa sababu haya masuala yanaihusu serikali nenda kafute. Mhe. Naibu Spika, naomba nilithibitishie Baraza lako tukufu kwamba hilo halipo.

La mwisho kabisa ambalo limezungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu la kuwa na mkutano wa pamoja juu ya kujadili ripoti hii. Sina hakika lakini nadhani kwa kule Bungeni kanuni zao zinawaruhusu kufanya hivyo. Lakini sina hakika naweza nikasahihishwa kama hivyo ndivyo.

Mhe. Naibu Spika, si jambo baya lakini bado nahisi utaratibu huu unamuwezesha kila mjumbe kuweza kuishauri serikali juu ya mambo ambayo yamo humo. Kwa sababu wakati wa bajeti tutakapokuja tutakuja na bajeti ya mdhibiti, hapo sasa Mhe. Mjumbe una nafasi nzuri ya kuweza kutoa maoni juu ya hichi kitabu ambacho umepewa na kuweza kuishauri serikali. Hata hivyo, suala hili wizara yangu italichukua na kwenda kulifanyia kazi na kuona kama Baraza la Wawakilishi linaweza likaweka kipengele katika kanuni zake za kuweza kuandaa mkutano kama huu, basi serikali nadhani itakuwa haina pingamizi.

Kwa hiyo, sisi kama wizara tunalichukua na tunakwenda kulifanyia kazi. Kulifanyia kazi kwetu tutashauriana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili tuone uwezekano kama hilo linawezekana. Kwa sababu halina tabu wala halimkwazi mtu lakini kwa sasa utaratibu wetu ni huu kwamba tunaleta ripoti mwenyekiti anapata nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya kamati na kamati hii inatoa maoni kwa niaba ya Baraza. Hatimaye vile vile kwenye kikao cha mwezi Aprili nadhani mwenyekiti atakuja kutoa taarifa yake kamili kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, naomba niwashukuru wajumbe wote ambao wameuliza maswali, maswali yao yalikuwa yana lengo la kujenga na kututanabahisha au kutukumbusha serikali juu ya yale mambo ambayo wanayahisi wao kuwa si sawa. Ninachoweza kusema tena kwamba wizara yangu itajitahidi kutekeleza na kufuata ushauri lakini zaidi kufuata matakwa ya katiba, sheria na kanuni ziliopo ili kuhakikisha kwamba tunafikia kiwango cha kutekeleza dhana nzima ya utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri, baada ya kutoa maelezo na kujibu maswali, limebaki swali moja liliulizwa limeelekea upande wa Baraza kwangu mimi Naibu Spika. Naomba nimjibu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwamba Baraza kazi yake ni kuisimamia na kuielekeza serikali ichukue hatua kwa mujibu wa sheria juu ya mambo yote waliyoyaona kwenye makosa. Lakini na Baraza likishaipokea ripoti hii inakukabidhini nyinyi Kamati ya *PAC* ili kuifanyia kazi. Kwa hiyo, kilichobakia sasa hivi ni kuwahoji wajumbe juu ya ripoti hii iliyowasilishwa, ikishakupokelewa na Baraza basi tutakukabidhini kwa kuifanyia kazi.

Suala la mwisho kwa kuhitimisha mada yetu hii, naomba sasa hivi niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali iliyowasilishwa hapa na waziri je, mmeipokea wanyooshe mikono walioipokea. Walioikataa. Walioiopokea wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kwa hivyo, ripoti hii tutawapa Kamati ya PAC na tutajitahidi kutafuta siku za kutosha ili kazi iweze kukamilika. Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu nambari 6 y 2001 na Kuweka Sheria Mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inatoa fursa mbali mbali za kupata elimu ya juu kwa vijana wanaomaliza elimu ya sekondari ya juu hapa nchini. Fursa hizo za masomo ya juu zimekuwa zikitolewa kwa vijana wenye sifa za kujiunga katika vyuo vya elimu ya juu ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwapatia mikopo ya fedha za kulipia ada na huduma nyengine muhimu za kuwawezesha kusoma katika taasisi hizo.

Mikopo hiyo imekuwa ikitolewa na serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mfuko wa elimu ya juu ulioanzishwa mwaka 2002 mara tu baada ya kupitishwa sheria nambari 6 ya uanzishwaji wa mfuko wa elimu ya juu ya Zanzibar ya mwaka 2001.

Tokea kuanzishwa kwa mfuko huo, idadi ya vijana wenye sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Kwa mfano, mwaka 2010/2011 jumla ya vijana 1073 wametimiza sifa za kujiunga na mafunzo katika taasisi ya elimu ya juu na walistahiki kupatiwa mkono katika mfuko huu. Hata hivyo, ni waombaji 700 tu ndio walioweza kupatiwa mikopo kutokana na uchache wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu unapendekeza kuanzishwa kwa sheria ya kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ya mwaka 2011, kuchukua nafasi ya sheria nambari 6 ya mwaka 2001 ya Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar ya mwaka 2001, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, anakuwa moja kwa moja Katibu wa Mfuko wa Elimu ya Juu kutokana na dhamana yake. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya vijana wenye sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu, imekuwa ni vigumu kwa Mkurugenzi huyo kuweza kuhudumia idara na mfuko wa elimu ya juu kwa wakati mmoja. Mswada huu unapendekeza kuundwa kwa bodi inayojitegemea wenyewe.

Vile vile mswada huu unapendekeza kuongezwa kwa idadi ya wajumbe wa bodi ya mikopo ya elimu ya juu, kutoka wajumbe 6 waliokuwepo katika mfuko wa elimu ya juu hadi wajumbe 10. Ongezeko hilo la wajumbe limezingatia ongezeko la idadi ya waombaji mikopo na pia kutoa uwakilishi mpana zaidi wa taasisi zinazohusika na mahitaji ya watendaji kazi, fedha na mipango ya maendeleo na uwakilishi wa taasisi za elimu. Kuongezwa kwa idadi ya

wajumbe kutaiwezesha bodi kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya idadi ndogo ya wajumbe waliopo katika mfuko wa elimu ya juu, sheria ya uanzishwaji wa mfuko wa elimu ya juu ina kasoro katika taratibu za kuwafanya waliofaidika na mikopo hiyo kurejesha fedha walizokopeshwa mara baada ya kumaliza masomo na kuajiriwa.

Sheria mpya imeweka utaratibu wa wazi wa kuwataka wanaofaidika na mikopo hiyo kurejesha fedha hizo kwa awamu mara tu watakapomaliza masomo na kupata ajira. Pia imeweka wazi majukumu ya muajiri na mdhamini katika suala zima la kurejesha mikopo hiyo. Utaratibu uliowekwa katika sheria inayopendekezwa utaiwezesha bodi kukusanya madeni na kuzitumia fedha hizo kwa kutoa mikopo kwa waombaji wapya.

Muundo wa Sheria

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya Sheria ya Uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar, imegawika katika sehemu kuu 6. Sehemu hizo ni hizi zifuatazo.

Sehemu ya Kwanza

Sehemu hii imeainisha jina la sheria husika, taratibu za kuanza kutumika kwake na tafsiri ya maneno muhimu yaliomo katika sheria.

Sehemu ya Pili

Sehemu hii ya sheria inatoa maelezo ya juu ya uanzishwaji wa bodi, wajumbe wa bodi, majukumu yake na taratibu za vikao vya bodi na namna ya kufikiwa kwa maamuzi. Sehemu hii inaendelea kwa kueleza uundwaji wa kamati za bodi na wajumbe wake, kamati muhimu ni kamati ya elimu ya juu ambayo itakuwa inashughulikia kupitia kwa maombi ya wanaotaka mikopo na kupendekeza waombaji wanaostahili kupatiwa mikopo kwa mujibu wa fedha zilizopo.

Vile vile kamati itashughulikia suala la kuwepo mikataba baina ya bodi na wakopaji. Sehemu hii pia inazungumzia kuhusu uteuzi wa Mkurugenzi ambaye atakuwa ndiye Katibu wa Bodi na majukumu yake.

Sehemu ya Tatu

Sehemu hii inazungumzia kuwepo kwa mfuko wa mikopo ya elimu ya juu na madhumuni yake.

Sehemu ya Nne

Sehemu hii inazungumzia kwa jumla kuhusu mikopo na taratibu zake. Pia inazungumzia jukumu la muombaji mkopo, mwajiri na wadhamini wa muombaji mkopo. Sehemu hii inaendelea kwa kuweka utaratibu wa warejeshaji wa mikopo hiyo na adhabu kwa atakayeshindwa kurejesha mkopo.

Sehemu ya Tano

Sehemu hii inaelezea vianzio vya fedha vya mfuko ikiwemo ruzuku inayotolewa na serikali, inayopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Fedha zinazotolewa kama msaada au zawadi na watu binafsi, wafanyabiashara na wahisani mbali mbali.

Pia sehemu hii inazungumzia vianzio vyengine vya mapato ikiwemo mikopo ya huduma zinazotolewa na bodi, fedha za marejesho ya mikopo na faini watakazotozwa watakaoshindwa kurejesha mikopo kwa wakati.

Sehemu ya Sita

Sehemu hii ya sita ambayo ndio ya mwisho imeelezea kuhusu uwezo wa waziri anayeshughulikia elimu, kuandaa kanuni mbali mbali za utekelezaji wa sheria hii. Sehemu hii inamalizia kwa kueleza ufutwaji wa sheria nambari 6 ya uanzishwaji wa mfuko wa elimu ya juu ya mwaka 2001.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya mswada huu yatasaidia sana katika kuimarisha na kufanikisha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa vijana wetu wenye sifa za kielimu za kujiunga na mafunzo ya elimu ya juu ambao baadhi yao bila kupatiwa mikopo hawatakuwa na uwezo wa kifedha wa kujihudumia wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, naomba ridhaa ya Baraza lako tukufu chini ya uongozi wako kupitisha sheria hii kwa manufaa ya vijana wetu na maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jami Kuhusu Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Zanzibar

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumkushuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa mara ya kwanza tangu kuingia katika Baraza hili kuwa Mwenyekiti wa Kamati nikiwa mzima wa afya njema, kwa lengo la kuwasilisha mchango wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusu Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa wajumbe wa kamati na watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mashirikiano ya kutosha wakati wa kuuupitia na kuuchangia mswada huo. Napenda kusema kwa niaba ya kamati tunawashukuru kwa dhati watendaji hao.

Mhe. Naibu Spika, ningependa pia kuwashukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wanasheria wetu wa Baraza, kwa kutoa mchango wa kutosha kwa kutupa muongozo na ufafanuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo na kabla kuanza kutoa maoni au mchango wa Kamati kuhusu mswada huu, ni vyema kukutambulisha kwa kuwataja wajumbe 10 wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambao walihusika katika kuupitia Mswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ambao wajumbe wa Baraza lako tukufu nao watapa nafasi ya kutoa baraka zao juu ya Mswada huu muda mfupi baadae. Wajumbe hao ni:-

1.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3	Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4	Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
8	Mhe. Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9	Nd. Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
10	Nd. Talib Enzi Talib	Katibu

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umelenga kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya juu nambari 6 ya mwaka 2011 na kuweka Sheria mpya itakayojulikana kama Sheria ya kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Zanzibar.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kuwa suala la upatikanaji wa elimu ni muhimu katika maendeleo ya taifa na ustawi wa watu wake. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitoa fursa mbali mbali za elimu kwa vijana wake wenye sifa wanaomaliza elimu ya sekondari ya juu kwa kuwapatia mikopo ya fedha za kulipia ada na huduma nyengine muhimu za kuwawezesha kusoma. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikitoa mikopo hiyo kupitia Mfuko wake wa Elimu ya Juu ulionzishwa kupitia sheria nambari 6 ya mwaka 2001.

Mhe. Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Sheria ya Mfuko huo idadi ya vijana wenye sifa ya kujiunga katika elimu ya juu, imekuwa ikiongezeka hali ambayo pamoja na mambo mengine kamati yetu inaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuona umuhimu wa kuwa na chombo cha kisheria kitakachosimamia mabadiliko hayo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Kwa mfano, sheria mpya itakayoanzishwa, itatoa uwezo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kujitegemea zaidi na kwamba Bodi hiyo itaongozwa na Mkurugenzi ambae atakuwa Katibu wa Bodi. Hatua hii imefikiwa kutokana na kuonekana kwamba imekuwa ni vigumu kwa Mkurugenzi wa Mfuko wa Elimu ya Juu, kuweza kuhudumia sambamba taasisi aliyokabidhiwa, kwa maana ya idara, na Mfuko wa Elimu ya juu kama inavyoelekeza sheria iliyopo.

Mhe. Spika, kamati yetu pia inaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuzingatia haja ya kuongeza uwakilishi wa wajumbe wa bodi ya mfuko katika sheria mpya itakayoanzishwa. Hoja ya serikali juu ongezeko hili la wajumbe wa bodi ni kwamba bodi itakuwa na uwakilishi mpana wa waombaji kupitia taasisi zao za utoaji elimu, fedha na mipango ya maendeleo. Hoja hiyo tumeiona ni ya msingi kwa vile uwakilishi huo unaweza ukachangia kuleta ufanisi katika maendeleo ya mfuko.

Mhe. Naibu Spika, sheria mpya itakayoazishwa inakusudia kuweka utaratibu wa wazi wa kuwataka wanaofaidika na mikopo hiyo kurejesha fedha hizo wakati wanapomaliza masomo yao na kupata ajira. Lengo la kufanya hivyo ni kuujengea uwezo Mfuko wa Bodi ya Mikopo kuwafikia wengine wenye sifa kwa ajili ya kuwasaidia katika maendeleo ya upatikanaji wa elimu ya juu nchini. Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu iliyopo imeonekana kuwa na mapungufu juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inasisitiza kuwa sheria mpya itakayopitishwa ni vyema ihakikishe kuwa inadhibiti vyanzo wa upatikanaji wa mapato ya Bodi ya Mikopo ili kuwepo na uhakika kwa maendeleo ya baadae ya mfuko wa mikopo.

Kabla ya kuingia moja kwa moja katika marekebisho ya kamati yetu ya mswada huu, kwa ujumla napenda kusema kuwa mswada huu umezingatia mapendekezo ya maeneo muhimu ikiwa pamoja na kuweka wazi majukumu ya muajiri na mdhamini pamoja na adhabu kwa mtu yeyote atakayeshindwa kuandaa utaratibu wa malipo na mkopaji, yenye lengo la kuhakikisha kuwa fursa ya upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu na urejeshwaji wake kwa vijana wetu, inaleta ufanisi katika maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Mhe. Naibu Spika, kamati imepitia mswada na kufanya marekibisho ya mapendekezo yafuatayo:-

Katika sehemu ya kwanza katika ukurasa wa 78 marekebisho yaliyofanywa na kamati katika maana ya Maneno, neno “Mdhamini” ni kuwa pamoja na sifa nyengine zilizotajwa katika mswada ni kwamba pia awe na mali ambayo inaweza kuhamishika na iliyosajiliwa hali hii itaweza kutoa fursa zaidi kwa Wadhamini ambao hawana mali zisizo hamishika .

Mhe. Naibu Spika, katika sehemu ya nne Kamati imefanya marekebisho juu ya neno “Msaada” lisomeke mkopo. Sababu ya msingi ni kwamba sheria ilinayoanzishwa inahusiana na kutoa mikopo, sio misaada kwa wanafunzi, kwa njia mbali mbali ambazo zimeainishwa ndani ya mswada huu. Aidha, marekebisho mengine ya jumla ni kukurekebisha baadhi ya makosa madogo madogo ya kiuandishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kuwepo katika Baraza lako hili tukufu, kwa madhumuni ya kujadili mswada wa sheria unaohusiana na masuala ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuona umuhimu wa kubadilisha sheria ya mfuko wa elimu ya juu ya mwaka 2001 na kuanzisha sheria mpya ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar. Nampongeza sana kwa hatua hiyo, baada ya kuona kwamba sheria ya mwaka 2001 tayari imeshapitwa na wakati na ina mapungufu na kwa sababu ni zaidi ya miaka 10 sasa tokea kupitishwa kwa sheria hiyo.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba na Waheshimiwa Mawaziri wengine waige mfano kama huo, pale wanapoona kwamba sheria imeshatumika kwa muda mrefu na inahitaji kufanywa marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa hivi wako katika mchakato wa kupokea maoni juu ya wananchi kuhusiana na suala la bodi kama hii ya mfuko wa elimu ya juu, na kwa sababu tayari mfuko huo ambapo na sisi Zanzibar tunahusika umekuwa na malalamiko mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, kwetu sisi Zanzibar pamoja na kwamba sheria hii iliyopita inaonekana ilikuwa na mapungufu, lakini bado hakujawa na malalamiko mengi kiasi cha wanafunzi wa elimu ya juu kuandamana. Hiyo inaonesha dhahiri kwamba bado sheria ilikuwa inakwenda vizuri. Lakini Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameona kuna haja ya kufanya hivyo, basi tunamshukuru *Alhamdulillah*.

Mhe. Naibu Spika, suala la kutoa mikopo ya elimu ya juu ni suala muhimu sana na kwa sababu tayari tuna watoto wetu wengi ambao wanafaulu kuendelea na mafunzo yao ya elimu ya juu, lakini kwa bahati mbaya wazee wao wanakuwa hawana uwezo wa kuwaendeleza. Hata kwa wale ambao wanapatiwa nafasi za mikopo basi mikopo ile inakuwa haijatimia kabisa kabisa. Kwa maana hiyo hata baadhi ya wazee wanashindwa kuwaendeleza watoto wao.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi watoto wetu wengi wanajitahidi kusoma na wanafaulu, lakini wanashindwa kuendelea na masomo kutokana na wazee wao kukosa fedha za kuwasomesha.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa mikopo uliopo wa fedha zinazotengwa na serikali unaonekana ni chache mno na zinakuwa haziwezi kukidhi mahitaji ya mikopo kwa wanafunzo wale wanaofaulu. Kwa hivyo, naiomba serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iongeze fungu katika eneo hili muhimu sana, nchi yetu inahitaji wataalamu katika fani mbali mbali na ili watu waweze kuwa wataalamu ni lazima wasome na waweze kupata elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye mswada wenyewe, kuna jamba ambalo wananchi wengi wamekuwa wakililalamikia. Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya kuwaongezea mikataba wafanyakazi ambao sio wataalamu, mikataba ya ajira, jambo hili wananchi wanalilalamikia sana. Sasa tunapowajazisha mikataba ya ajira wale ambao wametimia muda wao wa kuwatumikia. Je, hawa watoto wetu ambao tunawasomesha kwa gharama kubwa wao watafanya kazi gani.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili kwa kweli linasononekewa na linahitaji kuangaliwa kwa makini sana. Wafanyakazi wanaofanya kazi wakafika muda wa kustaafu basi wanatakiwa kustaafu ili watowe nafasi kwa watoto wetu tunaowasomesha kwa gharama kubwa na wao wapate nafasi ya kulitumikia

taifa hili. Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa niingie katika mswada.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya pili ya mswada kifungu cha 3(1) kinaeleza kunaanzishwa bodi ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar, ambapo kifungu cha 4(1) kinaelelezea muundo wa bodi yenyewe, ambapo ametajwa Mkurugenzi kama ni mjumbe wa bodi hiyo, kama niko sawa.

Kifungu cha 4(1)(b), lakini kifungu cha 16(2) kinazungumzia kuwa, Mkurugenzi atakuwa Katibu wa Bodi na atashiriki katika vikao vya bodi, lakini hatokuwa na haki ya kupiga kura kwenye jambo lolote ambalo linahitaji kuamuliwa na bodi. Hapa Mhe. Naibu Spika, naona kidogo pana kasoro, kwa kuwa Mkurugenzi tayari ni mjumbe wa bodi, mimi ninahisi bado ana haki ya kuwa na kura.

Vile vile Mkurugenzi huyu hatakiwi kuwa Katibu wa Bodi ni lazima apatikane mwanasheria, bodi iajiri mwanasheria wa serikali ili mwanasheria yule awe ndio Katibu wa Bodi na kwa sababu chombo hiki tayari kinajitegemea, kina haki ya kushtaki na kushtakiwa basi ni vyema kikawa na mwanasheria na hapa hapaoneshi kwamba kuna mwanasheria katika bodi hii. Kwa hivyo, kuwe na mwanasheria ambaye atatakiwa kuwa ndio Katibu wa Bodi na Mkurugenzi abakie kuwa ni mjumbe wa bodi ambaye atakuwa na haki ya kupiga kura.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 19(2) kinaeleza aina ya mkopo unaotolewa na bodi, naomba kunukuu.

Kifungu cha 19(2)

> " Msaada wa fedha utakaotolewa chini ya kijifungu cha 1 cha kifungu hiki, utasaidia:-"

ambapo neno "msaada" kwa mujibu wa marekebisho limefutwa na pamewekwa neno "mkopo", ambapo pameelezwa maeneo ambayo yatatolewa mkopo, ambayo ni:-

(a) ada ya masomo,
(b) gharama za mitihani,
(c) gharama za chakula na malazi,
(d) vitabu vya kusomea na kuandikia.

Vile vile kuna mtiririko mzima mpaka kufikia bima ya afya. Lakini kwa kuzingatia kwamba bodi itatoa mkopo kwa mwanafunzi kwenye maeneo yalioelezwa katika kifungu cha (2) cha kifungu hiki, kwa kadiri ambayo itaamua.

Mhe. Spika, nadhani hapa hapahitaji maamuzi ya bodi, hapa panahitaji maamuzi ya kisheria, kwa kweli sheria itakapotoa mamlaka ya maamuzi, kwa maana hiyo inawezekana kukawa na vifungu katika maeneo haya havitotolewa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema mwanzo kwamba, uzoefu unaonesha wazee wa watoto wanaosoma elimu ya juu wanashindwa kutoa hata ile asilimia ndogo ambayo wanatakiwa watoe. Kwa mnasaba huo na kwa mujibu wa sheria hii ikiwa gharama hizi zote zinalipiwa na serikali, basi moja kwa moja watoto wetu wanaweza kupata nafasi na kuendelea na masomo ya juu bila ya pingamizi na wala matatizo yoyote pamoja na wazee wao kutohangaika hata kwa ile asilimia ndogo ambayo inatakiwa itolewe.

Katika kifungu cha 19 (5) Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 19 (5) kinasema hivi:-

> "*Endapo Bodi itakuwa imeweka kiwango maalum kwa mujibu wa kijifungu cha 3 cha kifungu hiki, ambacho kila mwanafunzi, mzazi, mlezi na mtu mwengine anayehusika itamlazimu amchangie mhusika kiwango hicho cha fedha ambacho kimewekwa na Bodi".*

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, ikiwa mzazi au mlezi ameshindwa kuchangia hiyo sehemu ambayo bodi imeamua, inamaana mtoto huyu wa mkwezi na mkulima hawezi kuendelea na masomo yake kwa mujibu wa sheria hii.

Vile vile kifungu cha 20 (1) kinazungumzia sifa za kupata mikopo, ambapo kifungu cha 20 (2) Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 20 (2) kinasema hivi:-

> "*Kozi ambayo lakini neno kozi limefanyiwa marekebisho, atakuwa ameiomba lazima iendane sambamba na kozi zilizowekwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo".*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza kuhusu huu Mpango wa Taifa wa Maendeleo, kwamba nani anaweka hivyo vipaumbele, ambapo kozi hii ni muhimu na ile si muhimu, wakati kozi zote hizi tayari zipo katika vyuo. Mimi ninavyoelewa ni kwamba kozi zote ni muhimu, isipokuwa inategemea na mwanafunzi mwenyewe anavyopenda, sasa ikiwa tutaweka vipaumbele kwamba tusomeshe hili na hili, lakini lile tusilisomeshe na ikiwa yule

mwanafunzi anahitaji kusoma somo lile na kwa kuwa anasoma somo ambalo halikuekewa kipaumbele, basi itakuwa mwanafunzi hawezi kupata mkopo.

Kwa maana hiyo itakuwa hatuwatendei haki, yaani itakuwa hatuwapi uhuru watoto ambao wanataka kusoma masomo yale na hawataki kusoma masomo haya. Kutokana na hali hiyo, itakuwa tunawalazimisha lazima wasome masomo fulani.

Kwa hivyo, nadhani eneo hili linahitaji marekebisho Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 23 (1) kinazungumzia wajibu wa muajiri, ambapo kifungu cha 23 (1) (c) naomba kunukuu.

Kifungu cha 23 (1) (c) kinasema hivi:-

> *"Muajiri atalazimika kulipa kwa Bodi mkato kutoka kwenye mshahara wa mkopaji au mafao ndani ya siku kumi na tano ya kila mwezi katika utaratibu utakaowekwa na Bodi*".

Mhe. Naibu Spika, nafikiri siku kumi na tano zilizowekwa kwenye sheria ni nyingi na badala yake zipunguzwe na ziwe angalau siku kumi. Katika kipindi hicho muajiriwa anakuwa tayari ameshakatwa mshahara wake na muajiri, sasa kwa nini ziwekwe siku kumi na tano. Kwa hivyo, iwe ndani ya siku kumi tayari fedha zile ziwe zimesharejeshwa katika bodi, ili fedha hizi ziweze kutumika kwa wanafunzi wengine wanaohitaji mikopo.

Nikiendelea na mchango wangu katika kifungu cha 24 (1) hadi kifungu cha 28 vinazungumzia juu ya ulipaji wa mikopo, ambapo vifungu hivi vyote kwa ujumla vimetoa maelezo mbali mbali.

Kutokana na hali hiyo, naomba kutoa ushauri kwa Mhe. Waziri, baada ya kupitishwa kwa sheria hii na Mhe. Rais alikubali kwa kutia saini, basi ni lazima kuwe na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi, kwa sababu humu mnazungumziwa masuala mbali mbali ya ulipaji, udhamini pamoja na mambo mengine, ili wananchi wapate kuelewa sheria hii.

Mhe. Naibu Waziri uzoefu unaonesha kwamba wananchi wengi hawaelewi sheria hizi, kwa hivyo, wanaweza kuja kuingia katika kudhamini na mambo mengine, lakini wakawa hawajui taratibu za sheria. Kwa maana hiyo, bodi inapoanzishwa iwe na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi, ili wajue nini wajibu wao juu ya ulipaji wa fedha hizo, vyenginevyo tutakuja kuwatia hatiani kwa jambo ambalo hawalielewi.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 27 (1) kinazungumzia adhabu, ambapo kifungu cha 27 (1) kinazungumzia kuhusu suala la riba ya benki, naomba kunukuu.

Kifungu cha 27 (1) kinasema hivi:-

> *"Muajiri yeyote, mdhamini au mtu mwengine yeyote atakayeshindwa au kucheleweshe kuwasilisha malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Bodi ndani ya muda uliowekwa, atapewa adhabu ya kulipa iliyosawa na riba ya Benki".*

Sasa hapa kidogo nimejiuliza hii riba ya benki ni benki ipi, kwa sababu mabenki yote yanatofauti ya riba. Kwa mfano, wengine wana-*charge* asilimia 20, wengine 16 ama 15. Nadhani ni vyema ingeainishwa hii riba ya kibenki ni asilimia ngapi.

Vile vile katika kifungu cha 27 (2) katika sehemu hii ya adhabu kinazungumzia juu ya adhabu Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 27 (2) kinasema hivi:-

> *"Mtu yeyote aliyemuajiri au aliyempa dhamana ya mkopaji na akashindwa kuandaa utaratibu wa malipo na mkopaji, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalazimika kulipa faini ya shilingi milioni tano au kutumikia kifungu cha muda usiopungu miezi kumi na mbili ama adhabu zote mbili ya faini na kifungo".*

Mhe. Naibu Spika, hali hii inaonesha dhahiri kwamba elimu ya kutosha inahitajika kuhusiana na masuala haya, ili kuona wananchi wetu pale ambapo watakwenda kuwadhamini watoto wao na adhabu ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria hii. Lakini vyenginevyo tunaweza kuwatia hatiani kwa jambo ambalo hawalielewi, pamoja na kwamba kutokujua sheria sio kusameheka na adhabu katika sheria.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tano ya mswada inazungumzia masharti ya fedha, ambapo kifungu cha 28 (a) kinazungumzia fedha ambazo zitatolewa na Baraza la Wawakilishi kwa Bodi.

Kwa kweli hapa ndipo kwenye tatizo Mhe. Naibu Spika, nadhani ni vyema tukaiomba serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya jambo hili muhimu, ili kila mtoto ambaye atakayekuwa na sifa ya kuendelea na masomo au kupata mafunzo, basi fedha za kutosha ziwepo kwa lengo la kuwakopesha wanafunzi wetu hawa. Pamoja na kuzingatia kifungu cha 5 (a) naomba kunukuu.

Kifungu cha 5 (a) kinasema hivi:-

> *"Kutoa mikopo kutoka kwenye mfuko kama ambavyo Bodi itaona inafaa, kwa mtu yeyote mwenye sifa, ili kuwezesha kusaidia mwanafunzi yeyote kulipia gharama za elimu ya juu".*

Kwa maana hiyo, mikopo hii itatolewa kwa wale wote wenye sifa na wala hakutokuwa na ubaguzi au malalamiko kwamba mimi nimekwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kukosa mkopo kwa mujibu wa kifungu cha 5 (a) kwa mtu yeyote mwenye sifa. Kwa maana hiyo, mwanafunzi yeyote aliyefaulu na kuwa na sifa basi atahitaji kupewa mkopo.

Kutokana na hali hiyo, ni lazima serikali iweke fedha za kutosha kwa ajili ya mfuko huu, ili kukidhi haja ya watoto wetu hawa ambao wanapata nafasi ya kuendelea na masomo yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu mafupi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono Mswada huu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya 2011, pia tunaiomba serikali katika bajeti inayokuja iweke fedha za kutosha katika mfuko, vyenginevyo mfuko huo tutaurejesha huko kwao na kwa sababu uwezo huo tunao, maana mifuko hiyo tunaipitisha hapa katika Baraza letu.

Kwa kweli huu tutauangalia kwa makini sana kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu na kwa vile tunajua wananchi wetu wanahangaika na wakati mwengine wanauza rasilimali au amana zao kwa lengo la kuwasomesha watoto wao. Kwa hivyo, tunaiomba serikali itenge fedha za kutosha, ili mambo haya ya matatizo yasiweze kuendelea na kila mmoja aweze kupata haki yake kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya pili ya uchangiaji katika mswada huu. Nachukua fursa hii kumshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima, afya na tukaweza kuzungumza katika majilisi hii tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nitoe pongezi sana kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mhe. Waziri mwenyewe, kwa kuona ipo haja baada ya malalamiko mengi ambayo yalikuwa yakitolewa kuhusu utaratibu mzima wa kupata mikopo kwa wanafunzi wetu.

Kwa kweli sisi wenyewe tulikuwa tukiulizwa maswali mengi kama Wawakilishi kuhusiana na utaratibu wa utoaji mikopo ambao ulikuwa hauko wazi katika kila hali. Kwa hivyo, kuanzishwa kwa chombo ambacho tungekitarajia kikawa na uwazi pamoja na upeo zaidi, ili tuweze kuendeleza shughuli za elimu ya juu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nataka niingie moja kwa moja kwenye mswada wenyewe nianzie na kifungu cha 4 cha mswada huu kinachozungumzia kuhusu wajumbe. Kuhusu suala la Mkurugenzi kuwa ni mjumbe na halafu akakataliwa si mjumbe nitakuja kulizungumza baadaye tukijaaliwa.

Lakini nianzie kwenye kifungu cha 4 (c) kifungu kidogo (i), (ii), (iii) na (iv) wajumbe wenye ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Katibu wa Tume ya Mipango na Mkurugenzi wa Utumishi. Kwa kweli tatizo halipo hapo Mhe. Naibu Spika, isipokuwa tatizo lipo pale unaposema au mwakilishi wake, nadhani si sahihi kusema au mwakilishi wake ikiwa hatukuongeza kitu chochote, kama tunahisi Katibu Mkuu asingepata nafasi basi tungesema mwakilishi wake wa kudumu.

Kwa hivyo, Katibu Mkuu ateue mwakilishi wake wa kudumu atakayewakilisha katika bodi hii, lakini kusema mwakilishi wake inawezekana siku moja akaenda yeye na siku nyengine akamtuma mwengine na kikao kikakosa *sequence* nzuri, kwa sababu leo anakuja mjumbe huyu na kesho anakwenda mengine sasa bodi hiyo itakwenda vipi.

Mhe. Naibu Spika, nadhani si vyema kusema au mwakilishi wake tukasita hapo awe mwakilishi wake wa kudumu. Kwa hiyo, vifungu vyote vinne napendekeza kwa Mhe. Waziri isomeke kwamba au mwakilishi wake wa kudumu, kama Katibu Mkuu akijitoa kuwakilisha yeye, basi atakayempeleka pale awe wakudumu ili ile kamati iwe na *sequence* nzuri katika mazungumzo yao pamoja na vikao vyao. Hilo la mwanzo.

Nikiendelea na mchango katika kifungu cha 5 kuhusiana na kazi za bodi. Nadhani kazi zilizotajwa pale hazikukamilika, kwani ipo kazi moja ambayo ni muhimu sana haikutajwa kwenye kazi za bodi. Kuhusu suala la upangaji wa bajeti mbili katika bodi hiyo.

Kwanza kuna upangaji wa bajeti ya bodi yenyewe pamoja na uendeshaji wake, pia kuna bajeti hiyo aliyoizungumza mzungumzaji wa mwanzo, yaani ile bajeti ya mkopo wenyewe na lazima waipange, kwa sababu wana-*focus* wanafunzi wangapi tunatarajia, gharama yao ni kiasi gani. Kwa hivyo, wao ndio tungewatarajia kwamba watapata ile bajeti itakayoombwa katika Baraza la

Wawakilishi, ili iidhinishwe kwamba ndio bajeti au *fund* ya mkopo utakaokuwepo kwa ajili ya kukopeshwa wanafunzi.

Kwa hivyo, kazi hii kama imeondolewa bajeti hii ya wanafunzi atapanga nani pamoja na ile yao wenyewe ya kufanyakazi. Mhe. Naibu Spika, napendekeza kwa Mhe. Waziri kiongezwe kifungu kimoja cha kuoneshwa kwamba kazi za bodi moja wapo ni kupanga bajeti kwanza ya uendeshaji wa shughuli zao na pili bajeti ya *fund* ya mkopo wenyewe itakayokuwepo kwa ajili ya kukopeshwa hao wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, suala la tatu katika mchago wangu ni utatanishi uliopo baina ya Mkurugenzi Mjumbe wa Bodi na Mkurugenzi si Mjumbe wa Bodi. Wakati nilipokuwa nikilisoma Gazeti Rasmi la Serikali Mhe. Naibu Spika nilihisi labda kuna Wakurugenzi wawili, kwa sababu huyu wa kwanza alitajwa tu kwamba ni Mkurugenzi, lakini katika kifungu cha 16 akatajwa tena kwamba huyu Mkurugenzi ndiye atakayekuwa Katibu wa Bodi na nilipiga mstari hapa alipoambiwa kuwa hatokuwa na haki ya kupiga kura. *(Makofi)*

Sasa nikasema kwamba kifungu cha kwanza kimemkubali kwamba ni Mjumbe wa Bodi na kifungu cha pili cha 16 (2) kikamkataa kwamba huyu si Mjumbe wa Bodi. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anifafanulie vizuri kupitia kwako Mhe Naibu Spika, kuhusu suala hili, kwamba huyu Mkurugenzi ni Mjumbe wa Bodi au vipi.

Nadhani pendekezo alilotoa Mhe. Salmin Awadh Salmin lingefaa kwamba Mkurugenzi abaki kuwa Mjumbe wa Bodi, kwa sababu yeye ndiye atakayepeleka zile sera za wizara katika ile bodi kwa wale watakaohudhuria. Lakini katibu awe Mwanasheria, ili mambo yaende sawia kama washairi wanavyosema.

Mhe. Naibu Spika, na Mwenyezi Mungu atakupa Uspika.

Mhe. Naibu Spika: Amin. Lakini na mwenyewe anasikia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nimeshazoea kwa sababu miaka mitano iliyopita hatukupata fursa ya kuzungumza na Naibu Spika, kwa hivyo tumeshazoea tuchukulie tu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 11 cha mswada huu kinatatanisha kidogo, kwa sababu mbili zifuatazo. Kwanza naomba kuuliza Bodi hii haina *secretariat* kwa sababu haikutajwa humu na bodi zote huwa na *secretariat*. Ukitizama kifungu cha 12 kazi zilizoandikwa pale za kamati ndogo ni kazi za *secretariat*.

Kwa hivyo, badala ya kusema kamati ndogo, basi zile ni kazi zote za *secretariat* na yule mwanasheria aliyetajwa huko nyuma ambaye tumempandekeza sisi ndiye mwenye hiyo *secretariat*. Kwa maana hiyo, tatizo moja kubwa ambalo limo katika bodi hii haikuwekwa *secretariat* yake na hilo ni tatizo moja.

Lakini tatizo la pili katika kamati ikiwa itaundiwa kamati ndogo basi mwenyekiti haingii tena katika kamati ndogo, kwa sababu mwenyekiti yeye ni *overall*, kwa hivyo anaweza kuunda kamati ndogo mbili au tatu na yeye akawa huko anasubiri aletewe. Sasa mwenyekiti yule unamwambia bodi ndiye mwenyekiti na kamati ndogo ni mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, nadhani hapa kuna haja wanasheria watusaidie, kwa sababu sisi tumeingia humu si wanasheria, lakini labda wanasheria wametuzidi kidogo.

Kutokana na hali hiyo, nafikiri ni vyema wakatueleza kwamba bodi anakuwa ni mwenyekiti na kamati ndogo pia ni mwenyekiti, kwa sababu aliyetoa *authority* ya kuundwa ile kamati ndogo ni yeye na wala hawezi akajifanya yeye kuwa ni mwenyekiti. Kwa hiyo, hapa bado kuna tatizo, yaani hilo tatizo ni *two in one* utaliona ni moja, lakini linazaa jengine ndani yake.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atufafanulie kuhusu suala hili kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba alipata ushauri kutoka wapi. Kwa kweli nilifikiria kifungu cha 13 ni sahihi kwamba bodi kwa kushirikiana na Mhe. Waziri inaweza kuanzisha kamati nyenginezo si zaidi ya mbili na wajumbe wake watateuliwa kutokana na miongoni mwa wajumbe wa bodi endapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Lakini hizo kamati ndogo na sio *secretariat*, kwa sababu wajumbe wa bodi wao hawawezi kufanyakazi za *secretariat*, isipokuwa wao ni *policy markers* wa kile chombo, yaani ni watungaji sera, wapitishaji wa bajeti, sasa kazi za kupitia fomu pamoja na maombi, wakati bodi tayari imeshaweka sera na utaratibu wake basi *secretariat* ndiyo inayoshughulikia.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mmoja katika wajumbe hapa ni mwakilishi, kwa hivyo ikiwa leo maombi yameshapatikana kule, sasa yule mwakilishi atakayeteuliwa kwa ajili ya kupitia fomu ya mtu mmoja mmoja kwamba huyu anafaa na yule hafai, nadhani hapa kidogo kuna matatizo. Kwa kweli *secretariat* ndio kazi yake na wala sio kamati ndogo, kwa sababu kamati ndogo inaundwa ikiwa kuna dharura ya kushughulikia tatizo fulani.

Katika kifungu cha 16 (4) kuna mazonge mengine kuhusu Mkurugenzi pamoja na maafisa wengine wa bodi wataunda Kamati Tendaji ya Bodi na haya mapya.

Kwa kweli hapa kuna mazonge, kwa sababu Mkurugenzi ambaye sehemu moja ni Mjumbe wa Bodi na wakati mwengine si Mjumbe wa Bodi ni Katibu na halafu yeye pamoja na wajumbe wengine wataunda Kamati Tendaji ya Bodi na hapa kuna mashaka na sisi wengine hatukusoma sheria, lakini tumekaa nao karibu kidogo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi kuhusu suala hili kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba kifungu hiki kimetokea wapi au ilikuwa ile *cut and paste*, maana kuna lugha za *computer* siku hizi unaweza kukikuta kifungu pahala na kukichukua na kukibandika na wala hukukiandika wewe umekikuta tu, ndiyo hiyo *cut and paste*. Kutokana na hali hiyo, inawezekana Mhe. Naibu Spika waliofanya hivyo walifanya hiyo *cut and paste* bila ya kutizama kinatokea wapi au kina mantiki gani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 24 kuna vifungu viwili ambavyo vimenitia mashaka kidogo naomba kunukuu.

Kifungu cha 24 kinasema hivi:-

> *"Itakuwa ni wajibu wa kila mtu aliyefaidika na mkopo chini ya sheria hii kurudisha mkopo wake wa Serikali kupitia Bodi.*
>
> *"Mkopo uliotolewa chini ya kifungu 22 (2) cha sheria hii utalazimika kulipwa haraka na wanafunzi mara tu watakapoajiriwa kama ambavyo bodi inavyoelekeza".*

Sasa naona kutumia neno haraka inawezekana akasubiriwa pale anapopokea siku ile na yeye ni mshahara wake wa mwanzo, pengine ameshaposa anataka angalau akatoe mahari na wewe unakwenda kumkalia pale. Kwa hiyo ni vyema kidogo pangewekwa muda kama vile miezi mitatu au sita baada ya kuajiriwa kwa mujibu bodi itakavyoona tunajijua sote tulimopitia mtu mwezi alioajiriwa na ndogo zake anazokuwa nazo. Basi mtu umlipishe mwezi ule ule alioajiriwa si kitu ambacho rahisi.

Lakini kifungu 24(7) kinasema: Mkopaji yeyote ambaye kwa kipindi cha chini ya miaka miwili atakuwa hakuajiriwa wadhamini wake watalipa deni hili nawatetea wazee, katika nchi jukumu la kuajiriwa ni jukumu la serikali. Si kwamba serikali iajiri watu wote, lakini vijana wake kuwapatia ajira ni jukumu la serikali ndio maana ikawa na huu uanzishwaji wa sekta binafsi na serikali ihakikishe kwamba kuna viwanda vya kutosha, kuna biashara za kutosha, kuna mitaji ya kutosha katika nchi ili vijana wapate ajira.

Sasa ikiwa tumeshamsomesha katika elimu ya juu kashamaliza na hakupata ajira ina maana ni ukosefu na upungufu katika serikali, sasa wanatiwa adabu wale wazee wake kwa upungufu katika serikali kidogo kigungu hiki kina matatizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri akitizame tena kifungu hiki, ingekuwa imeandikwa hapa kakataa kuajiriwa maana anachagua kazi, kapewa ualimu hautaki, kapewa hiki hakitaki. Kwa hivyo kakataa kuajiriwa. Lakini hajaajiriwa kwa maneno haya kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ziwani, nitaunga mkono kwa asilimia mia moja na hamsini ikiwa Mhe. Waziri ataniweka sawa kwa masuala yangu haya.

Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi kutoa mchango mdogo tu kuhusu mswada huu. Mimi nitaanzia pale kwenye kazi za Bodi kwenye (j) ya kazi za bodi kimeelezwa kuwa kupokea zawadi michango, mikopo au vitu vya thamani vinavyotolewa kwa bodi. Hili suala la kupokea zawadi, mikopo na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kuomba na kama bodi ipo tayari kupokea zawadi hofu yangu hapa ni kujichomoza mwanya wa rushwa, watu wengi katika nchi hii tumejijengea mazoe hata lile jambo lililokuwa ni haki yako kupewa basi tumejenga mazingira ya kumfungulia mkono aliyekupa huduma wakati ambapo ni haki yako akupe huduma ile. Inawezekana watu wenye uwezo wakaenda kwenye bodi wakatoa zawadi na thamani ili watoto wao wapatiwe mikopo hiyo.

Mimi nahisi kufungu hiki cha zawadi kwenye kazi ya bodi tungelikiondoa kusiwe na zawadi za itakayotolewa, mchango utolewe kwa kusaidia bodi lakini kusiwe na zawadi, kipindi kilichopita Waziri kasema maombi yalikuwa mengi lakini wanafunzi waliopata ni kama mia saba kama sikosei, sasa kadri siku zinavyokwenda wasomi wanaongezeka na maombi yataongezeka. Kwa hivyo lazima bodi hii iweke vyanzo mbali mbali vya mapato ili iweze kuhimili maombi ya wanafunzi wote wenye sifa za kupata huo mkopo, isiwe mtu kaomba ana sifa lakini anakosa tusiwe na ile kuchagua kuwa wako waliopasi lakini wanakosa nafasi, kila ambae atakuwa na sifa aweze kupata hiyo haki ya mkopo ili aende akasome.

Halafu kile kifungu cha mwisho alichokizungumzia Mhe. Rashid Seif Suleiman kifungu cha saba kuwa pale ambapo mwanafunzi chini ya miaka miwili hakuajiriwa itabidi mkopo huo wadhamini wake walipe, mimi nadhani hawa watu walikopa kwa sababu hawana uwezo na kijana wao bado hajaajiriwa sijui

walipe nini, nadhani kama wangelikuwa na uwezo wasingelikopa. Na mimi naendelea kuungana na wenzangu waliopita kuwa wazee au wadhamini hapa nawatetea kuwa wao wasilipe pale ambapo kijana wao bado hajaajiriwa, ama katika taasisi za serikali au taasisi nyengine yoyote. Kwa hivyo jukumu hili kama kijana hajapata ajira tufikirie mkopo huu utarudi vipi lakini sio kupita kwa mtu aliyemdhamini hali ya kuwa bado kijana wao hajapata ajira yoyote aidha kwenye taasisi ya serikali au taasisi nyengine yoyote ile.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kataja hapa kuwa mkurugenzi hapa ni katibu wa bodi, lakini pia kawekwa katika mambo ya maamuzi yeye hatokuwa na kura, mtendaji mkuu wa taasisi fulani katika maamuzi yeye atakuwa hayumo, hapa kidogo kama walivyosema wenzangu panahitaji marekebisho, huwezi kuwa mtendaji mkuu lakini ikawa huna sauti katika chombo unachokitumikia. Katibu Mkuu yupi aliyekuwa hana mkia, kama katibu mkuu awe na kura ya maamuzi kama walivyo wajumbe wengine.

Mhe. Naibu Spika, huu muda wa mkopo uwekewe muda maalum sio pale mara tu mtu atakapoajiriwa, mimi ningependekeza aanze kulipa mkopo huu miezi sita baada ya kupata ajira wala isiwe mara tu baada ya kuajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussab Ladhu: Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima leo wakati tunajadili mswada huu, pili nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua hii ya kuleta mswada huu wa kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu na kuanzisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ni hatua muhimu sana kwa sababu sote tunajua umuhimu wa elimu katika maendeleo ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka wakati mimi nasoma nipo nchini Uingereza mwaka 1967 wakati kunatokea mabadiliko makubwa ya serikali pale takriban baada ya miaka kumi na saba ya utawala wa Chama cha Conservative, wakati ule aliyekuwa Waziri Mkuu ni Tony Blayer kabla hajaingia madarakani alisema vipaumbele vitatu vya serikali yake mpya vilikuwa ni *Education, Education, Education* kwa hivyo hiyo ni kuonyesha umuhimu wa elimu hata kwa nchi zilizoendelea seuze kama zetu ambazo zinachukua hatua kwa kutaka kuelekea hayo maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni muhimu sana lakini na mimi kabla sijaingia katika mswada wenyewe na kutizama baadhi ya vifungu kulikuwa na baadhi ya mambo ya jumla ambayo ningependa kuyazungumzia.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmini hapa kabla kuletwa kwa mswada huu kumetokana na mapungufu ambayo yameonekana katika sheria illiyokuwepo ya mfuko wa elimu ya juu, hili mimi naomba nilitilie mkazo kidogo, vijana wetu wengi sana wamekuwa wakitufuata wakilalamika sana juu ya suala zima la uendeshaji wa uliokuwa mfuko wa elimu ya juu fedha hata kwa wale ambao wanapatiwa mikopo haziingizwi kwa wakati zinachelewa mno, mpaka wakati huu tunaozungumza kuna wanafunzi wamefanya mitihani mwezi uliopita na wengine mwezi huu lakini hawajaingiziwa fedha, imekuwa ni utaratibu uliozoeleka sasa kwamba kila kikifika kipindi cha mitihani katika vyuo vya Elimu ya Juu hata vikiwemo Tanzania wanafunzi wa Zanzibar wanakuwa wanyonge wanafika kubandikwa orodha za mitihani hawamo, mpaka Wizara ya Elimu itoe barua kusema kwamba waruhusiwe kufanya mitihani baadaye malipo yao yatafuata, limekuwa ni tatizo sugu au donda ndugu hasa inawasumbua sana sana vijana wetu na wanajisikia unyonge kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kule kusoma kwenyewe ni kugumu sasa baada ya kuwa mtu ashughulikie masomo yake anajiandaa na mitihani basi anafikiria nitaishi wapi na wapi nitakula na huduma za msingi, hili limekuwa likilalamikiwa sana.

Lakini lililonipa moyo pia katika lalamiko la vijana wetu wengi sana ilikuwa ni suala zima la ile mikopo iliyokuwa ikitolewa maeneo mengi ya msingi ilikuwa haijagusa kabisa bodi, sasa nashukuru mswada mpya umezingatia karibu mahitaji yote ya mwanafunzi ni matumaini yangu kwamba haya hayatabakia kwenye mswada tu au katika sheria, lakini yatazingatiwa kweli katika utelezaji.

Mhe. Naibu Spika, jengine nisema ambalo niliwahi kuliulizia katika masuala hapa kumekuweko na hisia na wanafunzi wengi wanazitaja na wazee wengine na sitokuwemo katika siasa nadhani ni fikira za wananchi wakiwa hawana imani na chombo fulani inaleta matatizo makubwa sana, wakati fulani nakumbuka Mwalimu Nyerere alisema kwamba ikiwa mke wa Julias Kaydhari atatiliwa mashaka basi inatosha kumuondolea sifa za kuwa mke wa spika. Sasa seuze kwa chombo kama hicho kinachosimamia mambo ya msingi ya kutujengea mustakabari wa nchi yetu, kumekuweko na malalamiko mengi ya hisia kwamba kulikuwa na harufu za rushwa katika uliokuwa mfuko wa Elimu ya juu, sasa kama ulikuwepo naomba urekebishwe katika bodi mpya. Kama haukuwepo vyema tunaomba usikuwepo katika hii bodi ambayo inaanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, moja katika mambo yaliyokuwa yakilalamikiwa yalikuwa ni maelekezo yaliyokuwepo na uongozi uliokuwepo unasema kwamba kozi za aina fulani hazimo katika kozi zinazotolewa mikopo, lakini mwengine akipita kwa njia zake anashtukizia anapata. Sasa nasema mimi unaninyima lakini kuna mwenzangu kapata kwa njia zake inaondoa ile dhana nzima ya kuwepo usawa

na mwengine anajihisi labda kuna upendeleo fulani. Kwa hivyo nasema hizo ni hisia ambazo tunapaswa kuzirekebisha vyoe vile ili kuondosha manung'uniko kama hayo.

Moja ya malalamiko ambayo yanatolewa na wanafunzi ni kwamba ulikuwepo katika uongozi uliopita kupeleka idadi kubwa kuliko ule uwezo uliokuwa umewekwa, kwamba uongozi wa idara ulikuwa unaidhinisha tu watu kuliko uwezo wenyewe. Matokezeo hata uongozi mpya wa idara umeridhi idadi kubwa sana kuliko uwezo wake matokeo yake nguvu zinatawanyika haziwezi kukidhi yale malengo yaliyokusudiwa, sasa kama kulikuwa na tatizo hili lilikuwa linafanywa katika hali iliyokuwa sio nia ya serikali naomba uongozi mpya pia ulitizame hili na lirekebishwe yasije yakatokezea yale yaliyotokezea.

Jengine Mhe. Naibu Spika, la jumla vile vile lakini linahusiana na mswada huu katika vyanzo vya mapato, suala la elimu ya Juu ni suala la Muungano ilikuwa ni dhima ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwasomesha Wazanzibar kama inavyowasomesha Watanzania Bara, sasa kupata nafasi katika vyuo vyao ilikuwa ni mashaka, tumeanzisha vyetu kupewa hata hiyo ruzuku kwa vyuo vya elimu ya juu kiasi gani inapelekwa katika Vyuo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambavyo vinatekeleza shughuli ya muungano lakini havisaidiwi chochote, ikaambiwa kwamba hivi ni vyuo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vitagharamiwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe.

Kwa hivyo katika hii mikopo nafikiri tusimamie kama ulivyo kwa mfuko wa muungano nao pia unachangiwa na serikali ya Muungano kwa sababu Elimu ya juu bado ni suala la Muungano.

Mwisho kabisa ni lile suala alilozungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin la kusema kwamba tunasomesha vijana wetu ili wapate kuajiriwa na kulipa hii mikopo, sasa tukiweka utaratibu huo kwamba watu wanastaafu wanaagwa mpaka wanapewa zawadi za vyarahani halafu tunashtukizia wanarudi tena katika utumishi wa serikali hii haileti picha nzuri kwa vijana wetu hata kidogo, kwa sababu inaonekana kama hatuwathamini au hatuwaamini lakini hata hao walioteuliwa hatujaona huo ufanisi wao hapo kabla sasa kigezo gani kinatumika kumpa kazi tena huyu na kumuacha kijana ambae ana uwzo mzuri angeweza kuleta tija katika nchi.

Kwa hivyo hayo nilikuwa nasema Mhe. Naibu Spika, ya jumla sasa nije katika Mswada kwanza nianze na pongezi, kuna vifungu viwili vimenipa moyo kwanza kifungu cha 30 kifungu kidogo cha pili kinachoweka sharti la kwamba mfuko huu hesabu na kumbukumbu zake zizingatie vigezo au masharti yaliyowekwa na Afisi ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali, hilo nasema ni muhimu

kwa sababu itazidi kuweka misingi ya uwajibikaji katika masuala ya nidhamu ya fedha.

Lakini pili nimefurahishwa vile vile na kifungu cha kumi na saba nne na kifungu cha thalathini na moja moja vilivyoweka *link* baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Fedha, kwa kutaka Waziri wa Elimu ashirikiane na Waziri wa Fedha katika masuala ya utungaji wa kanuni zinazoongozwa katika mfuko huu, lakini vile vile katika kuhakikisha utekelezaji bora wa sherehe nasema hili linatia moyo kwa sababu mswada huu unahusu fedha, kwa hivyo tunadhani kwamba itasaidia utekelezaji mzuri wa majukumu haya.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 sehemu ya Kwanza (a) kinachohusu Mwenyekiti nadhani sio utaratibu mzuri wa kisheria kwamba kila siku tunaweka pamoja na kumuamini Rais na kutambua kwamba matakwa yote ya serikali Rais atakuwa anagawa mwenyewe kwa mujibu atakavyoona inafaa, lakini tunapoanzisha vyombo kama hivi tukaweka nafasi kama hizi hasa tunaposimamia masuala ya fedha kama haya, kusema tu kwamba kutakuwa na mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Rais mimi nafikiri haitoshi, tulikuwa tumuwekee Rais vigezo fulani ambavy anapaswa avizingatie na ndio utaratibu wa siku hizi katika serikali, Rais naye ni binadam sio tu ateue yoyote tu, na bila shaka anatengezewa sasa yule anayemtengenezea awe na vigezo ambavyo vinawekwa vya kumpata mwenyekiti wa kusimamia bodi hii ambayo inasimamia masuala ya fedha na masuala mengi ya masomo kwa vijana wetu.

Kwa hivyo hapo nilikuwa naomba hapo kwanza tungewekewa sifa za mtu ambaye anapaswa kuwa mwenyekiti, kuwa na uadilifu, ikiwa mtu ambaye anaheshimika katika jamii na vitu vyengine kama hivi na kutuhakikishia kwamba mtu huyu labda ana uzoefu wa masuala kama haya ya elimu ya juu na kuona anasimamia vizuri dhamana hii.

Lakini jengine limenipa matatizo hili nafikiri ni uandishi wa kisheria tu, kufungu hicho hicho cha (4)c kuanzia nambari za kirumi (i) mpaka nne hapa kidogo napata matatizo Mhe. Naibu Spika, kifungu kinasema.

Kifungu cha (4)c Wajumbe wengine wanane ambao watateuliwa na Waziri kama ifuatavyo, sasa ukianza moja mpaka nne hawa hawateuliwi na Waziri kwa sababu wanaingia kwa nafasi zao, Makatibu Wakuu wa Wizara, Katibu wa Tume ya Mipango sasa mimi nadhani tungetafautisha kidogo, kama mtu anaingia kwa nafasi yake basi huyu hateuliwi na Waziri tutaje kwamba anaingia kwa nafasi yake, kwa sababu sheria hii haimpi tena uhuru Waziri kumteua au kutomteua. Kwa hivyo hili katika utaratibu wa uandishi wa sheria pakawekwa sawa na pakatafautishwa.

Lakini hapo katika kufungu hicho hicho cha nne nilikuwa naomba kupendekeza kwa Mhe. Waziri atukubalie kwamba pale kwenye wawakilishi nane ametajwa mjumbe mmoja atakayewasilisha wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, hawa ndio walengwa hasa Mhe. Naibu Spika, na hii bodi inaonekana imetawaliwa mno na wateule ambao wanaingia kwa nafasi zao za serikalini, mimi napendekeza ingelikuwa angalau wawili wanaowakilisha taasisi za elimu ya juu. Vile vile ningependekeza hawa wapendekezwe na umoja wa wanafunzi wa taasisi na elimu ya vyuo vya juu hapa Zanzibar kwa sababu wanao umoja wao, ili iwe kweli wanawasimamia maslahi yao kwa sababu hawa ndio wenye malalamiko mengi katika utekelezaji wa mfuko katika kipindi hichi ambacho tunakimalizia.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 6(9) kipo ukurasa wa 82 pale kinazungumzia: *(Endapo mjumbe wa bodi atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya sababu maalum bodi itamshauri mteuzi,****(mimi napendekeza baadaye kisomeke mamlaka ya uteuzi lakini nitakuja wakati wa kupitisha kifungu****). Mamlaka ya uteuzi uwa mjumbe huyo juu ya uhalisia wa taarifa za mjumbe huyo na mteuzi anaweza kutengua uteuzi wa mjumbe na kuteua mjumbe mwengine kwenye nafasi yake).*

Hiyo inanipa mashaka jambo moja tu kwamba hapa tuna wajumbe wengi ambao wameingia kwa nafasi zao, sasa je hawa ikiwa wawakilishi wao hawakuhudhuria nao watasita kuwa wajumbe na ikiwa wanateuliwe wengine kwa nafasi zao watateuliwa kutoka wapi wakati wao wameingia kwa nafasi zao. Lakini kama si hivyo je hawa hata wasipohudhuria wao hawapunguki kwa hivyo kifungu hiki cha 6(9) kinanipa mashaka ningeomba pia Waziri akija akatuwekea vizuri hapo.

Kifungu kingine Mhe. Naibu Spika, ni kile ambacho alikigusia Mhe. Rashid Seif hapa kifungu cha kumi na moja, na hichi nacho pia kinatupa mashaka hata mimi kinanipa mashaka, kwamba una bodi halafu una kamati, badala ya kuwa na *secretariat* na hii ukitizama kamati yenyewe ambayo imepewa kazi hasa ya kuchagua hawa wanafunzi, kwa hivyo hapa unakuta sehemu kubwa ni wale wale wajumbe wa bodi wanaingia tena. Makatibu Wakuu wa Wizara zinazotajwa hapa na Mwenyekiti mwenyewe wa bodi na Mkurugenzi, lakini utaona kimsingi wale wawakilishi wengine wa jumuiya zilizokuwa si za kiserikali hapa hawaingii, kwa hivyo pale pahusika hasa wamebakishwa wenyewe kama alivyosema Mhe. Rashid Seif kwamba pengine ingependeza pangekuwa na *secretariat* na mimi nadhani ipo lakini pana matatizo hapo alipogusia Mhe. Rashid Seif.

Kifungu 16 kifungu kidogo cha 4 kilichopo ukurasa wa 84 pale kiliposema Mkurugenzi na Maafisa wengine wa Bodi wataunda kamati tendaji ya bodi, hapa mimi nadhani palikuwa paundwe *secretariat* kwa sababu ukisoma kiingereza hapa pametajwa *management team* hii sio kamati tendaji lakini nafikiri tungeitafsiri kwamba ndio watakaokuwa *team* ya uendeshaji wa bodi. Lakini kama hivyo basi hii ingefanya hii kazi ambayo imetajwa hapa kwamba itafanywa na kamati ndogo, vyenginevyo itakuwa kama alivyosema Mhe. Rashid Seif na wengine kwamba hii kamati itakuwa ipo na itakuwa inafanya kazi zinazopaswa kufanywa na bodi.

Pia naomba ufafanuzi kama kamati inabakia huyu muwakilishi au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ambaye anakingia katika kamati hii jee, huyu ndio yule yule ambaye anaingia katika bodi au ni tofauti, kwa sababu imesema tu ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi mjumbe sasa ni yupi yule aliyetoka na bodi au kutakuwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawili mmojua anaingia katika kamati mwengine katika bodi, hilo pia nilikuwa naomba nipate maelezo.

Mwisho kabisa ni lile ambalo ameligusa Mhe. Salmin Awadh Salmin kifungu cha ishirini kifungu kidogo cha pili kinachosema kwamba. *Kozi ambazo zitatolewa kwa mikopo ni zile ambazo zinaendana na mpango wa taifa wa maendeleo.* Sasa hii kidogo mimi imenipa shida kwa sababu tungelikuwa tuna hicho kitu kinachoitwa mpango wa taifa wa maendeleo ningeikubali, lakini sasa hapa sisi tuna mambo chungu nzima, tuna *vision 2020, tuna MKUZA,* kuna mipango mingi ambayo tunaambiwa yote ni utekelezaji huo huo wa 2020 lakini kama kilichokusudiwa hapa ni *vision 2020* tungeambiwa. Lakini je katika *vision 2020 au MKUZA* kweli Kuna sehemu imetaja kwamba hizi ndio *priority* za elimu katika nchi yetu kwa hizo kozi zitakazoendeshwa hapo. Kama hazikutajwa utaishaia kwamba wao bodi au kama ndio waamue na hapo patapita upendeleo, kwa sababu hapana vigezo wanaweza kutazama namjua fulani kwamba kozi aliyoomba haihusu basi apatiwe. Kwa hivyo na hili naomba tufafanuliwe ili tuweze kuridhika.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mengine ni ya uandishi hayo nitakayokuja kuzungumza wakati wa kupitisha vifungu, lakini na mimi niseme kwamba nitauunga mkono mswada huu pamoja na mazuri yote yaliyokuwemo, pamoja na mapendekezo tuliyoyapendekeza pamaja na ufafanuzi tulioomba kwa Mhe. Waziri ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuweza kutoa mchango wangu mchana huu, mimi ni miongoni mwa wajumbe wakamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na nimpongeze sana Mhe.

Spika, kwa kunichagua mimi kuwa Mjumbe wa Kamati hii pamoja na Mhe. Saleh mjumbe mwenzangu wa Jimbo la Wawi.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi mimi sitaki kutoa mchango zaidi kwa sababu nimekaa nao mswada huu pamoja na wenzangu kwa muda mrefu zaidi, kwanza ninachotaka kusema ni kwamba nimuombe Mhe. Naibu Spika, wajumbe kupitia kwamba au wajumbe wanapotoa marekebisho watoe mapema ili wajumbe waone marekebisho yaliyofanywa, ili ile bidii na kazi ya kamati isiende ovyo kwa sababu ya kujadili mswada, mimi kama mjumbe wa Kamati nina haki ya kulinda kamati yangu kwa sababu tumekaa na tumetumia fedha za umma kutetea mswada huu.

Kwa hivyo ningeomba tu Baraza wanapotoa marekebisho ya miswada wawapatie wajumbe mapema ili wajumbe wapate muda wa kupitia kama ambavyo Mhe. Ismail Jussab Ladhu amepitia na kutoa makosa, amelinganisha mswada na marekebisho ya kamati lakini kuwaachia tu wajumbe bila ya kutoa marekebisho mapema inakuwa wajumbe hawapati ule mchango mzuri. Kwa hivyo kusimama kwangu hapa najaribu kutetea hoja ya kamati ambayo mimi ni mjumbe tena ni Makamo Mwenyekiti, nahofia kuja kuambiwa nimekula fedha bila ya kufanya kazi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hoja ya page 79 ya kuhusu nafasi ya Mkurugenzi kuwa mjumbe wa bodi katika Kamati tumejadili na tumeona kwamba si busara Mkurugenzi kuwa mjumbe wa bodi kwa sababu hawezi kupiga kura, hivyo mkurugenzi awe mkurugenzi kama ilivyo katika sheria nyengine.

Jengine ambalo ningeweka sawa kama ni mjumbe wa Kamati katika ukurasa wa 83 kuanzishwa kwa Kamati ya Bodi, hapo wametajwa wajumbe kwa maana akiwemo na Mwenyekiti wa bodi ninachopenda kuwaambia marekebisho ya kamati ambayo tumepatikwa wajumbe ni kwamba Mwenyekiti wa bodi amefutwa kuwa mjumbe wa kamati, kwa hivyo wajumbe wasipate tabu katika eneo hili, kwamba tumemfuta mwenyekiti wa kamati kwamba sio mjumbe wa kamati ya bodi. Kwa hili kamati imezingatia sana na tumefuta ile hoja.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika ukurasa wa 87 marekebisho ya kamati tumefuka kifungu cha 24. 5,6,7 na kwa hivyo hoja ya wajumbe kwamba wadhamini watapatwa na kazi ya kulipa madeni tumeiona sisi kama kamati na tumefuta vifungu vyote vitatu kwa kuwanusuru wadhamini watakaowadhamini watoto wetu, kwa hivyo mkopaji atalipa mwenyewe baada ya kuajiriwa ndio hoja iliyopo. Tumeona hilo kwa sababu unaweza kumkopesha mtu asiajiriwe baadae mdhamini akapata mashaka akaingia hatiani na kwa mujibu wa sheria akapata adhabu., kwa hivyo vifungu hivyo tumevifuta kwa kulinda hao wazee

wetu wanyonge tumefuta, sasa wajumbe wakija kujadili wazingatie marekebisho hayo ya kamati.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya marekebisho hayo ambayo natetea kamati yangu niseme tu kwamba mswada huu kwa mujibu wa ulivyoandikwa na malengo ya serikali ni kutetea Wazanzibar walio wanyonge, tumeambiwa wazi kwamba lengo la mswada huu ni kufuta ile sheria namba sita ambayo dhahiti ilikuwa ikitoa upendeleo kwa njia moja au nyengine jambo ambalo lilikuwa likiashirika kama kwamba kuna rushwa kwenye mfuko wa mikopo, kumbe hakuna rushwa lakini kuna sheria ambayo haitoshelezi mahitaji ya Wazanzibari. Sasa kuja kwa mswada huu nadhani kutatoa fursa pana zaidi kuwapatia Wazanzibari fursa nzuri za upatikanaji wa mikopo ya fedha kwa ajili ya huduma za elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kama muwakilishi ninachoomba tu katika utungaji wa kanuni za kulingana na sheria hii Mhe. Waziri azingatie dosari ambazo zilikuwepo kwenye mfuko ule wa mikopo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ahsante kama bado una maelezo zaidi nitakupa nafasi jioni muda wetu unakaribia kumalizika na nataka kuzungumza mambo mawili matatu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nafasi ya jioni usinipe naunga mkono hoja, Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nishukuru kwamba kikao chetu kimekwenda vizuri tokea asubuhi mpaka sasa hivi na nawashukuru wale wote waliopata nafasi ya kuchangia, tunategemea mswada wetu huu tuumalize leo jioni na mimi huku sina jina la mchangiaji, kwa hivyo nawaomba wanaotaka kuchangia wote wafike mapema ili wachangie, vyenginevyo nikija hapana wachangiaji namkaribisha Mhe. Naibu Waziri na baadaye Mhe. Waziri tunahitimisha ratiba yetu.

Kwa hivyo nawaomba wajumbe tujitahidi tuje mapema tunaotaka kuchangia ili tuchangie.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuchangia. Mimi naunga mkono kuhusu mkopo ambao umetokeza hivi sasa hivi wa Sheria ya Elimu ya Juu.

Bodi ya Mkopo ya Sheria ya Elimu ya Juu imetoa nafasi kubwa sana kwa wanyonge. Mimi naunga mkono asilimia kwa mia mkopo huu kuweza kukopeshwa wanyonge. Lakini kama itakuwa mkopo huu unaweza kuupata kamili na sio kupata nusu ya mkopo kama unavyotakiwa kutoka.

Majimboni wengi wetu ni wazee wa wanafunzi ni wanyonge kwa hivyo uwezo wa kupewa nusu halafu nusu wakalipia hawana. Ingeliwezekana moja kwa moja mkopo huu wakapewa wote kwa pamoja ili uwawezeshe wanafunzi kusoma kwa wakati. Hilo litasaidia hata sisi Wawakilishi na Wabunge majimboni kuweza kuchangia mambo mengine na sio elimu tena kama ilivyo hivi sasa. Hivi sasa mkopo unaopatikana ni nusu, utakuta wazee wengi wanamalizia kuomba nafasi hizo kwa Wawakilishi na Wabunge ili vijana wao kuweza kusoma.

Mimi naunga mkono mkopo huu upitishwe ili tupate kusomesha vijana kwa wakati ili tuweze kupata vijana bora katika sehemu zetu za kazi. Na kwa vile vijana hao hujitoa muhanga kwenda kusoma kwa muda mrefu ni vyema wanapomaliza kusoma zipatikane ajira za kuweza kuwasaidia kuweza kulipa madeni yao ambayo yanahitajika kulipwa kwa muda mfupi.

Si vizuri mwananchi ameweza kusoma kwa muda wa miaka zaidi ya 20 akimaliza hana ajira na hapo hapo anahitajika kulipa mikopo ambayo ameikopa. Je, mwananchi huyu atapata wapi mkopo huo wa kulipia wakati ajira hakupata tangu mwanzo. Hivi sasa utakuta vijana wetu wanajitoa muhanga sana kwenda kusoma na wanasoma kwa bidii zote, lakini utakuta baada ya masomo kijana huyo unamkuta yupo jimboni anakuja kwa Mwakilishi au Mbunge kukuomba, hana kazi ya kufanya.

Naiomba serikali izingatie sana vijana wetu wanapotoka masomo ziwepo ajira za kuwasaidia angalau kufuta machozi kwa kuweza kupata ajira ingawa za viwanda au mahotelini. Leo utatembelea katika mahoteli ya Zanzibar ambayo ni kiinua mgongo cha maendeleo ya Zanzibar lakini huwezi kumkuta kijana wa Kizanzibari yule ambaye amesoma elimu ya juu yupo nafasi nzuri, ukenda nafasi ile utawakuta wengi wao ni wageni tena nje ya Tanzania. Mzanzibari

yule akenda anaambiwa nafasi hakuna na pengine yule aliyekuja sio msomi kuliko Mzanzibari huyo na huku amepewa mkopo na serikali kwenda kusoma. Lakini hautumii mkopo wake na kisomo chake kupata nafasi ya kazi. Nafasi hizo ukenda kwenye viwanda utazikuta zimo, katika watu 100 utamkuta Mzanzibari 1 na amesharudi Chuo Kikuu kwenda kuchukua ya kuweza kufanikisha sehemu ile.

Mhe. Naibu Spika, ni bora serikali ichukue nafasi ya kujali sana wananchi wa Zanzibari ambao wanachukua mikopo kwenda nje kusoma au kusoma katika vyuo vikuu vyetu, ili wakirudi wapangiwe mawazo mazuri na maarifa ya kuweza kujielimisha katika sehemu za kazi. Mimi nachangia kwa nafasi hii ya mkopo upite kwa asilimia mia, zaidi uzingatie kwamba wananchi wengi ni wanyonge wasipewe pesa hizo kwa nusu na kwa kulipa kwa muda mdogo, ili wapate nafasi ya kusomesha vijana wao, angalau kwa muda wa mwaka mzima au baada ya kurudi masomoni. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naahirisha Baraza mpaka umeme utakaporejea.

(Saa 11:05 Baraza liliahirishwa mpaka umeme utaporejea)

(Saa 11:10 Baraza lilirudia)

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuchangia elimu ya juu tunaendelea na masuala yetu kwamba hivi sasa vijana wengi wanajitoa muhanga kwenye masomo kwa mategemeo akimaliza masomo na kupatiwa mikopo ambayo amepewa. Anaelewa wazi kwamba taifa lake litamjali na ataweza kupata angalau kifuta machozi cha kupata ajira katika nchi yake. Lakini utakuta teknolojia ambayo tunaendelea nayo sasa ni ngumu na ambayo haiendi na wakati. Utakuta vijana wengi tunao wasomi lakini utakuta bado anaendelea mtu ambaye ameshamaliza umri wa kustaafu anaendelea miaka mitano mengine, anapewa tena miaka mitano mengine, bado utakuta wanafunzi ambao wamekwenda elimu ya juu wapo wengi katika mitaa na majimboni kwetu. Hiyo inakuwa ni mzigo mkubwa kwa sisi viongozi ambao tupo katika majimbo.

Naishauri serikali hili suala la kuongezwa miaka kwa hivi sasa liachiliwe mbali na lifutwe kabisa kwa watu ambao wameshapitwa na wakati. Hivyo tuzingatie mtu wa kumchangia kwamba tunamuhitaji labda yule ana teknolojia ya kuunda jambo ambalo sisi Zanzibar tunaliita na hasa kama litapitishwa ni bora mtu huyo tunaemuhitaji liletwe katika Baraza la Wawakilishi tumjadili ana umuhimu gani kwa taifa. Sio tu kumjali mtu kwamba katika Wizara ana umaarufu wa jina au ni rafiki wa kiongozi kuweza kuendelea miaka hadi

miaka. Wananchi tunawadhalilisha kuweza kutumia nafasi yao ya masomo ambayo wameyasoma na mikopo ambayo wamechukua na kulipa kwake ni kugumu. Hilo nachangia na naunga mkono suala la elimu ya juu kwa mkopo wake.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kusema machache katika Mswada huu ambao ninavyoona miye ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nyenzo moja muhimu sana ya maendeleo ya nchi ni elimu. Lazima tukiri Wazanzibari hali yetu ni mbaya sana kielimu. Hivi karibuni nilipokuwa katika kazi za Kamati tulitembelea Wizara ya Elimu. Moja katika masuala yaliyojitokeza kuwa na changamoto kubwa ni ukosefu wa fedha za kusomeshea vijana katika elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa nakumbuka alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, alitwambia makisio yao kwa mujibu wa wanafunzi ambao wapo kwenye masomo hivi sasa ya kuwasomesha kwa mwaka karibu shilingi bilioni 4. Walipopeleka Wizara ya Fedha wakaletewa *ceiling* kwamba walazimike kutumia bilioni 2. Wanafunzi wapo masomoni, nusu mwaka umemaliza bilioni mbili zimekwisha, ili wamalize mwaka wao wanahitaji bilioni 2 za ziada, pesa hapana. Sasa tunajiuliza je, warudi? Na wakirudi zile bilioni mbili za kwanza si zishapotea. Kwa kweli hii ni changamoto kubwa.

Mimi nafikiri lazima tutafute namna ya kuhakikisha kama vijana wetu wanaendelea kupata elimu hasa ya juu. Kama nilivyotangulia kusema kwamba elimu ya juu ni nyenzo moja muhimu sana ya maendeleo ya nchi. Tunahitaji kuendelea kwa hivyo ni lazima tupate vijana walioelimika vya kutosha.

Mimi binafsi naunga mkono sana kwamba hii ni njia moja ya kuelekea huko. Ila sikufurahishwa na madhumuni na sababu ya kuletwa Mswada huu hapa Barazani. Sikufurahishwa nao sio kwa sababu kwamba Mswada ni mbaya. Hapana, Mswada ni mzuri ila Mhe. Naibu Spika, madhumuni na sababu hayatoshi. Sentensi iliyoelezwa pale ni ndogo sana ambayo haikidhi haja naomba niisome.

Madhumuni na Sababu:

> **"**Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6 ya 2001 na kuweka Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo".

Hiyo ndiyo sababu ya kubadilisha ile sheria na kuweka sheria hii ya mfuko wa Mikopo. Mimi nilikuwa nadhani wameleta Mswada huu kwa sababu sheria ya kwanza ina mapungufu. Kama ni hivyo basi wangelitueleza katika haya madhumuni na sababu, lakini hakuna kilichoelezwa.

Nilikuwa naomba sana mawaziri wanapoleta Miswada yao kwenye kifungu hiki cha Madhumuni na Sababu basi wajaribu kueleza kidogo angalau mtu apate muelekeo hasa kilichokusudiwa ni kitu gani.

Kuna Miswada mengine nimeiona hata humu tutaijadili nafikiri kesho na keshokutwa, imejaribu kufafanua kidogo lakini Mswada huu haukufafanua hata kidogo. Hilo moja nilikuwa naomba tujitahidi kufafanua kidogo katika kifungu hiki cha madhumuni na sababu.

Nianze na kifungu cha 5 (a) Kazi za Bodi, naomba nikinukuu kidogo.

Kifungu cha 5(a) Kazi za Bodi zitakuwa:

(a) Kutoa mikopo kutoka kwenye mfuko kama ambavyo Bodi itaona inafaa, kwa mtu yeyote mwenye sifa ili kuwezesha kusaidia mwanafunzi yeyote kulipia gharama za elimu ya juu;"

Hiki kifungu katika uandishi wa sheria Mhe. Naibu Spika, naona kama kinajizonga zonga, kwa sababu mlengwa hapa ni mwanafunzi. Ilikuwa hapa isemwe tu ni kutoa mkopo kutoka kwenye mfuko kama ambavyo bodi itaona, kwa mwanafunzi yeyote kulipia gharama za elimu, lakini kwa mtu yeyote mwenye sifa ili kuweza…

Kwani huu mfuko unakusudia mtu au unakusudia mwanafunzi? Sasa kama unakusudia mwanafunzi nilikuwa nahisi hii *phrase* ya kusema kwa mtu yeyote mwenye sifa. Mimi nadhani tungesema mwanafunzi tu moja kwa moja, tukiacha mwanya huu maana yake mtu yeyote sasa asiyekuwa mwanafunzi atakuja kopa huku. Nilikuwa naomba tufanye marekebisho kidogo hapo.

Nikitoka hapo niende kifungu cha 6(7) pale ni vikao na maamuzi ya bodi.

Kifungu cha 6(7)

"Katibu atahifadhi na kuweka kumbukumbu na mwenendo wa vikao vyote na kumbukumbu ya kila kikao zitathibitishwa na Bodi kwenye kikao kinachofuata …"

Huyu Katibu tulipokuwa tukiangalia wajumbe wanaounda hiyo bodi yenyewe Katibu hajatajwa. Sasa nilikuwa najiuliza ni mtu gani hapa anaechukua nafasi ya Katibu ni Mkurugenzi au nani. Na kama mkurugenzi basi angeelezwa kwamba mkurugenzi ndiye ambaye atakuwa Katibu ya hiyo bodi, sasa hakutajwa hapa. Nadhani ilikuwa ni muhimu nae basi atajwe kwamba kutakuwa na Katibu wa Bodi na kama ana wadhifa mwengine humu basi afafanuliwe vizuri.

Kifungu cha 6(8)

> "Uhalali wa tendo lolote au mwenendo wowote wa Bodi hautoathirika kwa kuwepo nafasi ya wazi ya mjumbe au kwa kushindwa kuteuliwa kwa mjumbe yeyote miongoni mwao."

Yaani maamuzi ya bodi yataendelea kuwa halali hata kama kuna nafasi ipo wazi ya mjumbe pale, hata kama hajateuliwa. Nilikuwa nahisi kifungu hiki tumekiwacha wazi sana kinaweza kikaleta athari. Kwa sababu kuna wajumbe wengine katika bodi ni muhimu sana kwa mfano. Kuna mjumbe mmoja atakaewakilisha wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu. Sasa kama huyu hayupo halafu bodi ikakaa kwenye mashauri yake na ikaleta maamuzi, maamuzi yale yanaweza kuja kuleta *contradiction* baadaye baina ya bodi na wale wanafunzi wanaosomeshwa. Sasa nilikuwa nahisi labda tungetafuta namna japokuwa mantiki ibakie lakini isiwe kama hivi ilivyo. Tufanye marekebisho kidogo kwa sababu wajumbe wengine ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, Kifungu cha 7(3)(c) pale pana mambo ambayo yakitokea mjumbe atasita kuwa mjumbe wa bodi. Kifungu hicho kinasema:-

Kifungu cha 7(3) "Mjumbe atasita kuwa mjumbe endapo itatokea lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) atafariki,
(b) atashindwa kuhudhurua mikutano mitatu mfululizo bila ya kuwepo sababu ya msingi,
(c) atatiwa hatiani kwa kosa la jinai,"

Hii kidogo nina mashaka nayo. Sheria nyingi zinaeleza kuwa mtu atatiwa hatiani kwa kosa la jinai lakini katika kiwango gani. Kwa mfano nafikiri katika Katiba au Sheria ya Uchaguzi imeandika kama mtu hatafaa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa atatiwa hatiani na Mahakama na atapewa adhabu itakayozidi miezi 6 kitu kama hichi nakumbuka.

Sasa naona ilikuwa ni muhimu sana kuiainisha adhabu katika kiwango gani. Maana siku nyengine mtu anaweza akatiwa hatiani kwa kosa la jinai lakini akapigwa faini shilingi elfu kumi. Sasa ukim-*disqualify* kuwa hafai tena kuwa mjumbe wa bodi kwa sababu ya Shilingi elfu kumi mimi nadhani haileti sura nzuri. Kwa hivyo hapa pangeainishwa lile kosa na kiwango cha kosa lilivyo.

Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu cha 14(3) imeandikwa akidi ya Mkutano wa Kamati. Sasa hatupo kwenye bodi tupo katika Kamati ya Elimu hii.

Kifungu cha 14(3) "Akidi ya Mkutano wa Kamati itakuwa robo tatu ya Wajumbe"

Mhe. Naibu Spika, wajumbe hawa wa Kamati ya elimu ni 6 sasa labda iwe kuna *righting mistake* lakini robo tatu ya wajumbe ni wajumbe 4 na nusu. Na mimi sidhani kama kuna nusu mtu, nilikuwa nafikiri hapa waandishi wamepitikiwa kidogo hapa. Kuna haja ya kukifanyia marekebisho, kitakuwa kinachekesha chekesha kidogo hichi kifungu. Labda wamekusudia thuluthi mbili, kama ni thuluthi mbili basi sawa. Lakini robo tatu itakuwa ni watu 4 na nusu ambalo si jambo rahisi kupata watu 4 na nusu au labda Mhe. Mansour atwambie kama kuna nusu mtu duniani.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye kifungu cha 17 kunaanzishwa huo mfuko wenyewe sasa. Kifungu kidogo cha tatu kinasema fedha za mfuko zilizohifadhiwa zitatumiwa kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi ambao wanatarajia kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Hizo fedha za huo mfuko kazi yake itakuwa ni hiyo tu kutoa mikopo kwa wanafunzi waliopata nafasi ya kuendelea katika elimu ya juu.

Lakini tukumbuke kuna vyombo ambavyo vinaendesha huo mfuko moja ikiwa ni hiyo bodi ya elimu ya juu, lakini pia kuna Kamati ya Elimu. Sasa hawa watakaa, watakuwa na Vikao, kutakuwa na ufatiliaji, watafutaji uendeshaji. Lakini hivi fedha zote kwa mujibu wa kifungu hiki hazitatumika vyenginevyo isipokuwa kwa kutoa mikopo tu. Sasa hawa vikao vyao wakikaa huwa hawalipwi. Nafikiri pengelikuwa na marekebisho madogo hapa napo.

Mhe. Naibu Spika, labda sasa niende sehemu ya nne ambapo kuna masharti ya mkopo wa wanafunzi. Kifungu cha 19 kifungu kidogo cha 2 hapa wametaja mambo ambayo hizo fedha za wanafunzi akishakopeshwa mwanafunzi basi kapangiwa matumizi ya kutumia. Kwanza ni ada ya masomo, gharama za mitihani, gharama za chakula na malazi, vitabu, usafiri, utafiti na nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, mara moja niliwahi kufanya udadisi juu ya wanafunzi hawa wanaopata mikopo, ni kwamba jambo la kusikitisha sana kuna wengine kwa kweli wanakabiliwa na hali ngumu sana wakiwa masomoni. Mhe. Naibu Spika, posho la chakula mtumzima aliyetimia asiyepungua kilo mia na zaidi anapewa shilingi 2000 za kushindia mchana wa kutwa mpaka usiku. Mimi nafikiri haya ndio yale mapungufu niliyosema yamo, mambo kama haya lazima yazingatiwe.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni wanafunzi wa Chuo Kikuu waliandamana kwa sababu walikuwa wanagaiwa shilingi 5000 haiwatoshi, lakini Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa yako kuna wanafunzi wanashindia shilingi 2000. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri jambo hili hadi uliangalie sana kwani ni hatari mno utakuja kuuwa tena pengine mwanafunzi huyo yuko ugenini. Kwa hivyo, kama hawezi kujikimu kwa fedha atakazogaiwa maana yake ni kwamba afe. Hivyo nilikuwa naomba sana nitakapoweka kanuni hizi shilingi 2000 kwa kweli ziongezwe mara tatu zaidi kwani hazitoshi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 19 kifungu kidogo cha 5 naomba nikinukuu kidogo.

> *"Endapo Bodi itakuwa imeweka kiwango maalum kwa mujibu wa kijifungu cha (3) cha kifungu hiki, ambacho kila mwanafunzi, mzazi, mlezi au mtu mwengine anaehusika italazimika amchangie muhusika kiwango hicho cha fedha ambacho kimewekwa na Bodi".*

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nasoma Kiswahili na kwa taarifa yako nilipasi 'A' *level* ni kwamba hii sentesi haijakamilika kwa Kiswahili tunaita tungo tegemezi, ni sentensi ambayo inahitaji jawabu au vyenginevyo ibadilishwe hapa kati kati. Mhe. Naibu Spika, endapo Bodi itakuwa imeweka kiwango maalum kwa mujibu wa kijifungu cha 3 cha kifungu hiki, nilikuwa nashauri sana hili neno "ambacho" lifutwe na badala yake liwekwe "basi" kila mwanafunzi, mzazi, mlezi au mtu mwengine anayehusika itamlazimu amchangie muhusika kiwango hiki cha fedha ambacho kimewekwa na Bodi.

Mhe. Naibu Spika, ugomvi wangu liondoke neno ambacho pawekwe neno basi hii sentensi itakuwa imekamilika. Maana yake hiyo itakuwa ndio jawabu ya ile utegemezi wenyewe lakini kama si hivyo ikibakia kama ilivyo itakuwa hii sentensi yote nzima haikukamilika na mtu akiisoma anasubiri kuwe na jawabu ya kukamilisha hapa. Mhe. Naibu Spika, nafikiri waliosoma Kiswahili akina Mdungi watakubaliana na mimi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kifungu cha 24 kifungu kidogo cha 3 naomba nikinukuu.

"Mkopaji yeyote aliyeajiriwa na serikali au mashirika yake kwa muda usiopungua mikaa mitano atalazimika kulipa nusu ya mkopo wake na nusu iliyobaki italipwa kwa muda utakaoamuliwa na Bodi".

Mhe. Naibu Spika, hii mimi sikuifahamu hata kidogo yaani pana nusu mbili hapa. Kuna nusu moja atalazimika kulipa nusu ya mkopo wake yaani huyo mtu aliyekopeshwa kama ni muajiriwa wa serikali au mashirika ya serikali basi akishakopeshwa nafikiri nusu moja atalipa mwenyewe na nusu iliyobaki italipwa kwa muda atakaoamuliwa na Bodi, nafikiri itakuwa hivyo., Lakini tatizo langu je, hii nusu ambayo atailipa yeye atatakiwa ailipe mara moja haina muda hii. Mhe. Naibu Spika, hii sentensi kidogo ilikuwa inahitaji maneno mengine zaidi kuifafanua. Nafikiri Mhe. Naibu Spika, kuna vifungu vyengine vimefutwa hapa na kamati nafikiri si tatizo baada ya kusema hayo labda niseme tu kwa umuhimu wa mswada huu na mimi naunga mkono mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi AR na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu kuchangia kidogo mswada huu wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa wote wa Jimbo la Dimani naunga mkono sana mswada huu na naomba waheshimiwa tuupitishe kwa asilimia mia juu ya mia. Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikasema hivyo? Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sote tunafahamu matatizo tuliyokuwa tunayapata katika kusoma hasa elimu ya juu huko siku za nyuma, kwa kweli vijana walikuwa na uwezo, sifa zote wanazo lakini vyuo ni vigumu. Ni kwamba nafasi zipo lakini kujigharamia mpaka serikali yetu ikaja kurekebisha mambo wengi ndio tukapenya na nakumbuka Mhe. Juma bahati nzuri, nakumbuka mimi Maalim Seif Sharif Hamadi alinisomesha *Geograph* Lumumba *Form III* na *IV*. Aliponisomesha ilikuwa ametoka *Fidel Castro* palikuwa na upungufu wa walimu pale akatolewa Fidel Castro akaja akatufundisha pale. Mhe. Naibu Spika, basi ikawa tunamtania tunamuuliza hiyo ilikuwa ni mwaka 1968 anasema kamaliza tokea 1963 *Form VI* lakini alikuwa ana mark time tu anaambiwa utakwenda kesho, utakwenda kesho kutwa, ni kwamba hakwenda mpaka Mapinduzi imekuja akenda na kina Mhe. Juma Duni mwaka 1972.

Mhe. Naibu Spika, hii inaonesha ugumu wa zile *sponsorship* tunazozungumza ni kwamba nafasi zipo lakini nani akugharamie ukasome hapo ndio penye mtihani. Kwa hivyo, leo tunafurahi sana kwamba serikali yetu imeweka mkakati na vijana sasa watapatiwa fursa tena fursa sawa kwa wote, wewe upeo wako na sifa zako. Mhe. Naibu Spika, nimefurahi sana kwenye sehemu ya tatu kifungu cha 18 kuhusu malengo ya mkopo, panasema malengo ya mkopo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaotarajia kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Juma Abdalla alisema kwamba ingeandikwa kule madhumuni na sababu lakini baada ya kupekura humu ndani nimeyaona. Kwa hivyo, naweza kusema hii inafaa labda ni uandishi tu.

Kwa hivyo, mimi naunga mkono sana mswada huu na hasa hizo sababu alizoelezea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama wanavyosema kwamba na waheshimiwa wengi wamezungumza, wananchi wetu hali zao sio nzuri, na mafunzo ya elimu ya juu ni ghali. Kwa hivyo, kuwekwa kwa mfuko huu naamini kutasaidia sana kuwapa elimu ya juu wanafunzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mswada umeandikika vizuri na ukitizama kwenye sehemu ya 4 unazungumzia masharti ya mikopo ya wanafunzi. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki ni kizuri sana kwa sababu hao wanafunzi wenyewe nao wafahamu kabla hawajakopa wanawajibika nini, wanatakiwa wawe na sifa gani, hii itapunguza sana mizozo inayotokezea kwani maombi ni mengi, mwengine anasema anapendelewa huyu, mwengine anasema anapendelewa yule. Lakini hajui kwamba yale masharti na sifa zilizowekwa ziko kwenye kifungu cha 20, sifa za kupata mikopo. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hizi sifa ukizizingatia basi utaona kwamba mimi bora mwenyewe nisiombe kwa sababu sina sifa. Lakini tunatoa fursa nyingi kwa akina mama kwa sababu tunataka na wao wajisogeze.

Mhe. Naibu Spika, hii kueleza kwa uwazi kabisa sifa za kupata mikopo na watu wetu wakazifahamu ni suala la msingi kabisa. Naifikiri hii itazidi kutoa changamoto kwa vijana kwamba mtu ajue mimi kupata mkopo natakiwa niwe na sifa kadha na kadha. Mhe. Naibu Spika, hili suala ni muhimu sana na ningeomba sana wizara baada ya mswada huu kupita basi kidogo maelezo haya yafahamishwe kwa wale wanaotaka mikopo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika sehemu ya 4 imeelezea kwamba msaada wa fedha utakaotolewa chini ya kifungu cha 1 utasaidia yako mambo mawili kwanza ni ada ya masomo, gharama za mitihani, gharama za chakula na malazi, vitabu vya kusomea na kuandikia, gharama za usafiri, gharama za utafiti, gharama za kazi za vitendo, gharama maalum za kitengo na bima ya afya.

Mhe. Naibu Spika, kama wanafunzi wachache ni imani yangu kwamba hizi gharama zote serikali na wizara ingeweza ikazihudumia mia juu ya mia. Lakini matatizo ni kwamba wanafunzi wanaoomba ni wengi na kuwaacha sio vizuri kwa hiyo tumesema basi “haba na haba hujaza kibaba”. Hivyo sisi serikali tutoe kidogo na wazee nao wachukue jukumu au wafadhili wengine wasaidie. Kwa hivyo, nafikiri ni suala la msingi bora wakapata kidogo na naamini

hawatokufa na njaa wala hawatotaabika. Najua unaposoma lazima ujipinde kidogo kesho kutwa utakuwa ofisa.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumtolea mfano rafiki yangu Maalim Juma kwa sababu tumesoma pamoja yale mabanda ya Rahaleo pale zamani yalivyokuwa ndio tulikuwa tunakwenda pale tunajipinda mtu anakwenda kusali anatafuta muhogo anarudi pale mpaka saa kumi na mbili. Mhe. Juma alikuwa *partner* wake Mhe. Mzale basi pale wenyewe wanajipinda wenyewe mabanda yale hatuyasahau maisha yale, tena nafikiri yapo mpaka leo hayajavunjwa. Kwa hivyo, lazima tuwaelimishe vijana wetu unapotafuta cha mvunguni lazima ujipinde uiname ndio utafanikiwa ukiwa unasoma huku na mastarehe basi hivyo haviendi sambamba. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana wizara kwamba wamejitahidi kusema kwamba msaada wa fedha hizo utachangia mambo hayo yaliyotajwa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye sehemu ya nne anazungumzia katika kifungu cha 7 mkopaji yeyote ambaye kwa kipindi cha chini ya miaka miwili atakuwa hakuajiriwa wadhamini wake watalipa deni. Hii Mhe. Naibu Spika, naomba kusisitiza tu kwamba kila mkopaji afahamu kwamba mfuko huu unazunguka, hivyo unatakiwa ulipe kwa mujibu wa wakati uliowekwa ili wenzako na wao wafaidike. Lakini ukishakopa wewe halafu ukasahau ujue unawanyima fursa hii wengine. Kwa hivyo, hili ni suala la msingi kabisa na mimi nasisitiza sana kwamba lisimamiwe vizuri, kweli wengi wakishafaidika na mkopo, wameshaajiriwa wanasahau tena kulipa hivyo tunawakosesha fursa wengine wale ambao wangepata mkopo huo.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tano inazungumzia masharti ya fedha na mapato ya Bodi vyanzo vyake. Mimi nimefurahi sana vyanzo viko mpaka (a-g) na vyanzo mbali mbali, lakini naona kidogo tungeongeza kuna wafadhili wengine wanaojitolea tu naona hawakuorodheshwa. Wengine tunao hapa Zanzibar na wengine wako nchi za nje, kuna vyuo vikuu vyengine wanaweka asilimia maalum wanasema fungu hili zitumike kwa kuwahudumia wanafunzi wa Chuo Kikuu. Kwa hivyo, ningeomba hawa nao waorodheshwe.

Vile vile ningeiomba sana wizara ijaribu sana kutafuta watu kama hawa kwani elimu haina mwenyewe kila mtu ni mwenyewe na tusaidiane. Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano kidogo katika Vyuo Vikuu mbali mbali vya nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wanatoa fungu maalum la utafiti, wanasema mimi kwa atakayefanya utafiti wa aina fulani basi naweka asilimia moja mapato yangu watumie. Huwa wanasaidia sana ndio utafiti unakwenda na wanajua matokeo yale ya utafiti yatasaidia sana jamii katika kuendeleza maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nashauri sana kwamba

tuwatafute watu kama hawa kwani wana fungu lao hapa duniani na hata huko mbele.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho uko sehemu ya sita kuhusu masharti mengineyo kwenye kifungu cha 31 (1) naomba kunukuu.

> *"Waziri anaweza kwa kushauriana na Waziri wa Fedha kutunga kanuni au kutoa miongozo ambayo ataona umuhimku na inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hii kwa usalama na kwa faida ya Bodi".*

Mhe. Spika, hiki ni kifungu muhimu sana na kwa kweli matatizo mengi sana haya madogo madogo yanayotokezea na kuletea hata wanafunzi wetu kugoma naamini kwa *flexibility* iliyowekwa hapa kwamba Mhe. Waziri kwa kushauriana na Waziri wa Fedha wanaweza wakarekebisha mambo. Hii ni *point* nzuri sana Mhe. Naibu Spika, maana yake tunangoja tena mpaka wakati mwengine migomo inakuwa mikubwa, wanafunzi wanalalamika mpaka aingie Waziri Mkuu tena ndio mambo yanakwamuka, tunashukuru hapa petu hayajatokezea. Mhe. Naibu Spika, lakini sasa hapa imeshawekwa *proposition* kwamba waziri kwa kushauriana na Waziri wa Fedha wanaweza kutunga kanuni na kutoa miongozo ambayo wataona ina umuhimu na ina faa juu ya utekelezaji. Hili ni suala zuri sana na mimi nampongeza waziri na serikali kwa ujumla kwa kuliona suala hili naamini utekelezaji wake utatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema sina mengi nasema tutie chumvi kidogo hapa na pale na naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana mimi nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika mswada huu wa leo ambao ni Mswada wa Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6 na kuweka sheria mpya ya Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu na mambo mengineyo.

Kwa hakika mimi ninachokiona kikubwa kwanza naweza kusema kwamba naishukuru Wizara ya Elimu kwa kuleta mswada huu, ni mswada ambao ni muhimu sana kwa anayeweza kufikia katika malengo ya serikali nini serikali inataka kwa wananchi wake. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia si mswada huu tu wakutoa nafasi kwa wanafunzi kupewa mikopo, lakini tuangalie jinsi gani serikali iko makini hata katika mambo ya mrajisi wetu wa shughuli za serikali ambao kuweza kutoa nafasi watu kukopa fedha kwa vitu ambavyo vinaweza kuhamishika. Mhe. Naibu Spika, hilo ni jambo muhimu kwa serikali.

Kwa hivyo, ukiangalia upande wa pili wa serikali utaona kwamba serikali kwa kuwapenda wananchi bado inaendelea kuangalia kwamba pia tuwatafutie mabenki ya kuweza kukopa. Hii ina maana ni kusema kwamba serikali inaona namna gani inawasaidia wananchi. Kwa hivyo, tukiingia katika mswada huu ni kwamba mswada huu unatoa nafasi kwa nani? Inatoa nafasi kwa wanafunzi. Wanafunzi wepi? Wanafunzi wa nchi hii wetu sisi wenyewe ni watoto wetu pamoja na wafanyakazi wengine katika kujiendeleza na kupata elimu.

Kwa hivyo, inaona ni jambo jema, ni jambo zuri kuwasaidia watu wetu kwa sababu imeshaonekana kwamba hali za watu wetu sio nzuri, haziridhishi kwa hivyo serikali inajikita kuona kwamba hao wanaotaka kujiendeleza na elimu ya juu ambayo ndio elimu inayotafutwa hiyo elimu ya juu. Kwa hivyo, ni kwamba wapewe wasikoseshwe nafasi kutokana na kuwa hawana uwezo wa kuweza kuutoa, lakini wapewe nafasi ya kukopa ili waweze kurudisha na kufanikisha malengo yao ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kuanzia kwenye mswada huu nimeona kuna sehemu ambazo ninahitaji kidogo nipate maelekezo. Mhe. Naibu Spika, katika kazi za Bodi ambayo Bodi ndio itakayokuwa dhamana. Mimi nasema hii Bodi au kuanzishwa kwa mfuko huu wa mkopo wa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Vyuo Vikuu au vyuo vyote vya elimu ni jambo zuri na ni jambo la busara, lakini kuna mambo katika Bodi hii ambayo yanahitaji kidogo kuletewa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kutafuta fedha na aina nyengine za misaada katika kazi za Bodi wanatakiwa wafanye hivyo, watafute misaada ya kuendeleza kazi za Bodi. Mimi hapa kwa *point* hii ya *(f na g)* kupokea zawadi, mchango, mikopo na vitu vya thamani vinavyotolewa kwa Bodi. Hapa kidogo katika maelezo hayana msimamo mzuri katika Bodi hii. Kwa nini isiwe na fungu lake maalum la fedha likajuulikana, hapa pana kitu ambacho kinaning'inia yaani hii Bodi japo ndio iliyopewa dhamana lakini mimi nilitegemea kwamba kutakuwa na mfuko maalum ambao wanapewa katika Wizara ya Elimu ili kunyanyua mambo haya. Lakini hapa inavyoonesha wakutegemea zawadi, wakutegemea misaada, wakutegemea mambo mbali mbali ili mfuko huu uweze kwenda vizuri. Kwa hivyo, ikiwa yote haya hayakupatikana maana yake nini? Kwa hivyo, ningelipendelea hapa hivi vifungu viwili vya mwisho vinavyozungumzia mambo haya viweze kuangaliwa kwa makini zaidi kwamba hapa tusitegemee Bodi kutafuta fedha hii kwa ajili ya kuwakopesha watu, lakini pawe na mfuko maalum.

Mhe. Naibu Spika, halafu kitu chengine ambacho nilichokiona mimi kuna sehemu ambayo wenzangu waliwahi kuzungumzia vile vile katika suala zima la Kamati ya Elimu na mimi nasema katika Kamati hii ya Elimu inahitaji

kuangaliwa kwa makini na inaonesha kwamba katika kamati hii haina kamati maalum inayozingatia mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia tena mbele utakuta kwamba kuanzishwa kwa huo mfuko fedha za mfuko zilizohifadhiwa zitatumiwa kwa kutoa mkopo wa wanafunzi ambao wanatarajia kuingia katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Waziri kwa kuzingatia utendaji bora wa mfuko kwa mujibu wa sheria atashauriana na waziri. Mimi hapa kidogo pananiletea mashaka hiyo fedha haijapatikana waziri hajashirikishwa, waziri hana mfuko aloipa Bodi au Wizara ya Elimu, lakini hapa atashauriana hivyo atashauriana kwa jambo gani. Hilo tunataka tulijue hapa waziri atashauriana na Bodi hii kwa jambo gani.

Mhe. Naibu Spika, katika jambo jengine ambalo nililoliona ni suala la ukurasa wa 86 unaosema Bodi itakapokuwa inatoa mkopo kwa mwanafunzi yeyote italazimisha kuwepo kwa mdhamini wa kudhamini mkopo wowote utakaotolewa kwa mwanafunzi, endapo mwanafunzi atashindwa kurudishwa mkopo na mdhamini yeyote atalazimika kulipa na kurejesha mkopo wote aliyopewa mwanafunzi pamoja na riba. Hapa baada ya mkopo kuna na *interest* yanini tena hii *interest*? Hivyo hilo lengo hasa mpaka tufikishane kwenye riba? Mimi naona hapa Mhe. Waziri hili suala la riba tuliondoe halina haja. Mwanafunzi ameshindwa kulipa basi aitwe kwa utaratibu mzuri kwa fedha ile ile aliyokopa arudishe fedha ile ile, hatuko benki hapa kwamba lazima tuwe na riba.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 25(3) kunasema kwamba:

> *"Mkopaji yeyote bila ya sababu za msingi atashindwa kulipa deni atafunguliwa kesi ya madai".*

Mengine hayo mapya, tunafanya nini? Afunguliwe kesi ya madai ndio tunasaidiana au tunamalizana. Mimi nasema hapa asifunguliwe kesi, kweli yeye mkopaji kakopa na 'kukopa harusi kulipa matanga', ndio inavyosemwa. Lakini mkopaji huyu bila ya sababu za msingi naseama sababu atakuwa nazo kwa sababu huyu ni mwanafunzi, tujaalie wote ni wanafunzi na mwanafunzi akishafanya kosa basi haendi kwenye taratibu, atakaa kwao au pengine ameshindwa katika mtihani au haelewi masomo yaliyoko pale anaweza akakaa kwako bila ya kwenda pale.

Sasa mimi natoa ushauri mwengine, huyu mkopaji ambaye atashindwa kulipa deni asifunguliwe kesi kwanza, nashauri kwamba huyu mtoto au yeyote ikiwa ni mfanyakazi wa serikali aitwe, lakini kesi asiwenayo. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo kwa ufupi tu ya kuchangia, ahsante sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi hii kuweza kuchangia angalau kidogo. Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 3(1) kinakusudia kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Bodi hii ambayo inakusudiwa kuanzishwa na mswada huu bilashaka ni chombo ambacho kinakusudiwa kuwa chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuhusu kazi za bodi hii kwa kweli Mhe. Naibu Spika, zimefanana sana na zile kazi za Bodi ya Mikopo ya Bodi ya Tanzania.

Mashaka yangu yapo kwenye uanzishwaji wa chombo hiki ambacho ni chombo cha pili kwa jambo moja, ambalo suala hili ni la Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 chini ya jadweli ya kwanza kipengele cha 14. Jambo hili ilikuwa ni kubaki kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama yalivyo mambo mengine ya Muungano hayakuanzishwa vyombo vyengine Zanzibar, bali ilianzishwa afisi tu ya Zanzibar kama vile *TRA*, Polisi, JWZ, Uhamiaji na mambo mengine. Serikali yetu tusiibebeshe mzigo mzito ambao matokeo yake yatakuwa ni migomo ya wanafunzi na maandamano yasiokwisha.

Kwa hivyo, pamoja na mchango wangu huu mfupi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kojani naunga mkono hoja. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa kuchangia mswada huu wa mikopo ya elimu ya juu. Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mfupi sana, katika sehemu ya nne, wajibu wa sifa na uwajibikaji.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna mambo yamezungumzwa zaidi ya sita, moja ni jinsi ya utoaji wa gharama za malazi, chakula, vitabu vya kusomea na kuandikia, gharama za usafiri, gharama za utafiti, gharama za kazi za vitendo na gharama maalum na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikiri kwamba serikali imefanya hivi kwa nia nzuri sana, kuanzisha bodi ya mikopo, ingawa sasa hivi ipo wanafunzi wanakopa, lakini pia imefanya hivi kuipitia sheria kwa nia safi. Lakini jambo la kusikitisha katika nchi yetu kwanza katika Serikali yetu ya Zanzibar mipango ya rushwa bado hatujaidhibiti.

Mhe. Naibu Spika, fomu zinazotolewa kwa ajili ya mikopo zinatolewa kirushwa, kwa sababu kipindi kilichopita Tunguu wanafunzi waliyoomba ni zaidi ya 60, lakini wanafunzi wanalalamika watu waliopata fomu kwa bei ya uhalali ni wanafunzi 12 tu, waliobakia wote walikuwa wanapatiwa fomu kwa shilingi laki mbili au tatu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa nia nzuri anataka hili suala liendelee. Je, atasimamia vipi suala hili kulidhibiti ili kuepukana na mpango huu unaoendelea? Kwa sababu ni mpango unaendelea. Sasa Mhe. Waziri atakabiliana nalo vipi suala hili ili kuhakikisha walengwa wanapata fomu za mikopo bila ya kutozwa rushwa?

Suala jengine ni suala la utafiti. Wanafunzi wa Chuo Kikuu wanakuwa wanafanya utafiti karibu na kumaliza, lakini wanachosikitika wanafunzi ni kwamba utafiti una gharama na mtu anakuwa anazunguka sehemu nyingi, pengine anataka kwenda kwa usafiri wa magari au sehemu ya kuvuka pengine, utafiti ni utafiti unakuwa na gharama. Sasa linalosikitisha ni kwamba wanafunzi wanatakiwa wawe na fedha za kujikimu kufanya ule utafiti.

Kwetu Zanzibar wanapewa fedha hizo lakini wanapewa mwisho wakati pale wanapofanya ule utafiti zinatakiwa zipatikane kwa ajili ya kufanyia kazi, lakini wanapewa mwisho baada ya kumaliza kazi. Ninao mfano wa watu ambao walifanya utafiti kipindi kilichopita, lakini mpaka sasa hivi kuna wanafunzi zaidi ya 64 bado wamecheleweshewa kupewa fedha za utafiti. Kwa hivyo, Mhe. Waziri na hili nakuomba ulisimamie.

Suala jengine ni suala la uwiyano. Kwa sababu kama mimi mtu wa Micheweni kila tukija Barazani hapa tunazungumza kama Micheweni inaongoza kwa umasikini ni kweli kabisa, sasa nauliza uwiyano wa hawa wanafunzi wanaopata mikopo kwa sababu watu wanapitana kiuwezo kuna watu hawana uwezo kama watu wa Micheweni, kuna uwiyano gani wa wale watu ambao ni masikini kupewa kipa umbele cha zile fomu wanapokuja kuzitaka. Kwa sababu watu wa Micheweni ni watu wenye uwezo wa kwenda Chuo Kikuu au elimu ya juu, lakini je, kuna uwiyano gani? Namuomba Mhe. Waziri anambie Micheweni kuna wanafunzi wangapi ambao walipata nafasi zamu hii ya kupewa mkopo na wakenda katika elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie mchango wangu mfupi kwa kuunga mkono mswada kwa asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na mimi katika mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam.6 2001 na kuweka sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wake wote kwa kuona kwamba suala hili lina umuhimu

mkubwa na kuweza kulitayarisha kwa usarifu hadi kufikia hapa leo kuwa tunalijadili.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa mjumbe wa Bodi ya Chuo Kikuu cha Tunguu, vile vile na Bodi ya Chuo Kikuu cha Chukwani. Matatizo na mashaka makubwa ambayo wanafunzi walikuwa wakiyapata nimeona kwa kiwango kikubwa kabisa yamekidhi katika mswada huu. Matatizo yao yalikuwa ni makubwa na nilikuwa nikiyaeleza kila siku na kwa kweli baada ya kupitia hasa utaona kwa kiwango kikubwa kabisa matatizo hayo yametiliwa maanani, yamechukuliwa na naamini kwamba ikiwa walengwa na walengwa hapa ni wanafunzi pamoja na wazee wa hao wanafunzi.

Kama watachukua hatua au jitihada ya kusoma waraka huu utakaopitishwa wakauelewa vizuri naamini tutakwenda vizuri katika vyuo vyetu hakutakuwa na maandamano, msuguano wala matatizo yoyote. Kwa sababu sheria yetu imezingatia mambo mengi sana, utekelezaji ni suala jengine kwa sababu ni masuala ya kibinadamu, lakini naamini kuwa vile vile sheria yetu imeangalia namna gani ya kuweza kuwaweka wafanyakazi wa bodi kuweza kuwajibika ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ukiangalia katika ukurasa wa 84 mpaka 85 utakuta kwamba msaada wa fedha utakaotolewa chini ya kifungu cha kwanza cha mswada huu kinagharimia mambo tisa. Katika mambo tisa hayo ukienda chini zaidi penye ukurasa wa 85 endapo bodi itakuwa imeweka kiwango maalum kwa mujibu wa kijifungu cha (3) cha kifungu hiki ambacho kwa kila mwanafunzi, mzazi, mlezi au mtu mwengine anaehusika itamlazimu amchangie muhusika kiwango cha fedha ambacho kimewekwa na bodi. Hapa ndio nikasema kwamba lazima wazee pamoja na wale walengwa tuelewe.

Kwa mfano, kijana wako unae hapa hapa tena apewe chakula na wewe unaweza kumlisha, apewe usafiri na wewe unaweza kumsafirisha, kila tukiweza kutoa nafasi zaidi kwa watu wetu ndio nafasi zaidi itapatikana kwa wengi kusomeshwa kuliko kusema ziko fursa tisa lakini labda zote hizo huzipati.

Mimi kama nina uwezo basi watoto wangu wote nawasomesha kuanzia darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu ili nitoe fursa kwa wenzangu wengine ambao hawana uwezo waweze kusomeshwa. Kwa hivyo, naamini kwamba vile vile hili litazingatiwa kwa kina na katika sheria limo, mtu ambaye anaweza kugharamia gharama nafasi ipo.

Vile vile kuna suala ambalo linasema kwamba hii ni bodi ya mikopo naona kuna wachangiaji wengine wanafikiri labda hii ni Bodi ya Ufadhili, hii ni Bodi

ya Mikopo na kinachokopwa lazima kilipwe, kisipolipwa hakuna tena cha kukopwa. Kwa hivyo, lazima panapokopwa palipwe na kadiri patapolipwa ndio mikopo itakapozidi kutoka zaidi na zaidi. Kwa hivyo, uwezo wa bodi au wa Mfuko utategemeana na namna gani Mfuko unatumika, Mfuko kutumika na Mfuko kurejeshwa, ikiwa Mfuko unakopeshwa tu haurejeshwi itafika siku Mfuko utafilisika na tutashindwa kuwasomesha vijana wetu.

Kwa hivyo, ni suala zuri kabisa kuona kwamba lazima wazee pamoja na wote walengwa wanafahamu vizuri sheria hii na wanapoingia katika mikataba wanaingia kwa kuelewa wanafanya nini na kuelewa nini wajibu wao.

Vile vile ukienda katika masuala ya wajibu wa mkopaji. Wajibu wa mkopaji ni kulipa na wajibu wa yule mdhamini wa mkopaji ni kuhakikisha yule mkopaji amelipa. Lakini sheria yetu jamani haijamkandamiza hata kidogo huyo mkopaji, kwanza haijamtaka mkopaji kulipa kabla hajaanza kazi, kaambiwa kwamba yeye akienda kufanya kazi analipa. Kwa hivyo, kwa wale waliofahamu kwamba mwanafunzi atakwenda kudaiwa aa, mwanafunzi hadaiwi, mwanafunzi atadaiwa baada ya kumaliza masomo na kuanza kazi, akishaanza kazi ni lazima alipe mkopo na yule ambaye amemdhamini ahakikishe kwamba panalipwa, muajiri ahakikishe kwamba anamkata mkopaji na muajiriwa awe ana wajibu wa kulipa ule mkopo aliyokopa.

Suala la mkopaji katika kukosana nasaba kwamba mkopaji yeyote bila ya sababu za msingi atashindwa kulipa deni atafunguliwa kesi ya madai. Huyu anafunguliwa kesi ya madai hafunguliwi kesi ya jinai. Anafunguliwa kesi ya madai mkataba ameweka saini kwamba akimaliza masomo atalipa deni, masomo kamaliza, kazi anafanya, mshahara analipwa, ikiwa halipi lazima kesi ya madai ifunguliwe ili aweze kulipa, kama yeye lile deni hakulipa ndugu yake atakuwa hapati kusomeshwa, mwanawe hapati kusomeshwa, mjukuu wake hapati kusomeshwa. Kwa hivyo, suala la kulipa deni ni suala muhimu sana na mimi nasisitiza kwamba huu si mfuko wa ufadhili ni mfuko wa kukopa na kulipa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba hii sheria ni nzuri, imepangika na ukizingatia marekebisho ambayo yamo katika kurasa tatu hizi zilizokuja zimekidhi haja vizuri sana kwamba mambo mengi sana yamezingatiwa. Kwa hivyo, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni kwa niaba ya jimbo langu hilo nasema kwamba mswada huu nauunga mkono kwa asilimia mia moja na ninauombea kila la heri Inshaallah tuupitishe kwa pamoja chini ya Unaibu Spika wako na katika Baraza hili tukufu ili sheria hii ifanye kazi kwa haraka wapate kufaidika wanafunzi wetu wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia mswada huu. Mhe. Naibu Spika namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mzima na mwenye afya.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza niunge mkono hoja kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Magharibi ambao ndio walioniwezesha kufika hapa Barazani kuwawakilisha kama ni mwakilishi wao.

Zaidi ya hayo nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu wale ambao wameuchangia mswada huu na wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia kwa sababu moja au nyengine wote Mhe. Naibu Spika, tunawashukuru kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kuwa tokea Mapinduzi ya Mwaka 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitoa elimu bila ya malipo kuanzia ngazi ya msingi hadi elimu ya juu. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko mbali mbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, serikali imekuwa ikifanya mabadiliko mbali mbali ili kukidhi haja ya jamii katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata elimu.

Marekebisho tunayofanya leo hapa Mhe. Naibu Spika, ya sheria hii mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu yanalenga kuweka utaratibu ulio wazi utakaowawezesha wanafunzi wa Kizanzibari wenye sifa bila ya ubaguzi wa aina yoyote kupata mkopo kwa vigezo vilivyowekwa ili waweze kupata elimu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatambua wajumbe ambao wamechangia katika mswada huu.

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii)
2. Mhe. Salmin Awadh Salmin
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Mussa Ali Hassan
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
10. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
11. Mhe. Hassan Hamad Omar
12. Mhe. Subeit Khamis Faki

13. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi katika hoja zilizojitokeza hoja nzuri zenye mwelekeo wa kujenga kwa maslahi ya watoto wetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, taifa lolote lile ambalo linakosa wasomi basi taifa hilo bila shaka litachelewa kupata maendeleo. Hivyo, hatuna budi kushirikiana kwa umoja wetu wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wazee kwa upande mwengine na kama wizara kwa upande mwengine pia ili kuhakikisha hii azma nzuri ya serikali tunaifikia ya kupata vijana ambao watakuwa ni wasomi na wataweza kuisaidia nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mwenyekiti wa kamati tunamshukuru sana pamoja na kamati yake kwa mchango wake mzuri ambapo mchango huo aliuanza tangu kwenye kamati kwa kufanya marekebisho mbali mbali ya kuhakikisha mswada huu unakuwa bora na unakidhi haja na mahitaji hasa yanayotakiwa ya hivi sasa, lakini hata baadae tunakokwenda. Tunamshukuru ahsante sana pamoja na kamati yake.

Mhe. Salmini Awadh Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwanza alitupongeza, tunamshukuru kwa pongezi hizo kwa niaba ya wizara tunazipokea ahsante sana na tunamuomba azidi kushirikiana na sisi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin pia alizungumzia suala la wizara kuongeza mikataba ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi katika suala hili kama ifuatavyo. Kuna wafanyakazi wa aina mbili katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tuna walimu kwa upande mmoja na tuna watendaji kwa upande mwengine kama wizara. Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa walimu wale ambao tunawaombea mikataba ni wenye mahitaji maalum.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano hivi sasa tuna tatizo kubwa la walimu wa sayansi. Inapobidi mwalimu yule kumaliza muda wake na tuna mahitaji kama hayo na hatuna mtu wa kuweza kuikamata nafasi yake, basi huyo huwa tunafuata utaratibu kwa kuwaandikia Idara ya Utumishi nao huturudishia mwalimu huyo kwa mkataba.

Mhe. Naibu Spika, walimu wa *art* hata kama tutaandika tutahisi mwalimu huyu tuna haja nae lakini kwa kweli Idara ya Utumishi huwa hawaturudishii mwalimu huyo. Kwa hivyo, walimu ambao tunawapa mikataba ni walimu wa masomo ya sayansi tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa watendaji wetu wa wizara hii ni nadra sana kutokea. Isipokuwa tunao wachache katika kada ya ukaguzi ambao kwa kweli wewe mwenyewe utaona umuhimu wa watendaji hawa na uchache tulionao. Wakaguzi ni watu muhimu sana katika kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa maskulini mwetu inakidhi haja.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Salmin Awadh Salmin alitoa pendekezo la kupunguza siku 15 na kufikia siku 10 mwajiri awe tayari kayafikisha malipo yale kunakotakiwa. Naomba niseme kwamba hili hatuna tatizo nalo na tutalifanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Salmin Awadh Salmin alitaka kujua ni udhibiti gani ambao wizara itachukua kuhakikisha kuwa matumizi ya bodi ruzuku inayopatikana na misaada itakayotolewa kwa bodi inatumika kama ambavyo inatarajiwa itumike. Hili Mhe. Naibu Spika, tuliliona na liko katika kifungu cha 30 na 31 hata Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilisemea hili na kuipongeza wizara kama jambo hili waliliona.

Mhe. Naibu Spika, kifungu kile kiko kwenye hesabu za bodi hapa ndipo ambapo tutaweza kuidhibiti bodi kwa sababu inaelekeza kila baada ya mwaka ipeleke mapato na matumizi yake kwa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi kwa kusema kwamba hilo tumeliona na tutahakikisha tunalifuatilia na kulifanyia kazi kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman yeye alizungumzia kifungu cha 4 cha Muundo wa Bodi na kuzungumzia Uwezo wa Waziri Kuteua. Lakini pia akazungumzia wale wateuzi ambao wanaingia kwa nafasi zao 1, 2, 3 na 4. Mhe. Naibu Spika, pendekezo alilolitoa Mhe. Mwakilishi la kuwa Katibu Mkuu mwenye dhamana au mwakilishi wake. Akitolewa mwakilishi kupelekwa kwenye ile bodi basi awe wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, hio ndio maana hasa ya kifungu hichi. Labda niseme kilichokosekana ni tofauti ya uandishi, lakini hilo ambalo umetushauri ndilo lengo hasa lililokusudiwa. Katibu Mkuu akipeleka mwakilishi kwenye bodi basi mwakilishi huyo itakuwa ni wa kudumu kwenye bodi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman alikizungumzia kifungu cha 24. Hapa napenda kumueleza kuwa tatizo lililojitokeza ni yale marekebisho ya kamati hayakuwafikia wajumbe mapema kama ambavyo ilitarajiwa. Lakini kifungu hichi si namba 7 tu, namba 5 na 6 hizi tayari zilikuwa zimefutwa toka kwenye kamati.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye alizungumzia kifungu cha 24 (2) na kuitaka wizara kwa wale wanafunzi wetu ambao watamaliza masomo yao na kuajiriwa basi wapatiwe muda angalau wa miezi 6 ili waweze kujipanga na kujitayarisha.

Mhe. Naibu Spika, hili hatuna tatizo nalo tunalikubali na kwa wafanyakazi kuna sheria ambayo inatuongoza. Kwa sababu mfanyakazi wa serikali anatakiwa kuthibitishwa na anathibitishwa kuanzia miezi 6 mpaka mwaka mmoja. Kwa hivyo, kwa mfanyakazi wa serikali ataanza kukatwa makato haya baada ya mwajiri wake kumthibitisha kama tayari ni mfanyakazi wa serikali. Yule ambaye ataajiriwa binafsi basi baada ya miezi 6 ataanza kurejesha mkopo huu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye alizungumzia kuhusu kucheleweshwa kwa malipo katika vyuo. Hili nikiri kama ni kweli na kama wizara hatupendi hali hii iwepo. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunashona nguo kwa mujibu wa kitambaa tulichonacho. Kama wizara tungependa tukitiliwa fungu la mshahara basi na fungu hili la malipo ya wanafunzi walioko vyuoni liende sambamba na hili. Kwa sababu tunajua na tunaona wanatueleza wanafunzi tabu na idhilali ambayo wanaipata.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa mswada huu ambao naamini baada ya muda si mrefu utakuwa ni sheria bodi sasa itapatiwa ruzuku na hili ambalo tunalihitaji litaweza kufikiwa. Kwa hivyo, naomba tuupitishe mswada huu mia kwa mia ili haya matatizo tuliyonayo yaweze kutatuka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu pia alizungumzia suala la rushwa. Hili Mhe. Naibu Spika, kama nilivyowahi kulijibu hapo awali inawezekana kwamba ilikuwepo mianya ya rushwa lakini ni kutokana na utaratibu uliokuwepo haukuwa wa wazi. Kwa sababu hiyo ndio maana tumeleta kwenu marekebisho haya ili tuweze kuweka utaratibu mpya ambao tukiupitisha hapa utaweza kuziba hii mianya iliyokuwepo ya rushwa.

Lakini hata hivyo, niseme kwa sababu tunaofanya kazi nao ni binadamu na tunasema ‘binadamu ni mzito’. Tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, wananchi tushirikiane katika hili ili kuhakikisha kwamba haya matatizo madogo madogo yanaondoka. Haipendezi kitu kama hichi ambacho ni haki ya mwanafunzi ikawa kuna fununu kama hizi zinazungumzwa. Waswahili wanasema ‘lisemwalo lipo kama halipo linakuja’. Sasa ili lisifike basi tuhakikishe kwamba tunashirikiana pamoja kwa nguvu zote.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija Hassan Hija tunakushukuru kwa ufafanuzi ulioutoa na hii ndio maana ya wajumbe wa kamati. Kwa hivyo, kazi ambayo

umeifanya ndio hasa inayotakiwa ifanywe na kamati zetu katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru wale wote waliochangia kwa mara nyengine tena na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waunge mkono hoja hii kwa maslahi ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri wangu ameunga mkono hoja tukijaaliwa hoja nitatoa mimi baadae. Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuja kusimama tena hapa kwa kutoa ufafanuzi wa hapa na pale katika mswada huu ambao nimeuwasilisha asubuhi hii na wajumbe wamepata nafasi ya kuuchangia. Mhe. Naibu Spika, wajumbe wote waliochangia mswada huu kwa jumla ni 13 Mhe. Naibu Waziri amewataja ambao ni:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Mussa Ali Hassan
6. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
7. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
9. Mhe. Hassan Hamad Omar
10. Mhe. Subeit Khamis Faki
11. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
12. Mhe. Zahra Ali Hamad

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru wote na jambo linalonipa faraja ni kwamba wameipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua hii ya kuleta mswada huu hivi sasa ili kufanya marekebisho ya ile sheria iliyokuwepo Nam.6.

Mhe. Naibu Spika, huu ni wajibu wetu na kwa kweli tunatakiwa tutazame kila tukiona kwamba kunahitajika marekebisho basi tulete marekebisho na hii ndio kazi ya serikali muhimu kabisa tunayofanya.

Mhe. Naibu Spika, uamuzi unaochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ile ya mwanzo ya kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu na hii ya leo ya kuanzisha Bodi ya Mkopo kwa kweli ni uamuzi wa kijasiri sana, ni uamuzi wa kujiamini, ni uamuzi wa kusema tuna tatizo lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu yupo atatusaidia tutatue tatizo letu.

Mhe. Naibu Spika, tuna tatizo katika suala la elimu ya juu kwa vijana wetu na lazima wasome, hakuna njia ya kuepuka kuwa wasisome. Maana ulimwengu wanaokuja kuishi wao ni tofauti sana na ulimwengu tunaoishi sisi leo. Ulimwengu wao ni ulimwengu wa wasomi, ni ulimwengu utakaotegemea elimu ya juu zaidi kuliko elimu ya chini.

Mhe. Naibu Spika, enzi zinabadilika na kila zama na kitabu chake. Zamani ilikuwa mwanafunzi wa darasa la 4 alikuwa anatosha kupata ajira. Ukaja wakati mwanafunzi wa darasa la 8 anatosha kupata ajira. Ukaja wakati mwanafunzi wa kidato cha 4 anatosha kupata ajira hata matatizo. Ukaja wakati mwanafunzi wa kidato cha 6 anatosha kupata ajira hana matatizo. Lakini sasa hao tena wote hawamo katika soko la ajira, soko la ajira sasa liko katika elimu ya juu.

Kwa hivyo, vijana wetu hawa kama kweli tunawapenda lazima tufanye mpango wa kuhakikisha kwamba wanasoma na wanapata elimu ili kuweza kuingia katika hilo soko la ajira pamoja na kufanya mambo mengine ikiwa ya kujiajiri lakini wawe wana elimu ambayo ya kutosha. Hili ni suala muhimu kabisa Mhe. Naibu Spika, ndio nikasema uamuzi huu ni wa kijasiri.

Mhe. Naibu Spika, maana tunajua uchumi wetu sio mkubwa kiasi hicho. Vijana wetu wameamka siku hizi, wanasoma kweli kweli na wanafahamu umuhimu wa kusoma. Ndio maana nikasema katika kipindi cha asubuhi kwamba vijana wetu hivi sasa kila siku wanaongezeka wanaostahiki kuingia katika vyuo vikuu na kwengineko lakini uwezo wetu wa kifedha ni mdogo. Mwaka huu tu tumekuwa na wanafunzi 1,073 lakini tulioweza kuwaingiza katika kupata mkopo ni 700 tu kama nilivyosema mwanzo, kuna karibu 373 hawakupata.

Mhe. Naibu Spika, hilo ni tatizo na wala serikali haitaki kwamba iwe hivyo lakini uwezo ni mdogo. Kwa sababu hiyo ndio tukasema ni vizuri kuanzisha bodi ilishughulikie suala hili na hizi fedha tunazozitoa sasa kwa mkopo tuhakikishe zinazunguka. Mtu tumkopeshe azilipe tumkopeshe mwengine. Sina haja ya kusema sana nadhani wanafunzi ambao wameshasoma kwa mkopo katika utaratibu uliopita watakuwa wananisikia na wanajua kwamba hawajarejesha hata senti moja.

Sasa ni vizuri basi kuweka utaratibu utakaohakikisha kwamba wanarejesha hizi fedha. Ndio maana Mhe. Naibu Spika, tukaanzisha bodi sasa, badala ya kuwa na mkurugenzi wakati huo huo anaongoza idara na wakati huo huo ndio anashughulikia mikopo ni kazi ngumu. Ni bora kuwepo na bodi na mkurugenzi wake tunaondoa ile nafasi ya Mkurugenzi wa Elimu ya Juu ambaye tulikuwa nae huko nyuma tunakotoka, tunataka tuwe na mkurugenzi anayefanya kazi na

bodi ya mikopo yenye kujitegemea, ndio maana tunaongeza na watu atakaofanya kazi nao.

Wapi tutapata fedha jitihada zitapita, kazi zitafanywa, bila shaka bodi sasa hivi itakuwa na nafasi ya kufanya kazi kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya kuwakopesha vijana wetu zinapatikana. Hii ni kazi yao na tutawakabidhi waifanye kazi hiyo na mkurugenzi atakuwa wakati wote katika kazi hiyo kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa ajili ya mkopo. Bila shaka zitakuwepo zile fedha ambazo zinaingizwa kama ruzuku zinazopitishwa na Baraza lako tukufu hili Mhe. Naibu Spika. Lakini si itabidi ziongezwe, zitakazoongezwa na zitakazokopwa zote zitafanya kazi hiyo wakati wa kurejesha ile mikopo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu maana ya kutupongeza ni kwamba wamefahamu juu ya kazi hii ngumu. Hii ni kazi ngumu, ni tofauti kubwa sana na vile tunavyoizungumza na vile inavyotakiwa kuja kufanywa. Uwezo wetu wa kifedha sote tunaujua ni mdogo, njia zetu za mapato vile vile zina matatizo ni kidogo sana na fedha hizo ndio tunazotaka kufanya shughuli zote za kuendesha serikali.

Ni kweli elimu ya juu ni suala la Muungano lakini Waswahili wanasema ‘Hewe hewe na mwenyewe nyuma’. Kwa hivyo, ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatusaidia kwa sababu wapo wanafunzi wa Zanzibar ambao wanapata mkopo kutoka mfuko wa Muungano. Lakini kule kuna vigezo vyake sasa na sisi ni vizuri tuweke vigezo tukaviona kwamba vitawasaidia watu wetu wa hapa. Maana kule wakiamua tu sisi tutatoa mkopo kwa wanafunzi waliopata *division I* ndio hao tu basi. Sasa sisi tunaotaka wataalam, madaktari tukasema wa *division II* au *division III* anaweza akatusaidia si tutamchukua hapa. Ndio ile hewe hewe na mwenyewe nyuma kuliko tukategemea kwamba tutapata kule tu moja kwa moja.

Kwa hivyo, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatusaidia maana ni kweli hivi sasa wapo wanafunzi nje wanasoma na wamepata mkopo katika bodi ya mikopo ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, si haba tunalishukuru hilo kusema kweli.

Mhe. Naibu Spika, waliozungumza suala la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaunga mkono moja kwa moja ni suala ambalo lipo na ni zuri na watoto wetu wajaribu kuomba hapa Zanzibar na katika mfuko wa Jamhuri ya Muungano. Wamerekebisha tu mipango kidogo kwenye Jamhuri ya Muungano kule sasa hivi kwamba unapoomba upite katika ile *Tanzania Commission for University (TCU),* ili usije ukachukua mikopo

kutoka sehemu mbili, ikawa umepewa mkopo wa Zanzibar halafu umepata mkopo mwengine kutoka Jamhuri ya Muungano. Sasa pale wanaweza ku-*control* kabisa kuona ile hali namna inavyokwenda.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin amesema kwamba hawa watoto tunataka tuwasomeshe tena kwa nini kuna kifungu kinachosema kwamba kuwe na kigezo. Kigezo lazima kiwepo kwa sababu kinazingatia ule uwezo wetu. Tukikusanya tunaweza kusomesha tuseme wanafunzi 1,000 lakini walioomba ni 3,000, sasa ili uweze angalau hawa kuwahudumia ni lazima uwe na kigezo kitumike katika kuwachuja wale upate 1,000. Wale wengine watasubiri *inshaallah* tukipata uwezo na wao wataingia lakini lazima tuwe na kigezo.

Mhe. Naibu Spika, pia kigezo kinazingatia mahitaji yetu. Tuna mahitaji sisi maana liliulizwa swali kwamba mahitaji gani yanayohitajika ya mpango wa maendeleo. Mhe. Naibu Spika, tuna mpango wetu wa MKUZA ambao kwa sasa hivi tunautazamia hapa unamalizika mwaka 2015. Mle mna mambo yaliyopangwa yanahitaji kutekelezwa, tufanye nini katika afya, tufanye nini katika elimu, tufanye nini katika kilimo.

Kwa hivyo, tunapopeleka watoto kusoma lazima tuzingatie masuala haya ya MKUZA, tunahitaji nini kwenye afya, tunahitaji nini kwenye kilimo. Kama tunataka tuongeze mabwanashamba, hapa tuongeze wataalam wa wanyama imo ile katika suala la vigezo vyetu katika MKUZA. Sasa ndio maana tukasema kwamba lazima kuwasomesha vijana hawa na kwenda kwa mujibu wa malengo tuliyoyaweka katika mipango yetu ya maendeleo.

Kwa sababu huko mbele tunakokwenda mpaka 2020 ndio *vision* vyetu, tukifika huko mambo mengi haya tuwe tumeyatatua katika nchi yetu. Sasa hilo ni suala muhimu kabisa na ndio maana tumeweka vigezo hivyo ili tuweze kuelekeza huko. Sasa hawa wanafunzi wanaoomba nafikiri utafika wakati itabidi tuwatanabahishe tuwaambie kwamba safari hii tunataka kutoa fursa za elimu ya juu kwenye eneo kadhaa na kwenye eneo kadhaa. Itabidi tutangaze hivyo ili wale wanafunzi waamue kuomba katika maeneo kwa sababu ndio mahitaji yetu ya wakati ule sio mengine. Ni vizuri twende kwa mpango tuliokubaliana na tunautekeleza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amezungumzia suala la kuchangia. Ikiwa uwezo wako mdogo Mhe. Naibu Spika, lazima mambo ya kuchangia yawepo haya. Najua huko nyuma tunakotoka mwanafunzi anaanza tangu darasa la kwanza mpaka chuo kikuu bila ya kulipa hata senti moja. Lakini ni wakati ambao *population* ya Zanzibar ilikuwa laki mbili na hamsini mpaka laki tatu na hao wanafunzi waliokuwa wakisoma kwa wakati huo

hawakuwa wengi, unaweza ukahesabu kwa vidole wanaostahiki kwenda kusoma katika elimu ya juu.

Lakini sasa hivi *population* imeongezeka na wanaongezeka sana wanafunzi kusoma. Kwa hivyo, tunakuwa tuna wanafunzi wanasoma hapa ndani na wengine wanaosoma nje ya nchi. Mhe. Naibu Spika, wale wa nje ya nchi tunajua mzee wake hawezi akachangia chochote kule, sasa tukimpeleka Urusi, Ukraine, China tunamlipa *hundred percent* ya yote haya tuliyoyataja katika kile kifungu cha gharama zetu.

Lakini sasa kama alivyosema Mhe. Nassor Ahmed Mazrui hapa tunampeleka mtu Tunguu au Chukwani anaweza akasaidiwa na mzee wake maana ndio yupo hapa hapa. Kwa hivyo, ni vizuri tuwe tuna ule uamuzi unaolingana kwa mujibu wa ile kesi gani tunayoishughulikia, ile kesi ndio inatufanya tufanye uamuzi namna kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pia amezungumzia suala la riba ya benki. Riba ya benki bila shaka italipwa kwa kiwango cha benki ambayo sisi tumefungua akaunti. Huyo anayelipa hii *interest* ni yule ambaye amekaa na pesa zetu wee hataki kutulipa mpaka tunalazimika kumfikisha Mahakamani. Sasa yule basi na *interest* atulipe maana ameshakaa nazo sana. Kama hataki *interest* alipe mapema, ukilipa mapema hakuna matatizo. Mkopo ni lazima ulipwe hakuna njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika, masuala mengine Mhe. Naibu Waziri wangu ameyajibu naweza nikawa pengine nimeacha moja hapa na pale, lakini ndio binadamu. Kwa sababu haya sisi mawaziri huwa hatuyarikodi, huwa tunayaandika kwa mkono, sasa tunapoyaandikwa kwa mkono *speed* nayo inatakiwa iwe nzuri kuweza kuyashika yote kwa wakati mmoja na baadae uweze kuyatizama na kuyapatia majibu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman, alizungumza suala la kiongezwe kifungu katika kazi za bodi kinachoshughulikia bajeti. Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu kipo na kwa kuwa yeye pale anayosheria basi aangalie kifungu cha 29(1) cha ile sheria kimeeleza kwamba bodi pia itafanyakazi ya kushughulikia bajeti. Kwa hivyo, 1,2, na 3 atakuta imefafanua kusema kwali suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman alizungumzia suala la kamati ya bodi iliyotajwa katika kifungu hiki ni tofauti na kamati tendaji, kamati tendaji inafanyakazi za siku kwa siku katika afisi. Sasa hapa namjibu, katika suala zito kama hili ndio maana vikawepo vyombo vitatu. Cha kwanza kamati tendaji, ijapokuwa katika kuisoma ataikuta imeandikwa katika kifungu cha 16(5) chini. Kamati tendaji ndio hiyo inayofanyakazi za siku kwa siku na wao wenyewe

pake katika kufanyisha kazi zao wanakutana na Mkurugenzi ndio anaiongoza hiyo kamati tendaji, wanakutana pale, wanabadilishana mawazo wanaamua wanachoamua. Hao kamati tendaji walioko pale ndio wanapokea hizo fomu za maombi, wanazikusanya wao pale. Bila shaka katika kuomba kunakuja fomu ambazo zinastahiki kuzingatiwa na kunakuja fomu ambazo hazistahiki kuzingatiwa.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio kazi ya kwanza inayofanywa na kamati tendaji, wakimaliza wao ndio wanazipeleka kwenye kamati ya elimu ambayo itakuwepo pale pale, ambapo hiyo haitoongozwa na Mwenyekiti, tunafanya marekebisho, tulitoa ule waraka wa marekebisho, haikuongozwa na Mwenyekiti wa ile bodi yenyewe moja kwa moja. Sasa hivi pale atakuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, atakuwa ndio anaongoza ile kamati ya elimu. Pale ndio wanaanza kuchuja wale na ndio wanatazama kwanza mahitaji, na tufanye vipi ili tupeleke katika hiyo bodi kubwa ya kufanya maamuzi na ndio utaratibu wetu. Hata miswada ambayo tunaileta hapa Baraza la Wawakilishi mheshimiwa inaanza kwenye Kamati za Makatibu Wakuu, wakimaliza Kamati za Makatibu Wakuu zinakuja kwenye Baraza la Mapinduzi, wakimaliza huko ndio tunaleta hapa kwenye Baraza la Wawakilishi kwenye miswada mbali mbali ya sheria na mambo mbali mbali ambayo tunatakiwa tuyalete hapa, ndio utaratibu.

Kwa hivyo, nafikiri siwe kwamba ni jambo geni kabisa la kuwa tuna vyombo vitatu vya kushughulikia suala kubwa kama hili.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri ameshajibu kuhusu wajumbe wanaoingia kama ni makatibu wakuu wa wizara mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, lazima wateuliwe ili wapate ule uhalali. Sisi hapa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini ni lazima tuape, kwa kufanya ule uhalali wa kuingia katika hili Baraza la Wawakilishi. Huwezi tu kuchaguliwa huko ukaja hapa ukakaa juu ya kiti ukaanza kutoa mchango hapana ni lazima uapishwe. Sasa na hawa ni lazima wateuliwe. Kwa hivyo, ndio maana Mhe. Waziri kapewa uwezo wa kuwataja hawa. Kwa sababu tunakubaliana na wazo alilolitua Mhe. Rashid Seif kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ameambiwa aingie katika bodi hii, lakini akajibu kuwa, aah! Mimi kwa kazi zangu bora nimpeleke Kamishna wa Elimu. Sasa akimleta Kamishna wa Elimu, ndio basi yeye haji tena, anakuja Kamishna wa Elimu pale na mwakilishi wake na anahudhuria vikao vya kila siku, anakuwa ni mwakilishi wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, hiyo hata Bara kule ipo, Katibu Mkuu wetu anakuwa mjumbe kule, akini anapelekwa wakati mwengine Kamishna wa Elimu

anakuwepo kule muda wote basi, anakuwa anashiriki katika vile vikao. Kwa hivyo, itabidi wateuliwe katika hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohamme Haji Khalid alisema hili suala la zawadi liondoshwe, maana ni dalili ya kuwa rushwa. Mhe. Naibu Spika, zawadi hii hawapewi wajumbe wa bodi, zawadi hii inapewa bodi ambayo ni zawadi au mchango. Mtu anaweza kuwa kapata fedha zake nyingi tu akasema ngoja nizipeleke kwenye bodi kama ni zawadi zitasaidia kusomeshea watu, au nitakwenda kutoa mchango zitasaidia kusomesha watoto wa nchi hii. Hii Mhe. Naibu Spika, tunaiomba, hata wale wenzetu ambao wako nje ya nchi watumie nafasi hii, kuwasaidia watoto wa Kizanzibari hapa ili wapate elimu, kama kile anachokipata kule amekikusanya kiasi ambacho anaona kwamba hiki nawapelekea ndugu zangu wa Zanzibar wakapate elimu, basi atapata mahala pakupeleka ni katika bodi kusaidia. Kwa hivyo, na hao ndugu zetu walioko nje wanaweza kutusaidi kwa kutia mchango wao katika suala hili. Kwa hivyo, hio zawadi hapewi mjumbe wa bodi, ila inawekwa kwenye mfuko na itakuwa *accounted* na kila kitu, hivyo haina matatizo yoyote.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ametoa lalamiko zuri na bila shaka tutalizingatia, la kuteua wanafunzi wengi kuliko wote. Suala hili wakati mwengine linatokezea, tuna tatizo la madaktari, safari hii tukepeleka China watu karibu 46 kusomea udaktari. Hivyo, tutahangaika tupate fedha tuwalipie, hata kama tufanye *supplementary*, lakini tunalo tatizo la madaktari, kwa hivyo tumepeleka. Inabidi wakati mwengine tufanye hivyo, hatuna njia nyengine ili kuiwahi ile hali yenyewe, lakini hatuna haja tena ya kupeleka mwakani wala mwaka unaofuatia baadae, tumeshapeleka wasomi 46 tutizame watarudi wangapi, maana hapo ndio kwenye mtihani wenyewe Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, siku hizi dunia imebadilika Watanzania wanaowa China. Kwa hivyo, tena akifika kule anakua keshapata mwenyeji anakua keshahamia kabisa. Sasa hilo ni suala jengine. Lakini tunawaomba kwamba tukiwasomesha warudi, waje kufanyakazi kwao ili uzalendo upatikane wa kuisaidia hii nchi, hili ni suala muhimu sana Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, ni kweli inatokezea kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa, hutokea wakati tukapeleka watu wengi kutegemea mahitaji ili tuweze kuziba lile pengo kwa haraka kwa baada ya miaka, maana masomo ya udaktari yanachukua muda mrefu sana, kama miaka sita au saba. Kwa hivyo, ukiwapeleka kwa mkupuo moja inakuwa haijambo angalau baada ya miaka sita au saba mnakuwa katika kiwango kizuri sana wale wakirudi.

Mhe. Naibu Spika, zamani kulikuwa na utaratibu huu ambao Mhe. Ismail Jussa ameutaja wa *quotas* kwenye Chuo Kikuu katika Jamhuri ya Muungano, Zanzibar ilikuwa ina *quota* yake pale. Lakini baadae mambo yakabadilika

ikawa sasa hivi unakwenda kwa mujibu wa ulivyopasi. Sasa tumeona hapo ni tatizo ndio ule usimi unasema kwamba “hewe hewe na mwenyewe nyuma”.

Kwa hivyo, sasa hivi tunachotaka kufanya ni kwamba turudi tena kwenye *paper*, tuwe na *quota* Zanzibar kwenye masuala haya *Inshaallah*, turudi tena kwenye *quota* zetu tuwe na *quota* na sisi. Kwa sababu sisi tuna serikali tunaendesha hapa ni lazima tuwapatie vijana wetu ili wasome. Kwa hivyo, suala hili tunalikubali halina matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe alisema Mwenyekiti wa Bodi atowe vigezo. Sisi katika hii sheria tumemuwekea kigezo Mkurugenzi na akisome kwenye kile kifungu cha 16 kimechambua sifa za Mkurugenzi. Lakini Mhe. Naibu Spika, najua kwamba Mhe. Rais atatumia busara. Namuomba radhi kwamba hapa tumeona ni kawaida huwa tunafanya kama hivyo Mwenyekiti, huwa anachukuliwa mtu ambaye mwenye busara anaweza kuongoza vile vikao. Lakini Mkurugenzi awe na sifa na tumeweka mule kwenye sheria sifa za Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo wakati mwengine bwana huu uamuzi ni wa kijasiri sana, huwa tunachelewa kweli kupeleka fedha, tunakiri. Tunachelewa kwa sababu tunakuwa hatunazo, mpaka tutafute tuzipate, halafu ndio tupeleke. Lakini tutajitahdi kuona suala hili, madamu sasa hivi tunaweka bodi, nafikiri hili suala sasa hivi litapungua kasi hii ya kuchelewa sana. Vijana wetu wasipate tabu ya kutofanya mitihani kama fedha hizo hazijaliwa na matatizo mengine ambayo yanatokea. Kwa hivyo, tunataka tujitahidi sana.

Vile vile aliuliza huyu mjumbe aliyomo kwenye hii kamati ndio yule yule ambaye ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi alikwishaingia kwenye ile bodi. Ndio, ni yule yule tu tunamuongezea jukumu tu la kwenda kule.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, yeye alitoa ufafanuzi na tunamshukuru sana kwa kutusaidia na kututanabahisha kikao chako hiki, kwamba kuna marekebisho ambayo tumeyagawa ni vizuri yatizamwe hayo marekebisho.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, nimeshayazungumza masuala yao na Hija Hassan Hija ndio nimeshayajibu masuala yake, tunamshukuru sana kwa ufafanuzi wake. Pia alitoa indhari, lakini hakuimaliza pale. Aliomba waziri azingatie wakati wa kutunga kanuni. Sasa pale Mhe. Naibu Spika, ulimuomba kwamba aweke aje aseme jioni. Akakuambia hapana, musinipe jioni bwana, basi namaliza hapa hapa. Sasa hatukujua zaidi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, bado nafasi ipo, aonane na sisi atuambie tuchukuwe indhari katika jambo gani. Hilo tutalifanya mheshimiwa.

Mhe. Mussa Ali Hassan, alizungumzia suala la vijana wanaosomeshwa wapatiwe ajira. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, lengo la kuunda bodi ya mkopo ni kuwawezesha vijana wetu wapate uwezo wa kuingia katika soko la ajira. Soko la ajira siku hizi liko kwenye elimu ya juu, sasa ikiwa vijana wetu hatuwasaidii watashindwa kusoma katika elimu, basi hawatoingia katika soko la ajira. Kwa hivyo, tunataka wajitahidi.

Mhe. Naibu Spika, soko la ajiri, tushukuru na tushukuru sana, kwamba tunakuja katika *East African Common Market* sasa hivi, ambapo Mzanzibari anaweza kufanya kazi Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, hapa hapa Zanzibar na hata Tanzania Bara. Lakini wka vipi si lazima awe nayo elimu. Vinginevyo tutalalamika tu kwamba mbona sisi hatupati kule Afrika ya Mashariki. Ndio madhumuni ya jitihada hii kwamba apate elimu na aweze ku-*fit* katika lile soko la ajira kule, ndio maana tukaweka utaratibu huu na tukautilia mkazo katika marekebisho haya ili kuwawezesha vijana wetu kuingia basi katika hilo soko la ajira. Vyenginevyo kama hatuna utaratibu wowote, tukasema haa! Sisi masikini tukae tu hivi hivi, hapana tujikaze kaze hivyo hivyo, tutaona mbele tu. Wewe ukiwa katika kiza basi jikaze tu mara utaona mwangaza unakuja huo hapo unatoka, hivyo tujikaze kaze.

Kwa hivyo, Mhe. Mussa Ali ni kweli tuwaajiri hawa na kwa kweli sisi hatupendelei ule utaratibu wa kuongeza mkataba na umepungua sana kuliko ulivyokuwa sasa hivi, Idara ya Utumishi wanajitahidi sana kupunguza suala la kuongeza mikataba ili kuwapa vijana wetu nafasi. Lakini wasome na wapasi vizuri ili waweze kuingia katika soko la ajira.

Mhe. Naibu Spika, ama hili ombi moja, sijui Baraza litaamua vipi kwamba mkataba uletwe katika Baraza la Wawakilishi kwa kuidhinishwa kuwa uongezwe au usiongezwe. Suala hili Mhe. Naibu Spika, ni gumu kidogo, kwa sababu ni suala la siku kwa siku na katika kuendesha serikali mnagawa na madaraka kwa vyombo mbali mbali.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, namshukuru sana kwa marekebisho mengi aliyoyafanya kwenye mswada pamoja na kutengeneza Kiswahili na mambo mengineyo. Niliwahi kusema juzi nilipokuwa pale *Eacrotanal* kwamba nadhani tunawajibu kweli, nakubaliana na yeye kwamba tunawajibu wa kukisoma Kiswahili. Maana usiposema Kiswahili basi utasema Kingereza kwa Kiswahili.

Kwa mfano, ukisema tunamwita mheshimiwa fulani aje atowe neno la shukrani, yaani hiyo ni votothink ni Kingereza hicho. Badala ya kwenda kwa

miguu, anasema anakwenda kwa mguu yaani *walk on foot* ni Kingereza hicho, lakini kimeingia kwenye Kiswahili tu. Lakini tukisema Kiswahili tunajua kushukuru, kwenda kwa miguu hiyo tunajua ndio Kiswahili chetu cha kawaida. Sasa tukitafsiri hivi tunapata matatizo mara nyingi. Kwa hivyo, ni kweli Mhe. Abdalla Juma, tunashukuru sana kwa indhari yako uliotoa na tutaielekeza katika suala la kuandika Kiswahili sanifu katika mambo yetu mbali mbali.

Lakini mswada unaotumika hasa ni ule mswada wa Kingereza na wanasheria wanapendelea sana kutumia miswada ya Kingereza, kwa sababu ya kimbia hizi tafsiri. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, tumesema kwamba mkopaji aliyekwisha kuajiriwa basi alipe nusu ya deni lake ndani ya miezi sita, ni namna ya kupiga hesabu kila atakayechukua kwa miezi sita itakuwa asilimia 50. Halafu kilichobakia atakilipa kidogo kidogo kwa utaratibu atakaoamuliwa na bodi, lakini atalipa wote, lakini kulipa haraka haraka ndani ya miezi ni kwa sababu ya kumuezesha na mwengine naye aweze kukopa ndio maana yake.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema, makisio yaliokwenda pale yalikuwa ni bilioni 4, lakini tulipata bilioni 2.5 na tumeshazimaliza. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atatufikiria vyengine tufanyeje, maana wanafunzi ni wengi wale wako zaidi ya 300, hiyo ndio hali halisi.

Katibu hajatajwa katika sheria, lakini mimi nataka kusema hapa kwa wale wote waliosema kwamba maana katika kifungu cha 16 ametajwa Mkurugenzi wa Bodi kuwa ndio katibu. Kwa hivyo, Mkurugenzi wa Bodi ndio amepewa nafasi ya ukatibu katika kifungu cha 16. Kwa hivyo, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba katibu awe ni katibu tu basi abakie na kazi yake ya utendaji na tusimuhesabu kwamba ni mjumbe wa bodi, awe ni katibu tu ashughulikie mambo yake ya ukatibu pale, basi hana tena suala jengine.

Mhe. Mwinyihaji, namshukuru sana kwa ufafanuzi wake mzuri alioutoa na mfano mzuri alioutoa juu ya matatizo mbali mbali ya namna tunavyopata tabu kwa umaskini wetu kuweza kusoma.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, na yeye alitoa maelezo mazuri tu. Mhe. Naibu Spika, umeshanionesha saa, ni kweli saa nimeshaiona kuwa inakwenda sana. Maana humu ndani hujui kama mchana umeshaondoka huko nje, humu ndani unaona hali ndio ile ile ya asubuhi ulioingia.

Mhe. Naibu Spika, bodi itakuwa na fungu lake la fedha kama kawaida na itakuwa imepewa ruzuku yake na pesa za mfuko kwa ajili ya kuhudumia elimu ya juu, na nyengine watakuwa wanatafuta wenyewe Mhe. Suleiman Hemed.

Vile vile nimeshazungumza maana ya ile *interest* kwa nini inazo *interest.* Kwa mtu anayelipa chapu chapu hakuna *interest*.

Mhe. Hassan Hamad Omar suala lako nimeshalifafanua kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni kweli ina wajibu, lakini na sisi wenyewe tujikaze huku na huku katika kushughulikia masuala hayo.

Mhe. Subeit Khamis Faki, kuhusu suala la rushwa limeshajibiwa. Mhe. Subeit alisema suala hili tushirikiane na kama kweli kuna vijana wamekubali kutoa Shs. 200,000/- au Shs.300,000/-, aah! Kwa nini wakakubali kutoa Shs.200,000/= au 300,000/= wasiripoti. Uongozi wa wizara hauna habari kama kuna mwanafunzi katoa hizo Shs. 200,000/= au Shs. 300,000/=, lakini kakaa kimpya huko keshaliwa hizo pesa halafu ndio anakuja kusema mimi nimetozwa Shs. 200,000/= pale, sasa huyo hasaidii serikali kwa kimya hivyo. Ni lazima tusaidiane katika hili. Hao wanafunzi wanapokwenda huko wakatozwa pesa, basi waseme ndio ushahidi huo na ndio umeshapatikana kabisa na tutawashughulikia na suala hili tutalishughulikia bila shaka yoyote.

Ni kweli Mhe. Subeit Khamis Faki wakati mwengine huwa tunachelewa kutoa fedha za utafiti kwa matatizo haya haya. Hili suala la uwiano siwezi kumjibu kwa ghafla hapa, kwa sababu huu mpango umeanza muda mrefu na itabidi lazima nikapekuwe ma-*file* ili kuyaangalia masuala haya.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, nakushukuru sana kwa ufafanuzi wako ulioutoa pale pale na mimi naungana na wewe. Mkopo ulipwe ndio tutaweza kusomesha watu wetu, tukamatane ili mkopo ulipwe. Mkopo ukilipwa ndio tutapata hii nafuu, mkopo kama haukulipwa ndio tutaendelea kuwa na matatizo.

Vile vile nakushukuru ulivyoeleza juu ya masuala ya kesi ya madai na mambo mengineyo. Mhe. Naibu Waziri na wewe nakushukuru kwa ufafanuzi wako.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba kuomba radhi kama kuna hoja ambazo sikuzigusa yaani zikuzitolea ufafanu, basi mimi niko tayari kuendelea kupokea mawazo zaidi, maana hii hapa haijawa sheria. Kwa hivyo, niko tayari kupokea mawazo zaidi ili kushughulikia masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2011

Kifungu cha 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tufanye marekebisho madogo katika tafsiri ya mwanafunzi aliyekatisha masomo, hapa pametajwa mambo katika tafsiri yake, maana yake ni mwanafunzi ambaye amepewa mkopo na akashindwa kuendelea na masomo yake ama kwa kiwango duni cha mafunzo, tabia mbaya au kwa utoro. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba nipendekeze kwamba kisomeke, baada ya kiwango duni cha mafunzo, kwanza itanguliwe na uwezo mdogo wa mwanafunzi, maana kiwango kidogo cha mafunzo ni kwa ile taasisi inayotoa. Lakini inawezekana vile vile ukaamua kukatisha masomo kutokana na uwezo mdogo wa mwanafunzi kushindwa kuelewa ndio ikabidi kukatisha masomo, kwa hivyo mbali ya tabia mbaya na utoro tuongeze na uwezo mdogo wa mwanafunzi katika kifungu kile cha tafsiri ya mwanafunzi anayekatisha masomo.

Halafu sijui niendelee na mengine kabisa Mhe. Mwenyekiti katika tafsiri au niende moja moja.

Mhe. Mwenyekiti: Twende moja moja kwanza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimeyafahamu marekebisho yake. Suala la mwanafunzi ambaye kwa bahati mbaya ana uwezo mdogo, mimi nadhani ni yule mwanafunzi anayetakiwa kurudia masomo na huko tumeweka tafsiri ya mwanafunzi anayerudia masomo,

ambaye itabidi aufanye tena mtihani wake, hiyo ndio maana yake. Yule mwengine yeye ana utukutu wa aina fulani, tabia na mengineyo vile vile tumemuwekea kifungu chake. Lakini yule anayerudia masomo, yule ndio kidogo uwezo wake mdogo. Sasa tena kuna mara zake kule, ikiwa mara zote anaendelea kukosa tu tena itakuwa ndio basi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naikubali tafsiri ya Mhe. Waziri, lakini mimi niko katika kui-*protect* hiyo, kwamba isije ikafika pahala ikawa haiwezi ku-*claim* mambo haya, kwa sababu anaelewa Mhe. Waziri kwamba uwezo mdogo sio tu kurejea. Wako wenye uwezo mdogo ambao tunasema wanapigwa *disco*, wanakuwa *disqualify*. Sasa akitokezea mtu kwa sababu ya uwezo mdogo kawa *disqualify* na budi mmeshampa mkopo, huyo atakuwa haingii katika kifungu hiki ikawa bado anatakiwa kurejesha. Kwa hivyo, nilikuwa nasema tulitazame kwa upana wake, ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ikifika kiwango cha kufika tena kupata *disqualification* tena hiyo ndio hatuna vya kumsaidia vyengine. Lakini tutajitahidi kuiangalia sheria.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika tafsiri kwenye elimu ya juu, kuna neno pale kuzawadiwa. Mimi nilikuwa nadhani lugha ambayo ingetumika vizuri katika mambo haya ni kutunukiwa shahada au stashahada, kuliko kuzawadiwa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tulibadilishe lile neno badala ya kuzawadiwa litumike neno kutunukiwa pale. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, nadhani haina tatizo. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naona suala hili katika marekebisho lilishughulikiwa, limo katika marekebisho kwenye masuala ya ufafanuzi sehemu ya kwanza, hiyo stashahada imeshughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, imo kwenye marekebisho.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa imechukuliwa kuwa imekubaliwa ni sawa, lakini neno lililotumika humu ni kurekebisha stashada na kuandika stashahada, lile neno la kuzawadiwa na kutunukiwa halikuingizwa katika marekebisho ya kamati, ndio maana nikalitaja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Sawa Mhe. Mwenyekiti, na ni kweli kwamba marekebisho yaliyofanywa ilikuwa imeandikwa stashada na hivi sasa imeandikwa stashahada. Sasa yeye anachozungumzia ni suala la

kuzawadiwa, sijampata vizuri hapo, unajua hii *echo* ya humu ndani ya Baraza ina matatizo yake Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: ni kutunukiwa. Badala ya neno kuzawadiwa iwe kutunukiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kutunukiwa, nakubaliana na wewe.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika hiyo sehemu ya mwisho kwenye mswada wa Kiingereza Mhe. Mwenyekiti, kuna neno "*government*" limetafsiriwa, lakini kwenye mswada wa Kiswahili halipo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba na hili liingizwe katika mswada wa Kiswahili. Katika mswada wa Kiingereza ukisoma *government*, imeandikwa *government means the revolution government of Zanzibar*. Katika huu mswada imetajwa sana serikali, sasa hapa katika Kiswahili haikuwekwa hilo neno *the revolution*. Kwa hivyo, naomba nalo vile vile Mhe. Waziri akubali liingizwe, ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ipo tafsiri hapa inasema serikali maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Ipo eeh.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tafsiri ipo, kwa hivyo tunaendelea.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 3 Kuanzishwa kwa Bodi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 4 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia kulikuwa na utata wa Mkurugenzi kuwa ni *member* wa bodi au sio *member*. Wakati wa ufafanuzi wa Mhe. Waziri alitaja neno katibu awe katibu. Sasa sisi hatukulifahamu kuwa katibu sasa atakuwa ni mwengine na Mkurugenzi ni mwengine, au yule Mkurugenzi ndio anakuwa katibu anatolewa katika bodi, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba tumekubaliana na mapendekezo ya kuwa Mkurugenzi kumfanya ni katibu tu na sio mjumbe wa bodi tena, ni katibu wa bodi moja kwa moja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Imekubalika hoja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Rashid Seif kukubali, lakini mimi naomba ikiwa Mkurugenzi sasa anatolewa katika bodi awe sio mjumbe, basi maana yake hapa katika hao wajumbe wa bodi awe anafutwa au sikufahamu pengine Mhe. Waziri kakusudia hivyo tumfute au vipi, maana yake sijasikia hilo neno kuwa atafutwa hapa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio tunapitisha marekebisho muafaka. Kwa hivyo, sasa hivi itakavyokubaliwa hapa kwamba katibu ndio atakuwa ni katibu, kwa hivyo sasa hivi ataandikwa Mkurugenzi ambaye atakuwa ni katibu wa bodi moja kwa moja, hatotajwa kama ni mjumbe. Sasa hivi wajumbe watabakia 9 ambapo itapatikana witri wakati wa kufanya maamuzi na wakati huo ndio itakuwa ile kura ya Mwenyekiti ni ya uwamuzi hasa, kwa sababu patakuwa pana witri mzuri kabisa.

Kifungu cha 4 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia nilitaja wasi wasi wangu kuhusiana na kutajwa kwamba Katibu Mkuu au mwakilishi wake. Katika majibu ya waheshimiwa wawili, yaani Mhe. Naibu Waziri na mwenyewe Mhe. Waziri walitaja kwamba ndivyo ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Mhe. Waziri kuwa sheria inakubali kwamba ndivyo ilivyokusudiwa bila ya kuandikwa na hii haitoleta matatizo ya siku za mbele katika kutekeleza sheria hii, au sheria inahitaji kuwa neno liandikwe bila ya kuwa *by implication.*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati wa majumuisho yangu ni kwamba Katibu Mkuu sasa ataamua kuingia mwenyewe kwenye bodi au ataleta mwakilishi, akimleta mwakilishi basi ni wa kudumu. Sasa haya ni marekebisho, waandikaji wa sheria watajua lugha ya kuweka, mimi sio mwanasheria najua kueleza nini tumekubaliana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kama kilivyoandikwa kinasema Katibu Mkuu wa Wizara dhamana wa elimu au mwakilishi wake. Kwa hivyo, kifungu kinakubali kwamba Katibu Mkuu ikiwa anakwenda yeye mwenyewe au mwakilishi wake mmoja kati ya hawa wawili, akiamua kwenda mwenyewe sawa, akiamua kumpeleka mwakilishi wake ni sawa, kwa sababu kifungu kinasema Katibu Mkuu au mwakilishi wake, kwa hivyo yeye ndiye ataamua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kutokana na ufafanuzi aliotoa Mwanasheria Mkuu kwamba pana tatizo kama tulivyolizungumza, kwamba tungetarajia kuwa bodi ingekuwa na *sequence* katika mikutano yake bila ya kukatisha katisha. Sasa leo anakuja mjumbe huyu, kesho anakuja mwengine si itakuwa ni mashaka kila mmoja anaweza kujieleza kivyake.

Kwa mfano, Makatibu Wakuu watatu wakienda katika kikao kilichopita, kikao kijacho kikapeleka wawakilishi wengine watatu, je kikao hiki kitakwenda vipi na bodi itakuwa ipo. Sasa kidogo tunapenda tupate ufafanuzi hakutokuwa na mashaka hapa na mambo yenyewe yanahusiana na mikopo ya wanafunzi ambao inatakiwa kwa wakati ipatikane.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya yaliyokuwepo hapa, hao Makatibu Wakuu wanaweza wakaenda katika hii bodi au wawakilishi wao. Lakini tujuwe tu kwamba Katibu Mkuu anapokwenda, anakwenda pale kikazi, haendi Katibu Mkuu kama fulani. Kwa hivyo vyovyote atakavyokwenda bila shaka ana wajibu wa kutekeleza na anaporudi ni kuwaarifu uongozi wake wa wizara, kwamba kilichozungumzwa ni hiki na hiki na tunatakiwa tutekeleze haya na haya.

Kwa hivyo, hata huyo mwakilishi wake atakayekwenda, wakati anapokwenda atajua na atakuwa na uhakika kwamba yaliyozungumzwa katika kikao kilichopita yalikuwa ni haya na yanayotaka kutekelezwa ni haya. Kwa hivyo, anapokwenda Katibu Mkuu au mwakilishi wake Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba hakutokuwa na matatizo yoyote, kwa sababu ile *sequence* ambayo anayosema yeye mwakilishi itakuwa ipo kutokana na maelezo ambayo yule aliyekwenda atayatoa katika wizara yake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba uliozungumzwa nakubaliana na hoja, tuendelee.

Kifungu cha 4 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 5 Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 6 Kikao na Maamuzi ya Bodi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba niwekwe sawa tu katika mchango wangu, kifungu cha 6(9) katika ukurasa wa 82 pale juu. Mhe. Mwenyekiti, niliulizia *status*, hapa panazungumzia kwamba mjumbe ambaye hakuhudhuria kikao cha bodi kwa vikao vitatu mfululizo, bodi itaishauri mamlaka iliyomteuwa na kutafuta uwezekano wa kumteuwa mtu mwengine. Nisema kuwa katika bodi kuna wajumbe wengi ambao wameingia kwa nafasi zao.

Kwa hivyo, nilitaka kupata maelezo kuwa sisi tunakamilishaje hapa, kuwa hawa pia wakiwa kwa nafasi zao hawakuhudhuria wanaacha hizo nafasi zao. Kwa mfano hao Makatibu Wakuu, kidogo nilikuwa naomba maelezo kuhusu kifungu hiki, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, analouliza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ni suala la kawaida ambalo linaweza likatokea. Lakini tunadhania kwa mtu kama Katibu Mkuu ambaye kapewa dhamana kwa kuaminiwa, nadhani sio rahisi yeye kuwacha kuhudhuria vikao vile Mhe. Mwenyekiti, ipo tafsiri inayosema hapa kwamba serikali maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tafsiri ipo. Kwa hivyo, tunaendelea.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 3 Kuanzishwa kwa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kulikuwa na utata wa Mkurugenzi kuwa ni mjumbe wa bodi au si mjumbe. Sasa wakati Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho alitaja neno Katibu awe Katibu na wala hatukulifahamu. Kwa hivyo, Katibu atakuwa ni mwengine na Mkurugenzi ni mwengine au yule Mkurugenzi anakuwa katibu na kutolewa kwenye bodi. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba tumekubaliana na mapendekezo ya kuwa Mkurugenzi kumfanya kuwa ni Katibu tu na wala sio Mjumbe wa Bodi tena. Kwa hivyo, ni Katibu wa Bodi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali hoja na tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Rashid Seif Suleiman kukubali, ninaomba sasa ikiwa Mkurugenzi anatolewa katika bodi asiwe mjumbe, basi maana yake hapa katika wajumbe wa bodi afutwe, kwa sababu sikumsikia Mhe. Waziri kusema kwamba atafutwa hapa kwenye wajumbe wa bodi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo tunapopitisha marekebisho muafaka. Kwa hiyo, itakavyokubaliwa hapa kwamba Katibu atakuwa ni Katibu, basi Mkurugenzi atakuwa Katibu wa Bodi na wala hatotajwa kuwa ni mjumbe wa bodi. Kutokana na hali hiyo wajumbe watabakia tisa ambapo itapatikana witri katika kufanya maamuzi na ile kura ya mwenyekiti ndio itakuwa ya uamuzi hasa, kwa sababu kutakuwa na witri nzuri sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilitaja wasi wasi wangu kwamba Katibu Mkuu au Mwakilishi wake. Sasa katika majibu ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Naibu Waziri wake, walitaja kwamba ndivyo ilivyokusudiwa.

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba sheria inakubali kwamba ndivyo ilivyokusudiwa bila ya kuandikwa na hali hii haitoleta matatizo siku za zijazo katika kutekeleza sheria hii au sheria inahitaji neno liandikwe bila ya kuwa *by implication*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho ni kwamba Katibu Mkuu sasa ataamua kuingia mwenyewe kwenye bodi au ataleta mwakilishi na atakapo mleta mwakilishi ni wakudumu. Sasa haya ni marekebisho na waandikaji wanasheria watajua lugha ya kuweka, kwa sababu mimi si mwanasheria, isipokuwa najua kueleza nini tumekubaliana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kama kilivyoandikwa kinaeleza kwamba Katibu Mkuu wa Wizara dhamana ya Elimu au Mwakilishi wake. Kwa hivyo, kifungu kinakubali kuwa Katibu Mkuu ikiwa anakwenda yeye mwenyewe sawa au mwakilishi wake moja katika hao wawili, kwa sababu kifungu kinasema Katibu Mkuu au Mwakilishi wake, sasa yeye ndiye atakayeamua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kutokana na ufafanuzi aliotoa Mhe. Mwanasheria Mkuu kuwa kuna tatizo kama tulivyolizungumza, kwamba tungetarajia bodi ingekuwa na *sequence* katika mikutano yake bila ya kukatisha katisha. Sasa leo anakuja mjumbe huyu na kesho anakwenda mwengine si itakuwa mashaka na kila mmoja anaweza kueleza kwa namna yake.

Kwa mfano, Makatibu Wakuu watatu wakenda katika kikao kilichopita na kikao kijacho wakapeleka Wawakilishi wengine watatu, kweli kikao hiki kitakwenda vipi na bodi inakuwa hivyo. Kwa hivyo, kidogo tunaomba kupata ufafanuzi kwamba hapatokuwa na mashaka hapa na masuala yenyewe yanahusiana na mikopo ya wanafunzi, ambayo inatakiwa kwa wakati ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wametoa maelezo, lakini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria naye anataka kusaidia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya yaliopo hapa hawa Makatibu Wakuu wanaweza kwenda kwenye hii bodi au Wawakilishi wao. Lakini tujue tu kwamba Katibu Mkuu anapokwenda anakwenda pale kikazi na wala haendi kama Katibu Mkuu fulani. Kwa hivyo, vyovyote atakavyokwenda bila ya shaka anawajibu wa kutekeleza na kurudi ni kuiarifu ile timu yake ya wizara kwamba kilichozungumzwa ni hiki na hiki na tunatakiwa tutekeleze haya na yale. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hata huyo Mwakilishi wake atakapokwenda wakati anapokwenda, basi atajua na atakuwa na uhakika kwamba yaliyozungumzwa katika kikao kilichopita yalikuwa ni haya na yanayotaka kutekelezwa ni haya. Kwa hiyo, anapokwenda Katibu Mkuu au Mwakilishi wake Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakutokuwa na matatizo yoyote, kwa sababu ile *sequence* anayoisema yeye Mwakilishi itakuwa ipo, kutokana na maelezo ambayo yule aliyekwenda atayatoa katika wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Waheshimiwa Wanasheria wawili wameshatoa maelezo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba uliozungumzwa nakubaliana na hoja tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu cha 4 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 5 Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kupata ufafanuzi kidogo, wakati nilipokuwa nikichangia katika kifungu cha 6 (9) kwenye ukurasa wa 82 niliulizia *status* na hapa kinazungumzia kama mjumbe ambaye hakuhudhuria vikao vitatu mfufulizo, basi bodi itashauriana na mamlaka iliyomteua na kutafuta uwezekano wa kumteua mtu mwengine.

Vile vile nilisema katika bodi kuna wajumbe wengi ambao wameingia kwa nafasi zao, sasa nataka kupata maelezo kwamba sisi tunavipitisha vipi, kwamba hawa pia kama hawakuhudhuria kwa nafasi zao wanaacha hizi nafasi zao au vipi kwa mfano Makatibu Wakuu. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi kidogo kuhusu kifungu hiki.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, analoliuliza Mhe. Mjumbe ni jambo la kawaida ambalo linaweza kutokea, lakini tunadhani kwa mtu kama Katibu Mkuu ambaye amepewa dhamana kwa kuaminiwa, basi nafikiri si rahisi kuacha kuhudhuria vikao vile mpaka vitimie vitatu, lakini katika hali ya kawaida inaweza kutokea. Sasa itakapotokea basi itakuwa amejiondoa yeye mwenyewe na ni vikao vitatu sio mikutano mitatu ndivyo tulivyofanya marekebisho.

Kwa hivyo, suala hilo linaweza kutokezea na sisi tunatizama sana kwa hawa wajumbe wengine wanaoingia kutoka vyuoni kama vile wanafunzi na sehemu nyengine. Lakini kama Katibu Mkuu ana-*respect* dhamana yake, basi atajitahidi sana kuona anahudhuria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tuendelee.

Kifungu cha 6	Vikao na Maamuzi ya Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7	Muda wa Ujumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8	Kutumika kwa Muhuri wa Bodi.
Kifungu cha 9	Malipo ya Wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 10	Uwezo wa Bodi kuajiri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11	Kuanzishwa kwa Kamati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 12	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilitaja wasi wasi wangu kwamba bodi hii haikuekewa *secretariat* na badala yake kumeundwa hii kamati.

Kwa hivyo, naomba kupata ufafanuzi wa usahihi wa jambo hili, kwa sababu kifungu cha 11 kimetaja hao wajumbe watakaofanyakazi ya kifungu cha 12.

Lakini kazi watakayoifanya ni ile ya *secretariat*, yaani kuchagua wanafunzi ambao wanasifa za kupewa na hao ni Makatibu Wakuu kutoka sehemu mbali mbali pamoja na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sasa vifungu viwili hivi vinagongana, kwa sababu hiki kimoja ni kamati ya bodi, lakini kazi zilizopo kwenye kifungu cha 12 ni kazi ya *secretariat*, kweli Makatibu Wakuu wa wizara tatu, yeye mwenyewe wa Wizara ya Elimu pamoja na Mwakilishi atakayekwenda pale watakaa na fomu za kuchagua wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kupatiwa ufafanuzi kwa sababu hii ni kazi ya *secretariat*, hawa ni waamuzi waliofanya maamuzi ya kwamba tuchague wanafunzi wenye sifa hii. Sasa kazi ya kuchagua mwanafunzi mmoja mmoja kwamba huyu ndiye anayefaa ni kazi ya *secretariat*, lakini imetajwa hapa na wasi wasi huu niliuonesha tokea kwenye mchango. Kwa hivyo, sasa naomba kupata ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16 (4) kinasema kwamba Mkurugenzi na maafisa wengine wa Bodi wataunda Kamati Tendaji ya Bodi na hawa ndio watakaofanyakazi za siku kwa siku na bila ya shaka Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio watakaozipokea zile fomu na wanazo wao na lazima wazifanyie uchambuzi na baadaye ndio wanazipeleka kwenye Kamati ya Bodi.

Kwa hivyo, Kamati ya Bodi ndipo inatizama yale mapendekezo yaliyoletwa na ile Kamati Tendaji na itakapokubaliana nayo ndio yanakwenda kwenye bodi yenyewe, kwa ajili ya uamuzi na kuangalia uwezo wao wa kifedha na hivyo ndivyo tulivyokusudia. Kwa maana hiyo, hii Kamati Tendaji ndio tunaiona kama ni *secretariat*, ambayo itakuwa inafanyakazi za kila siku na inakuwa chini ya Mwenyekiti wake ambaye ni Mkurugenzi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri ananichanganya, kwa sababu kama kazi ya Kamati Ndogo ile ni kupitia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Tendaji kwa nini haikutajwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba ukae kidogo kwa ajili ya kufanya utaratibu kwa sababu muda wetu unamalizika.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kukamilisha shughuli iliyombele yetu, basi naliomba Baraza lako tukufu liridhie kuongeza muda, kwa ajili ya kumaliza shughuli iliyombele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wanaokubalia na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Katibu utaratibu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, sasa nitasema kwa ufupi kidogo, nilivyokusudia kusema ni kwamba kwa nini Mhe. Waziri katika mswada huu asiandike tu moja kwa moja kwamba kazi hizi za kifungu cha 12 ni kazi ya Kamati Tendaji kama alivyoitaja yeye mwenyewe, lakini kazi ya Kamati ya Ndogo iliyoundwa ni kupitia mapendekezo yote yaliyotoka kwenye kamati Tendaji ingekuwa *very simple*.

Kwa kweli hivi ilivyo naona kama inajizonga kwa sababu hizi kazi za Kamati Tendaji zimewekwa hapa kwa maana ya kazi za ile Kamati ya Ndogo na halafu kazi za Kamati Tendaji hazikuelezwa pahala *by implication* vile vile kwamba wao watafanyakazi za *office*.

Kwa hivyo, naomba pafanywe marekebisho, ikiwa Mhe. Waziri atakubali kuwa kifungu cha 12 kitafanyiwa marekebisho na iwe kazi za Kamati Tendaji, kazi za Kamati ya Ndogo ni kupitia mapendekezo yote yaliotoka kwenye Kamati Tendaji na kazi nyenginezo watakazopewa, basi mimi niko tayari kukubaliana naye.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mjumbe anakubaliana na mawazo yangu, isipokuwa sasa anataka iandikwe. Hali hiyo, nawaomba wanasheria wanisaidie kwa utaalamu wao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama tunakubaliana na kama Mhe. Waziri amesema kwamba tunakubaliana. Kwa hivyo, ni kuandika tu kubadilisha hizi kazi nadhani za Kamati Tendaji, kwa sababu huku haikutajwa

hasa isipokuwa imetajwa Mkurugenzi na maafisa wengine wa Bodi wataunda Kamati Tendaji ya Bodi.

Sasa nadhani hapa kunahitaji marekebisho makubwa kama tutakubaliana vile Mhe. Mjumbe anavyosema, ili tuweze kuona kwamba Kamati Tendaji wanafanyaje na Kamati yenyewe iliyoundwa hapa kwenye kifungu cha 12 inafanyakazi vipi. Kwa hivyo, tukeshakubaliana hapo basi tunaweza kurekebisha tu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa hiyo marekebisho yamekubaliwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana sana na Mwanasheria Mkuu yeye ameliona hilo suala na ninamuomba Mhe. Waziri akubaliane na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina hoja kwa sababu nilisema haya marekebisho nayapendekeza nataka msaada wa Mhe. Mwanasheria Mkuu na tayari ameshatoa msaada wake basi nakubali. *(Makofi)*

Kifungu cha 12

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa majukumu ya Kamati ya Elimu moja ni kuchagua wanafunzi ambao wanasifa na kupewa mkopo wa Elimu ya Juu kwa Vyuo tofauti. Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba huyu mjumbe mmoja anayewakilisha Vyuo Vikuu kwa nini naye asiingizwe hapa na sehemu hii ndio yenye matatizo na tukamuacha kwenye shughuli za bodi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akubaliane na mjumbe huyu naye aingizwe kwenye Kamati hii ya Elimu kwa sababu hapa ndipo panapochambuliwa hizi fomu, kwa hiyo aingizwe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, pendekezo lake sibaya lakini hiyo Kamati ya Elimu tutaifanya kubwa wakati ndio inaingia kwenye Kamati Kuu ya Bodi na uamuzi utakuja kuwa mgumu kufanyika, kwa sababu watakuwa wameshawazidi wale. Kwa kweli ilikuwa tuizingatie hiyo, kwa sababu kuna matatizo ya kuwa hawa huku wengi kuliko waliobakia kuingia katika ile bodi yenyewe, yaani itakuwa uamuzi hauwezi kupatikana vizuri.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa mtu kutoka kwenye vyuo naona ni bora tukapunguza kama Mhe. Waziri ataona wajumbe wako wengi, basi atafute wajumbe wengine wa kupunguza, ili tumuingize huyu kwa ajili ya uwakilishi wa wanafunzi upate nafasi katika sehemu hii muhimu ya uchambuzi, ambayo mara nyingi ndio inayolalamikiwa.

Kwa hivyo, kama atahisi kwenye Kamati ya Elimu kuna wajumbe wengi, nadhani kuna wajumbe wengine wanaweza kupunguzwa kama vile hawa Makatibu Wakuu, ili apate nafasi ya kumuingiza huyu, kwa sababu mjumbe huyu ni mdau muhimu sana katika suala hili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ilipoandikwa hii sheria lilizingatiwa suala hilo na kuonekana kwamba hawa watu wakitiwa hapa ndio yale malengo ya MKUZA na *Vision* 2020 yatapatikana, kwa kweli hakuna mtu ambaye utaona umuondoe kwa ghafla hivi sasa. Sasa sitaki kusema Mwakilishi, kwa sababu naye anao umuhimu wake kuwemo huko ni vizuri tuwe naye kwani anawakilisha wengi zaidi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nadhani amtafute mmoja ambaye anasimamia sera katika hawa, yaani amtafute mjumbe mmoja miongoni mwa hawa ambao wanalingana kwenye masuala yao hata kama ikiwezekana Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi abakie kwenye bodi.

Lakini hapa kwenye uchambuzi awaingize hawa watu wa Vyuo Kikuu au amtafute mwengine ambaye anasimamia masuala ya sera, ili kuona huyu kuwa tunamuingiza. Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu huyu ni mtu muhimu sana katika eneo hili na wala tusimuache nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nikiwatizama hawa wa kumpunguza simjui, lakini kama Baraza litasema tumpunguze Mwakilishi na tukikubaliana basi hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, limekubaliwa hilo. Tuendelee.

Kifungu cha 12 Majukumu ya Kamati ya Elimu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13 Kamati nyenginezo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 14

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tatizo langu ni dogo sana nafikiri tutakubaliana haraka sana na Mhe. Waziri. Wakati nilipokuwa nikichangia nilionesha wasi wasi wangu kuhusu muundo wa hii Kamati ya

Elimu nikasema kama ni robo tatu kwa mujibu wa idadi yao watu sita, robo tatu haitawezekana maana itakuwa ni nne na nusu.

Kwa hivyo, nadhani ni marekebisho tu, labda tutumie lugha nyengine ambayo itagawika ambapo hakutokuwa na nusu mtu. Sasa wakati alipokuwa akitoa ufafanuzi Mhe. Waziri sikusikia, kwa hiyo naomba hilo tu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama watu ni 6 basi robo tatu ni watu wane. Kwa kweli tutegemee zaidi kwa sababu hivi sasa ndio tunaanza na kama ulivyosikia hoja za Wajumbe inabidi tuongeze watu baadaye na hii ikibakia hatuji kuifanyia marekebisho tena. Kwa hivyo, ni vizuri ikiwa anataka kusema iwe nusu na hilo ni suala jengine, lakini sisi tuliona kwamba ndio tunaanza bila ya shaka wajumbe watakuwa wanaongeza humu.

Kutokana na hali hiyo, basi tunaweza kutoka kwenye robo tatu na kwenda kwenye thuluthi mbili. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tuendelee.

Kifungu cha 14 Mwenendo wa Kazi za Kamati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 15 Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 16

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu alikisoma Mhe. Waziri kabla ambacho ni kifungu cha 16 (4) kinachoelezea kuhusu Mkurugenzi pamoja na Wajumbe wengine wa Bodi wataunda Kamati Tendaji ya Bodi na katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe wengine walikuwa na wasi wasi kwamba hizi kamati zinakuwa nyingi.

Sasa Mhe. Waziri wakati alipokuwa akimjibu Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kwamba hii ndio itakuwa ni *secretariat* na wala sina tatizo kuwa hii ni *secretariat*, isipokuwa nina tatizo na hii lugha ya Kamati Tendaji. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tayari kuna kamati huku tumeshaipitisha katika kifungu cha 11 na 12. Lakini ukisoma mswada wa Kiingereza hakujaundwa kamati ambapo tumeambiwa mswada wa kiingereza ndio *authentic*. Kwa hivyo, naomba kunukuu.

> "*The Director and other office of the board shall constitute the Management Team of the board*".

Mhe. Mwenyekiti, *Management Team* si Kamati Tendaji hasa, kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri atuwekee sawa kidogo hapo kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tukizungumzia Kamati Tendaji pia tunazungumzia utaratibu wake pamoja na Mwenyekiti wake. Lakini tukizungumzia *Management Team* tu, kwamba ni utaratibu wa kawaida kwamba kuna *secretariat* ambayo inaongoza shughuli za kila siku.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atuwekee sawa kidogo ni Kamati Tendaji au ni *Team* ya Uendeshaji iliopo katika Bodi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Lugha ya Kiswahili inaeleza ni Kamati Tendaji na kweli kwenye Kiingereza imeandikwa *Management Team*, nadhani wanasheria walikusudia Kamati Tendaji. Mhe. Mwenyekiti, naomba wanasheria wanisaidie na hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, inavyoonekana kwenye kifungu cha 4 kwamba tunakusudia hapa kuunda *secretariat.* Mimi nadhani kwa kuweka sawa niseme kwamba Mkurugenzi na Maafisa wengi wa Bodi wataunda *secretariat* ya bodi, nadhani ndio itakaa sawa.

Kifungu cha 16	Kazi za Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 17	Kuanzishwa kwa Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 18	Malengo ya Mkopo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 19	Masharti ya Mkopo wa Wanafunzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20	Sifa za Kupata Mkopo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 21	Masharti ya Mkopo pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 21(2) ambacho kamati pia ilikifanyia marekebisho, lakini bahati mbaya kamati imefanya marekebisho madogo tu, kama neno “mdhamini” lisomeke “wadhamini”.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa najaribu kui-*capture* ile dhana nzima nikisoma Kiingereza, kuna vitu kadhaa ningependekeza tuvirekebishe katika maandishi. Kwanza kuna neno pale katika mstari wa mwanzo “italazimisha”, sio lugha nzuri ya kisheria. Mimi nilikuwa nadhani lingetumika neno “itataka”,

kwa sababu nilikuwa najaribu kutafuta neno *shall* lililokuwa katika Kiingereza, kwa sababu ukisema itataka, tayari itakuwa inalazimisha, haina haja tena kutumika neno kulazimisha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna neno ambalo linaachwa katika mstari wa tatu kwenye Kiswahili ambalo linashindwa kuunganisha maeneo mawili, labda nisome yote ili iweze kueleweka. Bodi itakapokuwa inatoa mkopo kwa mwanafunzi yeyote, itataka kwa mapendekezo yangu mimi, kuwepo kwa mdhamini au wadhamini wa kudhamini mkopo wowote utakaotolewa kwa mwanafunzi, halafu inaendelea hapo hapo, endapo mwanafunzi atashindwa kurudisha mkopo.

Sasa hapo palikuwa na neno liongezeke hapo, kwamba utakaotolewa kwa mwanafunzi, ambapo endapo mwanafunzi atashindwa kurudisha mkopo, halafu iendelee. Pia baada ya kurudisha mkopo koma, kuna neno limeingia pale "na", hili neno linapaswa litoke, likibakia neno "na" linaharibu maana nzima, linapaswa lisomeke kwamba endapo mwanafunzi atashindwa kurudisha mkopo, mdhamini yeyote atalazimika kulipa na kurudisha mkopo wote aliopewa mwanafunzi pamoja na riba linalotokana na limbikizo la deni.

Pia kuna marekebisho nataka yaongezwe, kwa Kiingereza inasema *I shall be notify to the guarantor or guarantors by the body*. Kwa hivyo, ilipaswa pia Kiswahili imalizie pale kwamba riba linalotokana na limbikizo la deni kama atakavyopewa taarifa na bodi, yaani huyo mdhamini atakapopewa taarifa na bodi juu ya hayo malimbikizo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka marekebisho hayo, moja pale kwenye mstari wa mwanzo kulazimisha lisomeke itataka. Pili mstari wa tatu baada ya neno kuwa mwanafunzi liongezeke neno "ambapo". Halafu mstari huo huo kule mwisho lile neno "na" kabla ya neno "mdhamini" liondoke na mwisho sentensi ikamilike kama ilivyokuwa katika Kiingereza yaongezwe maneno "kama atakavyopewa taarifa na bodi". Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakubali.

Kifungu cha 21	Masharti ya Mkopo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22	Wajibu wa Mkopaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23	Wajibu wa Muajiri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24	Ulipaji Mkopo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25	Wajibu wa lazima wa Mkopo pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 26	Majukumu ya Muajiri na Mdhamini pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 27	Adhabu.
Kifungu cha 28	Fedha na Mapato ya Bodi.
Kifungu cha 29	Makisio ya Mwaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 30	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pia marekebisho ya lugha pana tafsiri sahihi zilizomo katika miswada miwili hii.

Kifungu cha 30 (4) Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kifungu cha 30 (4) kinasema hivi:-

"*The audited accounts in the ouditers reports on such account shall be submitted to the board not later than three mounth after the end of the financial year to which they relate"*

Haya maneno ya mwisho hayapatikani katika tafsiri ya Kiswahili. Kwa hivyo, nilikuwa napendekeza isomeke, hesabu zilizokaguliwa na ripoti ya ukaguzi ya hesabu kwanza zitawasilishwa, sio itawasilishwa kwenye bodi sio zaidi ya miezi mitatu baada ya, sasa haya maneno kukamilika ukaguzi wa mwaka nilikuwa nayapendekeza yaondoke. Badala yake isomeke sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha, ambapo ukaguzi huo unahusika, itakuwa ina tafsiri sawa sawa na yale maelezo yaliyoandikwa kwa Kiingereza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye.

Kifungu cha 30	Hesabu za Kodi na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 31	Kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 32	Kufuta na Kubakiza pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubaliana pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mkono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2011

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu Juu ya mwaka 2011, usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwanza natoa shukrani kwa kazi kubwa tuliyoifanya tangu asubuhi hadi hivi usiku na kuweza kuongeza muda, ili kazi yetu iweze kukamilika kama ilivyotakiwa. Kwa hivyo, nakushukuruni sana na naahirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Alhamisi tarehe 24/03/2011 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa2:00 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/03/2011 saa 3:00 za asubuhi)